# UONGOZI WA KIDINI

## MAELEKEZO NA UTEKELEZAJI WA KIJAMII

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul-Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na::**
Alhaji Hemedi Lubumba Selemani

ترجمة

# القيادات الدينية

## الخطاب والأداء الاجتماعي

تأليف

حسن بن موسى الصفار

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

© **Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN No: 978 - 9987 – 17 – 039 – 5**

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul-Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Januari, 2014
Nakala: 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** w.w.w.alitrah.info

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji .......... 01
Utangulizi .......... 02
**Faslu ya Kwanza: .......... 08**
Nafasi ya Uongozi na Uhalali wa Kukosolewa .......... 08
Maulamaa wa Kidini Baina ya Utukufu na Ukosoaji .......... 08
Mwanachuoni na Mabadiliko ya Mazingira ya Jamii .......... 19
Marjaa wa Kidini na Utaifa .......... 28
**Faslu ya Pili: .......... 39**
Maelekezo ya Kidini, Changamoto naVipaumbele .......... 39
Maelekezo ya Kidini na Utandawazi .......... 39
Kuendana naWakati .......... 44
Ubinadamu wa Maelekezo ya Kidini .......... 51
Ni kutengeneza Matatizo au ni Kuleta Ufumbuzi? .......... 56
Vipaumbele vya Kuwasilisha Katika Maelekezo ya Kidini .......... 61
Maelekezo ya Kidini na Changamoto za Ndani .......... 68
Marekebisho ya Kitamaduni na Namna ya Kuishi na Watu .......... 77
Hotuba ya Kidini naVipengele vyaUfanisi .......... 83
**Faslu ya Tatu: .......... 102**
Utekelezaji wa Kijamii, Mtazamo na Unyoofu .......... 102
Mwanachuoni wa Kidini Baina ya Unyenyekevu na Kujikweza .......... 102
Tunda la Elimu ni Unyenyekevu .......... 114
Zaka ya Elimu .......... 128
Jamii na Maulamaa wa Kidini .......... 138
Nyanja Zingine za Kazi ya Kidini .......... 145

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, *al-Qiyadutu 'l-Diniyyah, al-Khitab wa 'l-Ada'u '-Ijtima'i.* Sisi tumekiita, *Uongozi wa Kidini: Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii.*

Kitabu hiki kinazungumzia uongozi, hususan uongozi wa kidini. Uongozi katika shughuli yoyote ni muhimu sana ili kufanikisha malengo yake na kufikia ufanisi wa hali ya juu na kuweza kuwanufaisha wale wanaoongozwa. Katika kitabu hiki mwandishi anajaribu kuelezea umuhimu wa uongozi na viongozi katika jumuiya na taasisi zetu za Kiislamu, hali ya uongozi wa zamani na uongozi mzuri unaotakikana kwa sasa bila ya kuvuka mipaka ya dini. Na hii ana maana ya kufuata kanuni na maadili ya Uislamu kama ilivyoainishwa katika Qur'ani Tukufu na Sunna.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ikiwa ni pamoja na sayansi na tekinolojia, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutoka na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Sheikh Abdulkarim Juma Nkusui kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kwa lugha ya Kiswahili; pia wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

# UTANGULIZI

## KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wavi-umbe. Ewe Mungu Wangu mteremshie rehema na amani Mu-hammad mwisho wa Manabii na hitimisho la Mitume, na kizazi chake kitwaharifu kitukufu, na Masahaba zake wema.

Mwanadamu katika zama hizi amekuwa ni mwingi wa maarifa na uelewa, kiasi ambapo maalumati mengi na taarifa mbalimbali kuhusu jambo lolote kati ya mambo au kadhia yoyote kati ya kadhia muhimu zinapatikana kwake, na duara la siri na la mambo yasiyo-julikana limekuwa dogo sana, hadi mazungumzo na vikao maalum-vya matapeli wa kisiasa wa Kimataifa zimeshapata njia ya kuvuja na kusambaa kupitia mtandao wa *WikiLeaks*[1] na mingineyo.

[1] **WikiLeaks** ni Shirika la Kimataifa lisilokuwa la kibiashara ambalo huchapisha taarifa na habari za siri, na kuvujisha habari na taarifa hizo kutoka kwenye vyanzo vya siri visivyoju-likana. Lilizindua tovuti yake kwenye Intaneti mwaka 2006 chini ya jina la *Sunshine Press* na likadai kuwa lina nyaraka za siri zaidi ya 1.2 ilizozipata ndani ya mwaka mmoja tangu kuanza kwake.

*WikiLeaks* inaeleza kuwa waanzilishi wake ni mchanganyiko wa wapinzani miongoni mwa Wachina, waandishi wa habari, wanahisabati, wanovisi, mafundi wa makampuni yanayo-fanya kazi nchini Marekani, Taiwan, Ulaya, Australia na Afrika Kusini. Na mkurugenzi wake ni Julian Assange, mwanaharakati wa Intaneti wa Australia.

*WikiLeaks* ilichapisha nyaraka ya kwanza mnamo Desemba 2006, nyaraka iliyoonesha ua-muzi uliotiwa saini na Sheikh Hassan Dahir Aweys, wa kuwateka na kuwauwa maafisa wa Somalia. Mnamo Agosti 2007 gazeti la '*TheGuardian'* lilichapisha habari zilizotolewa na WikiLeaks kuhusu ufisadi wa familia ya aliyekuwa Rais wa Kenya Daniel Arap Moi.

Mnamo Novemba 2007 ilichapisha nakala ya taratibu za uendeshaji wa kambi ya Delta ikiwa na maelezo kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Jeshi la Marekani katika kambi ya Guantanamo Bay yaliyotolewa Machi 2003, ambapo nyaraka hiyo imebainisha kwamba kulikuwa na marufuku ya baadhi ya wafungwa kufanya mahojiano na Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu, madai ambayo yalikuwa yamepingwa vikali na jeshi la Marekani.

Mnamo mwezi Februari 2008, *WikiLeaks* ilichapisha ripoti juu ya shughuli haramu ya Benki ya Uswisi ya Julius Baer katika visiwa vya Cayman, na hatimaye benki iliwasilisha kesi dhidi ya *WikiLeaks* huko Marekani, na kupokea amri ya mahakama yenye kupiga marufuku matumizi ya tovuti ya wikileaks.org.

Mnamo Januari 2009 *WikiLeaks* ilichapisha mazungumzo 86 ya simu kutoka kwa wanasiasa na wafanyabiashara kutoka Peru waliohusika katika kashfa ya mafuta ya Peru mwaka 2008. Mnamo Aprili 2010, *WikiLeaks* iliweka katika tovuti ya internet inayoitwa *Collateral Murder* video ya shambulio la ndege lililofanywa mwaka 2007 na vikosi vya Marekani na kuua kundi la raia wa Iraq wasio na hatia ikiwa ni pamoja na waandishi wa habari.

Kisha mnamo Julai 2010 *Wikileaks* ilivujisha Shajara ya Vita vya Afghanistan, Shajara ambayo ni mkusanyiko wa nyaraka zaidi ya 76,900 zinazohusu vita vya Afghanistan, nyaraka za siri ambazo hapo kabla isingewezekana umma kuzipitia na kujua ukweli.

Kisha mnamo Oktoba 2010 *Wikileaks* ilivujisha seti ya nyaraka 400,000 zilizojulikana kama Kumbukumbu ya Vita vya Iraq, hiyo ilikuwa ni kwa kushirikiana na mashirika makubwa ya kibiashara ya vyombo vya habari, ambapo iliyaruhusu kutoa mawazo kuhusu vifo vilivyotokea huko Iraq na kwenye mpaka wa Iraq na Iran.

Mnamo Novemba 2010 *WikiLeaks* alianza kufichua nyaraka za kidiplomasia za Wizara ya mambo ya nje ya Marekani. Mnamo Aprili 2011, *WikiLeaks* alianza kuchapisha nyaraka 779 za siri zinazohusu unyanyasaji na ukiukwaji wa haki za binadamu wanaofanyiwa wafungwa walioko kizuizini katika Gereza la Guantanamo Bay. Na mara *WikiLeaks* ikaanza kupokea sifa na shutuma kwa wakati mmoja. Na ilishinda idadi kadhaa ya tuzo ikiwa ni pamoja na tuzo ya mwaka 2008 ya ***Economist*** ya vyombo vipya vya habari, na pia tuzo ya mwaka 2009 ya Amnesty International ya vyombo vya habari vya Uingereza.

Baada ya kufichua siri kadhaa nzito hasa zinazohusu Marekani na unyama inaoufanya dhidi ya wanyonge duniani, Mkurugenzi wa *WikiLeaks* ambaye ndiye Mhariri mkuu wa mtandao huo aliwekwa kwenye orodha ya watu hatari wanaotafutwa na Polisi ya Kimataifa "*Interpol*", kwa maombi ya Mahakama moja ya Sweden kwa madai ya kosa la ubakaji, kwani Mahakama ya Stockholm ilikuwa imetoa hati ya Kimataifa ya kukamatwa kwa kisingizio kwamba mtuhumiwa anahusika katika ubakaji, unyanyasaji wa kijinsia na matumizi haramu ya nguvu katika tukio lililotokea Agosti 2010.

Hatimaye Julian Assange alikamatwa nchini Uingereza mnamo Desemba 7, 2010 chini ya Hati ya Kimataifa iliyotolewa na Mahakama ya Sweden kwa madai ya ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia. Marekani nayo ikatishia kumfungulia mashitaka Julian Assange ikiwa ni katika kukabiliana na kitendo cha tovuti ya *Wikileaks* kufichua maelezo ya siri ya kidiplomasia yaliyoitia aibu Marekani na washirika wake.

Mnamo Februari 2012, Mahakama ya Uingereza ikatoa Hukumu ya mtuhumiwa kukabidhiwa kwa Serikali ya Sweden ili kujibu mashtaka, lakini Julian Assange aliwasilisha pingamizi mahakamani ambalo lilikataliwa na Mahakama, hivyo akaamua kukimbilia Mahakama Kuu ya Uingereza, na mnamo Mei 30, 2012 nayo vile vile ikatoa hukumu ya mtuhumiwa kukabidhiwa kwa Serikali ya Sweden ili kujibu mashtaka, lakini ikasema: "Ana haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu mbele ya Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu."

Kupitia maendeleo ya teknolojia ya mawasilianao na kuwasiliana hakika inawezekana kusajili na kudhibiti kila neno linalotamkwa au kitendo chochote kinachotokea katika sehemu yoyote katika ulimwengu na inawezekana kulihifadhi na kulitoa wakati wa haja na litakapohitajika.

Mwanadamu leo amekuwa ni mwenye kuiamini nafsi yake zaidi, ambapo hashindwi kufikiria katika jambo lolote wala hasiti katika kutoa rai yoyote na msimamo wowote anaonufaika nao. Kama ambavyo umeongezeka ushujaa kwa mwandamu wa leo katika kutoa rai yake, ambapo utawala wa mabavu na ukandamizaji umetokomea na imewezekana kuvuka vikwazo vyake na udhibiti wake kwa kiasi kikubwa.

Na vituo vingi vyenye uwezo na nguvu katika jamii ya wanadamu vimepoteza sehemu kubwa ya haiba yake na vitisho vyake vya kimaada na kimaanawi ambavyo vilikuwa vinawatawala na kuwadhibiti walio pembezoni mwake na kuwazuia kukosoa, kupinga na kuasi.

Hata familia haiwezi tena kudhibiti watu wake kama ilivyokuwa katika wakati uliopita ambapo mke na watoto walikuwa wananyenyekea kikamilifu kwa baba wa familia.

---

Julian Assange hakukubali kwenda Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu na hivyo mnamo tarehe 19 Juni 2012 alikimbilia Ubalozi wa Ecuador huko London na kuomba hifadhi ya kisiasa. Rais wa Ecuador, Rafael Correa, aliahidi kupitia ombi hilo, na hivyo Ecuador ilijaribu kuzungumza na Uingereza na Sweden ili kuhakikisha Sweden inatoa hukumu ya haki kwa Assange, lakini haikufanikiwa, ndipo Rais wa Ecuador alipotangaza kuwa yeye atatoa maamuzi juu ya ombi la hifadhi ya kisiasa baada ya Michezo ya Olimpiki ya London. Uingereza ikasema kuwa inaweza kuvamia Ubalozi wa Ecuador Jijini London ili kumkamata Assange, jambo ambalo liliichukiza sana Serikali ya Ecuador, na kuchukuliwa kama tishio la shambulizi dhidi ya uhuru wao na ni ukiukwaji wa sheria za kimataifa. Na hatimaye mnamo Agosti 16, 2012 Waziri wa Mambo ya Nje wa Ecuador Ricardo Patiño alitangaza kuwa serikali yake imeamua kutoa hifadhi ya kisiasa kwa Julian Assange kwa kuzingatia hatari zitakazomkabili iwapo atakabidhiwa mikononi mwa Serikali ya Sweden. – Mhariri.

Uelewa juu ya haki umekua baina ya binadamu na sasa wanatilia umuhimu suala la kuneemeka na kuzitumia haki hizo katika maisha yao, katika sekta mbalimbali, na haki hizo zimekuwa ni zenye kulindwa kwa muundo wa kanuni, mikataba na makubaliano ya Kimataifa na rai ya jumla ya Kimataifa.

Kama ambavyo serikali, na hususan zisizokuwa za kidemokrasia zimekabiliwa na changamoto kubwa katika kuendesha utawala wake na udhibiti wake kwa wananchi wake.

Na kwa mtiririko huu tunafika katika kuzungumzia nafasiya uwezo wa kimaanawi unaopatikana katika taasisi za kidini na uongozi wa kiroho wa maulamaa, je wao hawaguswi na mabadiliko haya? Je, leo hii bado wana daraja lile lile ambalo walikuwa nalo wakati uliopita katika haiba na utukufu? Je, Maulamaa wa kidini na taasisi bado wangali ni sehemu yenye kulindwa na wala haiguswi na ukosoaji na upingwaji?

Ni sahihi kwamba nafasi ya dini imeongezeka katika jamii na kutokana na hilo imeongezeka nguvu ya maulamaa wa dini na kuathiri kwao, lakini hilo pia limepelekea wao kuangazwa, hivyo wako chini ya darubini ya uchunguzi, na kuna vituo na nguvu ambazo zinahisi ushindani mkubwa kutoka kwenye nguvu za kidini katika kutaka kutawala jamii, na hivyo zinakwenda mbio ili kuzidhoofisha nguvu za kidini na kuchukua nafasi yake na dauru yake katika jamii.

Kama ambavyo jamii ya kidini si jamii ya malaika, hivyo ni jambo la kawaida kupatwa na upungufu, kasoro na mianya, kama hali ilivyo katika kila jamii na katika utendaji wa kibinadamu. Katika safu ya maulamaa wa dini kumekuwa na mielekeo mingi, madhehebu mbalimbali, rai zinatofautiana na masilahi yamegongana, na bila shaka kuhitalifiana hakutaishia ndani ya jamii yao tu na wala haitowezekana kuficha tofauti hizo, bali kila upande unajitahidi

kuushinda upande mwingine kupitia jamii,  hiyo ni kwa sababu kupata kundi la watu ndio medani ya ushindani.

Na kinachoonekana ni kwamba kitendo cha baadhi ya maulamaa wa kidini kuwakoso amaulamaa wenzao nje ya duara la mjadala wa kielimu, ni kati ya mambo yaliyowashajiisha wengine na kuwapa ujasiri wa kushusha hadhi ya maulamaa wa kidini na kupaka matope shakhisiya zao.

Kutokana na yote yaliyotangulia hakika ni kawaida kuwepo na maswali na kupatikane ukosoaji na upinzani dhidi ya baadhi ya misimamo na utekelezaji wa taasisi za kidini na dhidi ya nyendo  na utendaji wa baadhi ya wanaojinasibisha na taasisi hizo. Na haiwezekani tena kukemea maswali haya na upinzani huu kwa onyo na kuhadharisha kwa waadhi, kama vile kusema kwamba  kuwasengenya maulamaa ni haramu, na kwamba mwenye kuwapinga ni sawa na kumpinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Kama ambavyo haisihi kupuuza hali ya ukosoaji na upinzani, kwa sababu kufanya hivyo itamaanisha kupanua wigo wake na kudhoofisha hali ya kidini na kupuuza nafasi ya maulamaa wa kidini na kusababisha ghadhabu kutoka katika kizazi kipya dhidi ya dini.

Na njia sahihi ambayo ni wajibu taasisi za kidini kuifuata ni kukubali ukosoaji na maswali kwa moyo mkunjufu na kuyachambua kimaudhui na kuyajibu kwa uwazi na kukiri sehemu za makosa na kwenda mbio kutatua na kusahihisha na kushajiisha ukosoaji wa dhati ndani ya jamii ya kidini, kwa kuanzia na maelekezo ya Nabii Mtukufu: “Zihesabuni nafsi zenu kabla hamjahesabiwa na zipimeni kabla hamjapimwa.”[2]

[2] Muhamaad bin Hasan al-Huru al-A’amiliy katika *Wasailus-Shiah*, Juzuu ya 16 chapa ya kwanza 1413 Hijiria Beirut-Muasasatu Aalil-Bait (as) lil-ihiyaai turaathi uk: 99 Hadithi namba  21082.

Ndani ya mtiririko huu imekuja fikira ya kuandika kitabu hiki kilichopo mbele ya msomaji mpendwa ambapo kinajadili baadhi ya mambo ambayo yanazungumzwa kuhusu maelekezo ya kidini nautendaji wa taasisi za kidini na nyendo za baadhi ya wanaojinasibisha nazo.

Nao ni mchango katika kujibu changamoto za baadhi ya maswali na ukosoaji, na kukabili baadhi ya ukosoaji wa dhati, ni mchango niliouandika katika nyakati tofauti tofauti kutokana na baadhi ya matukio na minasaba mbalimbali, nataraji kuchapishwa kwake kutakuwa na manufaa na faida, na ninamuomba Mwenyezi Mungu apokee hilo kwa mapokezi mazuri. Hakika Yeye anakubali machache na kusamehe mengi Naye ndiyeMwenye kuafiki na kusawazisha.

**Hasan bin Musa as-Saffar**
**8 Dhul-Qa'ad 1432 Hijiria/ 3 Oktoba 2011.**

# FASLU YA KWANZA

## NAFASI YA UONGOZI NA UHALALI WA KUKOSOLEWA

**Maulamaa wa Kidini Baina ya Utukufu na Ukosoaji:**

Hapana shaka kwamba uwepo wa kundi lililobobea katika elimu ya dini, na lenye jukumu la kubainisha dhana zake na hukumu zake kwa watu, ni jambo linalotakiwa na ni ladharura katika jamii yoyote inayo nasibiana na dini.

Na kwa kuongezea uwezo wa maarifa ambayo linakuwa nayo hili kundi – Maulamaa wa dini – hakika unawapa nafasi muhimu ya kijamii ambayo inaonekana katika kuilea jamii ili ijilazimishe kufuata maadili na tabia njema, na pia inaonekana kwa wao kuwa vielelezo na vigezo kwa watu, wanaiga kutoka kwao na wanajongea pembezoni mwao, jambo ambalo linatia nguvu mshikamano wa kijamii na umoja wake. Na kwa sababu hiyo Uislamu umewajibisha uwepo wa kundi hili ndani ya jamii za ummah kwa kiwango kinacholazimiana na nafasi yake na kazi yake, kwa namna ya wajibu wa kifai, anasema (swt):

۞ وَمَا كَانَ ٱلْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُوا۟ كَآفَّةً ۚ فَلَوْلَا نَفَرَ مِن كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَآئِفَةٌ لِّيَتَفَقَّهُوا۟ فِى ٱلدِّينِ وَلِيُنذِرُوا۟ قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوٓا۟ إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ ﴿١٢٢﴾

**"Wala haiwafalii waumini kutoka wote. Kwa nini kisitoke kikundi katika kila kundi miongoni mwao kujifunza dini na kuwaonya watu wao watakapowarudia, ili wapate kujihadhari."** **(Surat Tawba: 122)**.

Lakini kundi hili la– Maulamaa wa kidini- ni sehemu ya jamii na linapatwa na kukabiliwa na maradhi mbalimbali na upungufu ambao unaweza kumpata mtu yeyote katika wanadamu, hivyo wao wana-hali ya ubinadamu ambayo haiepukani na nukta za udhaifu, kasoro na makosa. Kwa sababu hiyo, hakika nususi za kidini wakati ambao zinalingania kuwaheshimu Maulamaa na kuwaenzi na kuchukua mafunzo kutoka kwao, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

فَسْـَٔلُوٓاْ أَهْلَ ٱلذِّكْرِ إِن كُنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٤٣﴾

**“Basi waulizeni wenye ukumbusho ikiwa nyinyi hamjui.”** **(Surat Nahli: 43).**

Ni wakati huo huo zinalingania kuwa macho na kuzinduka ili kusipenye katika kundi hili watu wenye kushukiwa na wenye kupotoka au yeyote kati ya watu mwenye kutumia nafasi yake na cheo chake kujinufaisha kwa gharama za misingi na maslahi ya jamii, na ili kosa ambalo linaweza kutokea kwa mmoja wao kwa kudhamiria au bila ya kukusudia, lisigeuke kuwa ni sehemu ya dini na sharia.

Na zimesimulia hadithi nyingi na riwaya zilizopokewa kutoka kwa Nabii (s.a.w.w.) na Maimamu watukufu (as) kuhusu wajibu wa kujihadhari na kujikinga kutokana na kuhadaiwa na Maulamaa wasio wema au kukubali yanayopingana na misingi ya dini kwa sababu ya kughushiwa na kupotoshwa. Kama ambavyo aya za Qur’aniTukufu ambazo zimezungumzia upotofu na upotoshaji wa baadhi ya maulamaa wa dini zilizotangulia miongoni mwa Mayahudi na Manaswara, zinaleta ujumbe wa kuwatahadharisha na kuwazindua watu wa ummah wa Kiislamu ili wachukue msimamo wa uelewa na uoni katika kuamiliana na hali hii wakati itakapotokea ndani ya maulamaa wa ummah. Na kati ya aya hizo tukufu ni kauli yake (swt):

وَإِنَّ مِنْهُمْ لَفَرِيقًا يَلْوُۥنَ أَلْسِنَتَهُم بِٱلْكِتَٰبِ لِتَحْسَبُوهُ مِنَ ٱلْكِتَٰبِ وَمَا هُوَ مِنَ ٱلْكِتَٰبِ وَيَقُولُونَ هُوَ مِنْ عِندِ ٱللَّهِ وَمَا هُوَ مِنْ عِندِ ٱللَّهِ وَيَقُولُونَ عَلَى ٱللَّهِ ٱلْكَذِبَ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٧٨﴾

**"Na hakika miongoni mwao kuna kundi linalopinda ndimi zao kwa Kitabu ili mpate kuyadhani hayo kuwa ni ya Kitabu wala si ya Kitabu. Na wanasema: Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu, na hali hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu; na wanasema uwongo juu ya Mwenyezi Mungu na hali wanajua." (Surat AaliImran: 78)**.

Aya inaweka wazi mchango wa baadhi ya Maulamaa wa Ahlul-Kitabu ambao wanazipa rai zao zinazotokana na matamanio yao na mielekeo ya kimaslahi iliyopotoka, sifa ya utakatifu wa kidini kana kwamba ni amri za kisharia, wanaingiza rai hizo katika mafunzo na katika aya za Kitabu cha mbinguni ili watu wadhani kwamba rai hizo zimeteremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kwa kulazimiana na maudhui na insafu hakika Qur'aniTukufu haikuhusisha tuhuma hii na maulamaa wote wa Kiyahudi na wa Kinaswara bali imewahusisha baadhi yao tu: **"Na hakika miongoni mwao kuna kundi."**

Na aya tukufu inaashiria kwamba kundi hili la Maulamaa lipo katika dini zote za Mwenyezi Mungu, lina mbinu mbalimbali za kupotosha ili watu wasigundue hiyana yao na upotoshaji wao katika maandiko matakatifu, kwa kuchanganya maneno yao na maandiko ya kidini:**"Na hakika miongoni mwao kuna kundi linalopinda ndimi zao kwa Kitabu,"**ambapo wanawasilisha maneno hayo ya uongo kwa njia ileile ambayo wanawasilisha maandiko matakatifu **"ili mpate kuyadhani hayo kuwa ni ya Kitabu"**ili watu wadhani kwamba hayo wanayoyasema ni sehemu ya dini.

Na wakati mwingine wanapotosha maandiko ya kidini kwa kuyapeleka kwenye maana nyingine isiyokusudiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu,[3]kama inavyosema aya nyingine:

يُحَرِّفُونَ ٱلْكَلِمَ عَن مَّوَاضِعِهِۦ ۙ وَنَسُوا۟ حَظًّا مِّمَّا ذُكِّرُوا۟ بِهِۦ ۚ ﴿١٣﴾

**"Wanageuza maneno kutoka mahali mwake na wakaacha sehemu ya yale waliyokumbushwa."** **(Surat al-Maidah: 13)**.[4]

## Hatari ya Kupotosha:

Hakika kati ya hatari mbaya sana ambayo inaikabili dini ni kuizushia uongo kutoka ndani, yaani kutoka kwa maulamaa wa dini ambao watu wanawazingatia kuwa ni rejea ya mafunzo ya dini na hukumu zake, hivyo wao wanawatolea watu fatwa na rai zinazokhalifu misingi ya dini na masilahi ya ummah kwa msukumo wa masilahi binafsi, kwa kutumikia masilahi binafsi au masilahi ya kundi au kwa kasumba ya kimadhehebu au ya mwelekeo fulani, na kunasibisha fatwa hizo na misimamo hiyo na dini na kuipa sifa ya taklifu ya kisharia.

Na tumeshaona katika zama zetu za sasa namna gani baadhi ya fatwa na rai zimesababisha kuenea mielekeo ya kigaidi yenye kutumia mabavu dhidi ya wasio na hatia, kuhalalisha damu zao na kuvunja heshima zao nje ya ummah na ndani ya ummah. Kama am-

---

[3] Kwa maelezo zaidi rejea kitabu **Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu**, kilichoandikwa na Sheikh Ja'far Subhani na kuchapishwa na Taasisi ya *al-Itrah Foundation*. Humo utaona jinsi baadhi ya ulamaa hasa wa tasnia ya historia, hadithi na tafsiri ya Qur'ani walivyotumia kalamu zao katika kupotosha dhana kadhaa za Uislamu, na mafunzo ya Mtume (s.a.w.w.) –Mhariri.

[4] Kwa nyongeza zaidi Mwenyezi Mungu anasema:

فَأَمَّا ٱلَّذِينَ فِى قُلُوبِهِمْ زَيْغٌ فَيَتَّبِعُونَ مَا تَشَٰبَهَ مِنْهُ ٱبْتِغَآءَ ٱلْفِتْنَةِ وَٱبْتِغَآءَ تَأْوِيلِهِۦ

**"Wale ambao nyoyoni mwao mna upotofu wanafuata zile za mfano kwa kutaka kuharibu na kutaka tafsiri yake…. (3:7) – Mhariri.**

bavyo tumeona uhamasishaji wa kibaguzi kwa anuani za dini kama vile kuhami itikadi, kulinda tauhidi, kuondoa bidaa, na kutetea madhehebu, na hatimaye tumeshuhudia yaliyozalishwa na miradi hiyo ikiwa ni pamoja na fitina, kusambaratisha ummah, mizozo na mapigano.

Na ndani ya madhehebu pia kunapatikana misuguano na hatimaye zinatumiwa fatwa za kidini baina ya pande zenye kutofautiana katika rai au masilahi, jambo ambalo linapingana na haki za udugu wa kiimani, na linapingana na hali ya kuheshimu haki ya ijtihadi na kutofautiana rai, na mwisho misuguano hiyo inaifanya jamii ya waumini kuwa ni uwanja wa mizozo na ugomvi.

Na katika sehemu nyingi imetokea baadhi ya watu wanaitumia dini katika misimamo na mielekeo ya kisiasa. Hakika matukio haya yenye kutia uchungu na yenye kusikitisha ni baadhi tu ya matokeo ya matendo mabaya yanayofanyika ndani ya jamii ya kidini kwa anuani na visingizio vinavyo nasibishwa na dini. Hadi inawezekana kusema: Hakika ndani ya kundi hili la Maulamaa wa kidini kuna kikundi badala ya kuchangia katika kutatua matatizo ya ummah kimekuwa ni chanzo cha matatizo magumu ya ziada, na wakati mwingine tunaona mizozo ya ndani ambayo imevuruga medani nzima ikiwazuia watu kujishughulisha na dini, na kusababisha ghadhabu mbaya dhidi ya dini na wanadini.

Na ikiwa mfano wa hali hii na mwonekano huu ni jambo linalotarajiwa kutokea, kwa sababu watu wa kundi hili – Maulamaa wa dini – sio malaika na wala sio maasumu, na hawako mbali na taathira za hali ya mazingira ya kijamii, basi hakika ni lazima kuwepo na vyombo vyenye kuzuia hali hiyo isitokee, na kuilinda jamii kutokana na athari zake mbaya. Na tutaelekeza mazungumzo juu ya baadhi ya vyombo na njia ambazo inawezekana kufaidika nazo katika kukabiliana na hali hii.

**Malezi ya Kimaadili:**

Seminari za Masomo ya Dini na shule za Kidini zinajikita sana na kutilia maanani suala la kuwaandaa wanafunzi wake kielimu kupitia masomo yake, na aghlabu zinapuuzia upande wa malezi ya kiroho na ya kimaadili, jambo ambalo linatoa mwanya wa kukua kwa hali ya umimi na ubinafsi, na kupenya mielekeo ya kimasilahi binafsi, na wakati mwingine wanafunzi hawa wanaokuja kwa ajili ya masomo huwa wametokea katika jamii isiyo nzuri au isiyokuwa na maandalizi ya kimalezi, kama ambavyo baadhi ya nguvu pinzani zinaweza kwenda mbio katika kupanda mbegu za ubinafsi ndani ya jamii ya watu wa elimu, au kwa sababu baadhi yao tayari wameathirika na hali hiyo.

Yote hayo yanasababisha dharura ya kutili amkazo, umuhimuna kutilia maanani upande wa malezi na maadili ya wanafunzi wa elimu ya dini. Na dharura hii imetiliwa mkazo na baadhi ya Marjaa wakubwa na Maulamaa na wamehadharisha kitendo cha kupuuzia hali hii, kama vile Shahidi wa pili Zainu Diyn al-Aamiliy aliyezaliwa 911-965 Hijiria, katika kitabu chake *Muniyatul-Muridi Fiy Adabil-Mufid Wal-Mustafid*, na Imamu Khomeni katika mihadhara yake juu ya jihadi kubwa, jihadi ya nafsi, na Marjaa Sayyid Shiraaziy katika kitabu chake *Ilaa WukalaainaFil-Bilaad*, na katika vingi kati ya vitabu vyake na mihadhara yake.

**Taasisi ni Hali ya Kidini:**

Hali ya elimu ya dini katika sehemu yake kubwa inakabiliwa na ukosefu wa mazingira ya kitaasisi, jambo ambalo linajenga mwelekeo wa ubinafsi kwa maulamaa wa kidini, hiyo ni kuanzia katika hatua ya mafunzo ambapo katika Seminari nyingi za Masomo ya Dini kwa Mashia, hazina mfumo rasmi unaofuatwa, bali mwanafunzi anachagua kwa uhuru wake, aina, sehemu, idadi ya masomo yake na wal-

imu wake wa kumfundisha, na wala hakuna yeyote anayemuuliza kuhusu kuhudhuria kwake au kutohudhuria kwake, wala hakuna muda maalumu uliopangwa wa kusoma kwake na kuhitimu kwake, au kuhama kwake kutoka hatua moja ya kielimu kwenda hatua nyingine.

Ni sahihi kwamba kuna ada na tamaduni zilizoenea ndani ya Seminari za Masomo ya dini, lakini sio lazima kuzifuata, na hususan kwa mtu mwenye kutaka kuziacha. Na pengine uhuru huu katika Seminari za Masomo ya dini unalandana na zama na nyakati zilizopita au ilikuwa ni kuyashinda majaribio ya baadhi ya mamlaka zilizotaka kuzitawala na kuzidhibiti Seminari za Masomo ya Dini, jambo ambalo liliwasukuma baadhi ya viongozi wake kunyanyua kaulimbiu ya kwamba: Hakika Seminari za Masomo ya Dini mfumo wake hauna utaratibu rasmi. Lakini nyakati zilizopo na mabadiliko yaliyopo katika maisha ya kijamii yanalazimisha uwepo wa kanuni zenye kuratibu hali ya Seminari za Masomo ya Dini na kuzilinda na kasoro na mmong'onyoko. Na mwelekeo huu umeanza kulazimisha uwepo wake, na hususan katika Seminari ya Masomo ya Dini ya Qum, kwani pamoja na kuwepo kizuizi (chenye kuzuia mmong'onyoko) bado ingali imesimama katika baadhi ya ada za zamani za kuiga.

Na mwanafunzi anaporejea katika jamii yake ili atekeleze wajibu wake wa kidini hakika huwa hafungamani na upande wowote au taasisi yoyote inayofuatilia uzoefu wake, si Seminari ya Masomo ya Dini ambayo huwa tayari imekata mahusiano naye, na wala si taasisi za ndani ya nchi yake, mara nyingi hali huwa hivyo. Hivyo huanza uzoefu wake peke yake na wakati mwingine anaweza kukabiliwa na hisia zisizokuwa nzuri kutoka kwa maulamaa waliomtangulia katika nchi yake kwa kumzingatia yeye kuwa ni mpinzani wao au anatofautiana nao katika baadhi ya mielekeo yake na mahusiano yake.

Yote hayo yanatengeneza mazingira ya kumea mielekeo ya ubinafsi, kujali masilahi binafsi na mienendo isiyokuwa ya tabia njema katika jamii zakidini.

Hakika uwepo wa uangalizi katika kila nchi kutoka kwa maulamaa wakubwa wa nchi husika kwa ajili ya kusimamia mazingira ya kidini humo, kwa kuwalea maulamaa wote na wanafunzi na kuwasaidia katika kutekeleza majukumu yao na wajibu wao, na kuwasaidia katika kutekeleza kazi zao na ujumbe wao, na kufuatilia mambo yao ya kimaisha na kuwaandalia mazingira ya kushauriana na kunasihiana baina yao, na kuwashajiisha juu ya kusaidiana na kukamilishana, hakika uwepo huo unasaidia sana kuvuka kasoro hizi na unawezesha kufaidika na vipaji na nguvu zilizopo, na hiyo inapeleka mbele hali ya kidini na kuiendeleza.

Kama ambavyo linalotarajiwa kutoka kwa Marjaa wa kidini ni kuweka utaratibu wa mawasiliano baina yao na Maulamaa na mawakala katika nchi na maeneo mbalimbali ili kufuatilia nyendo zao na utekelezaji wao, na kutoa maelekezo ya lazima katika kuondoa kasoro na makosa ambayo yanaweza kupatikana katika jamii yao, ili uhusiano usiishie tu katika duara la kuchukua haki za kisharia, kujibu mas'ala na kutoa fatwa.

**Kuilinda Jamii kwa Uelewa:**

Kuimarisha nafasi ya mwanachuoni wa kidini katika jamii ni jambo linalotakiwa, na watu kumheshimu ni kati ya mambo ambayo yamesisitizwa na nususi za kidini ili kuipa nguvu nafasi ya dini. Lakini kuwepo mwonekano mbaya ndani ya jamii ya kidini kunaleta hatari na madhara makubwa, na madhara yenye kujitokeza zaidi ni:

Kukosekana uhalisia wadini, na hivyo kusababisha baadhi ya watu kuikimbia dini kwa kuukasirikia mwonekano huu mbaya.

Watu kudanganyika kwa mifano isiyo mizuri ndani ya jamii hii, mifano hii inatoa fursa ya kuendelea kuwa katika makosa na kutumikia mielekeo yake ya kimakosa na kuwaongoza wafuasi wake katika njiayakimakosa.

Sekta ya dini hukabiliwa na mtikisiko, mkanganyiko na kujikuta ikishughulika zaidi na matatizo na misukosuko ya ndani.

Na kati ya mambo ambayo yanatudhihirikia kutokana na mfumo wa Qur'ani Tukufu na Hadithi za Nabii(s.a.w.w.) na riwaya zilizopokelewa kutoka kwa Maimamu Watukufu (as) ni dharura ya kuilinda jamii kwa uelewa, ili watu wasiamiliane na kila mwanachuoni wa kidini kwa utukufu na usafi wa moja kwa moja, na kumwamini kwa upofu bali ni lazima kutumia akili na kutafakari na kuwatazama watu, utendaji wao na nyendo zao kwa jicho la udadisi na uoni wa utambuzi. Kwani misingi ya dini iko wazi, na masilahi ya jamii yanajulikana kwa akili, na hakuna utukufu na usafi wa moja kwa moja kwa asiyekuwa maasumu.

Huu ndio ujumbe ambao aya hii tukufu inataka kuuwasilisha, aya ambayo inazungumzia ufisadi na upotovu wa baadhi ya maulamaa wa Ahlul-Kitabi, kama vile kauli yake (swt):

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِنَّ كَثِيرًا مِّنَ ٱلۡأَحۡبَارِ وَٱلرُّهۡبَانِ لَيَأۡكُلُونَ أَمۡوَٰلَ ٱلنَّاسِ
بِٱلۡبَٰطِلِ وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِۗ ٣٤﴾

**"Enyi mlioamini! Hakika wengi katika watawa na makuhani wanakula mali za watu kwa batili na kuwazuilia njia ya Mwenyezi Mungu."** **(Surat Tawba: 34).**

Hakika kuelekeza mazungumzo kwa wale walioamini ni ili kuwahadharisha wao, kwa kuwa mfano wa hali hii itatokea katika taba-

ka lao la kidini. Kama ambavyo kuna idadi kubwa ya Hadithi na riwaya ambazo zinahadharisha juu ya Maulamaa waovu. Imepokewa kutoka kwa Nabii (s.a.w.w.) kwamba amesema: “Ujihadhari ummah wangu na Maulamaa waovu.”[5] Na imekuja kutoka kwa Imamu Musa bin Ja’far (as) kwamba: “Hakuna elimu isipokuwa kwa mwanachuoni mchamungu, na kumjua mwanachuoni ni kwa kutumia akili.”[6] Yaani hakika ni juu ya mwanadamu kutumia akili yake ili kuwatathimini maulamaa, na kumjua anayefaa miongoni mwao na kumfuata, na kupembua maelekezo yao.

**Ukosoaji Wenye Kujenga:**

Kunyamazia makosa kunayafanya yazidi kuongezeka na kujirudia, na kosa linaweza kutokea kwa sababu ya mtendaji wake kughafilika au kukanganyikiwa, hivyo kuwepo kwa watoa nasaha wenye kukosoa kunapelekea kuacha kosa, kama ambavyo kitendo cha mtu yeyote kuhisi kwamba anakabiliwa na ukosoaji na kwamba kazi zake zinaangaliwa na kutathminiwa kinamfanya awe mwangalifu zaidi na mwenye kudhibiti nyendo zake kwa kuchunga heshima yake na nafasi yake.

Na kati ya matatizo ya sekta zetu za kidini ni kukataa kukosolewa na kumchukulia mkosoaji yeyote kwamba yuko dhidi ya dini na ni mpinzani wa hali ya kidini, na kuzingatia kuwa ukosoaji ni sababu ya kudhoofisha nafasi ya maulamaa na kuporomosha heshima yao na ni kutimiza malengo ya maadui wa dini na ummah.

Fikira hii sio sahihi na haikubaliki, kwa sababu ni kinyume na mfumo wa Qur’ani na nususi zingine za kidini, na ni kinyume na

[5] Alaau Diyn Ali al-Mutaqiy al-Hindiy katika *Kanzul-Umaal*chapa ya tano 1985 Beirut Muasasatu Risaalati Hadithi namba 29084.

[6] Al-Haji Miriza Husain Nuuriy Twabarisiy katika *Mustadrakul-Wasaail*, jz. 11, chapa ya tatu 1412 Hijiria Beirut, Muasasatu Aalil-Bait lihiyaai turathi uk. 258 Hadithi namba 12926.

mantiki ya akili. Ukosoaji na upinzani ni moja ya sababu za kugundua kosa na kupelekea kulisahihisha katika sekta yoyote ile. Na bila shaka sekta yetu ya kidini inahitaji zaidi ukosoaji wenye kujenga, kwani ndio badali sahihi kuliko kuleta kejeli na ushabiki baina ya pande zinazohitalifiana, ukosoaji huo ndio unaotoa fursa ya mageuzi na maendeleo kuelekea kwenye hali bora zaidi.

Hakika mwanachuoni wa kidini ni wajibu wake awashajiishe wale wanaomzunguka kukosoa na kutoa mtazamo wao, ili afaidike kutokana na ukosoaji wao katika kujirekebisha mwenyewe na kufanikisha jukumu lake, na si kulazimisha ubabe na vitisho ambavyo vinawazuia kutoa rai zao na msimamo wao. Imepokewa kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alipoona bedui amemuogopa yeye (s.a.w.w.) alimwambia: "Tulia, hakika mimi ni mtoto wa mwanamke aliyekuwa anakula nyama huko Makka."[7]

Bali ni juu ya mwanachuoni wa kidini aweke ratiba ya kuwashirikisha watu pamoja naye katika kutoa maamuzi na kuendesha mambo ya kidini ambayo anayasimamia, na awe na uvumilivu mbele ya ukosoaji na upinzani, kwani Mwenyezi Mungu amemwamrisha Mtume Wake Muhammad (s.a.w.w.) pamoja na umaasumu wake na ukamilifu wake awatake ushauri waliopo pembezoni mwake, anasema (swt):

وَشَاوِرۡهُمۡ فِي ٱلۡأَمۡرِۖ ﴿١٥٩﴾

**"Na ushauriane nao katika mambo."** **(Surat Aali Imrani: 159)**.

Na kwa upande mwingine, hakika ni juu ya wenye uelewa sahihi kati ya wanajamii kutokusita kuwasilisha ukosoaji wao na kutoa mao-

[7] Muhammad bin Abdillahi al-Hakim Nisaaburiy katika *al-Mustadraki Alaa Sahihain* Juz. 2 chapa ya kwanza 1311 Hijiria (Beirut Darul- Kutubi al-Ilimiyati) uk. 506, Hadithi namba 3733.

ni yao kwa maulamaa wa kidini na kuwadhihirishia rai zao zenye ukosoaji, maadamu tu lengo ni kutengeneza na kulinda masilahi ya dini.

## MWANACHUONI NA MABADILIKO YA MAZINGIRA YA JAMII

Inatofautiana hali ya jamii za Kiislamu kwa kutofautiana nchi ambazo wanaishi humo na mazingira ambayo wananasibiana nayo, ambapo zinatofautiana hali ya serikali zao na mazingira yao ya kisiasa, kuna mazingira ya kisiasa yaliyo tulivu, na kuna ambayo si tulivu, kuna serikali zinazotoa fursa ya kushiriki kisiasa na uhuru wa kufanya harakati na kutoa maoni, na kuna nyingine ambazo chini ya utawala wake hakuna fursa hiyo, na pia inawezekana serikali ikawa ni yenye kushikamana na misingi ya Kiislamu na sharia yake, na inawezekana ikawa ni ya Kimagharibi yenye kupiga vita dini au isiyofungamana na upande wowote. Kama ambavyo pia nyakati mazingira na hali za kijamii zinatofautiana kwa upande wa maingiliano, au aina ya watu na dini zao, na kwa upande wa uwiano na utulivu katika uhusiano wa pande mbalimbali katika nchi moja.

Na kuna tofauti katika kiwango cha utamaduni, ada na mazoea yaliyotawala katika jamii. Kama ambavyo mazingira ya kimaisha na kiuchumi yaliyo tofautiana huakisi na kuathiri fikra na tabia katika jamii, na hivyo kuna tofauti ya kifikra na kitabia baina ya jamii yenye kuendelea na ile isiyoendelea, baina ya jamii ya kilimo na ile ya kiviwanda, baina ya jamii inayoishi katika hali ya utajiri na wasaa wa kimali na ile nyingine yenye kukabiliwa na matatizo na ukata wa kiuchumi.

Tofauti hizi za mazingira na hali za jamii zinazalisha tofauti katika aina za changamoto na matatizo ambayo yanaikabili jamii, na

wakati changamoto hizi na matatizo haya yanapohitaji utatuzi wa kisharia na maelekezo ya kidini basi hakika wanachuoni wa fiqhi wao ndio upande unaorejelewa na unaokimbiliwa kwa ajili ya kuchukua hukumu za kidini na rai ya kisharia katika shida na matukio yenye kujitokeza.

Wakati ambapo katika baadhi ya jamii inawezekana hakuna wanachuoni wa kifiqhi kutoka ndani ya jamii hizo, wanajamii huamiliana na changamoto zinazowakabili na hutambua moja kwa moja taathira za mazingira mbalimbali ya maisha yao, na hakika wakatihuo ima waishi maisha ya kukosa na kutopata utatuzi na ufumbuzi wa kisharia unaohusu matatizo na changamoto zinazowakabili, na ima wakimbilie kwenye rai na maoni ya wanachuoni wa kutoka nje ya jamii yao na mazingira yao.

Na hapa kunaweza kujitokeza mushkeli unaohusiana na upeo wa uwezo wa mwanachuoni wa fiqhi wa kutoka nje, wa kuyatambua mazingira ya jamii ili kuipembua kwa kina maudhui ambayo yanahitaji rai ya kisharia, ukizingatia kwamba humo kuna mambo yanayo fungamana na siasa, yanayofungamana na uhalisia wa jamii, na yanayogusa sekta ya uchumi au yanayoingia katika mas’ala ya kiutamaduni.

**Umarjaa naVigezo vya Kisharia:**

Ni lazima kutilia mkazo hapa kwamba umarjaa wa kidini unamasharti na sifa, na katika masharti hayo hakuna kigezo cha kimaada na kijamii, mwenye kurejelewa katika kuchukua hukumu ya kishariani wajibu awe mwanachuoni wa faqhi, yaani ni Mujtahidi mwenye kuweza kuchambua hukumu za kisharia kutoka katika vyanzo vyake vilivyokubaliwa na awe mwadilifu, msafi asiyekhalifu katika nyendo zake na vitendo vyake jambo lolote katika mambo ya dini. Na kunaweza kuwekwa humo sharti la mjuzi zaidi, yaani awe ni mjuzi

zaidi kuliko mwingine, kama ilivyo rai mashuhuri kwa wanachuoni wa fiqhi wa Kishia wa zama hizi.

Ama mazingatio ya kimaada, kama vile nasaba au utaifa au uraia, yaani awe ni raia wa nchi hii au ile, hakika jambo hilo si kigezo katika kuchagua Marjaa kama yatakosekana masharti ya msingi yanayotakiwa.

Alhamdulilahi umarjaa wa kidini umeendelea aghlabu kutoathiriwa na mazingatio haya, Marjaa wa kidini anaweza kuwa Mwarabu au Mwajemi au Mturuki au Mwiraki au Mwirani au Mpakistani au asiyekuwa hao, na anaweza kuwa ni Mhashimiya katika nasaba au ni kutoka katika nasaba nyingine, na kipimo cha kuchagua aghlabu kimebaki kuwa ni uwezo wa kielemu, kiwango cha uadilifu na kulazimiana na dini.

Na kuzungumzia umuhimu wa kuwepo mwachuoni wa fiqhi kutoka katika mazingira ya ndani ya kijamii husika haimaanishi kukiuka masharti ya kisharia ya sifa za Marjaa wa kidini bali ni sifa ya nyongeza katika upande wa sifa hizo. Kama ambavyo hakuna mgongano baina ya kuwepo mwanachuoni wa fiqhi wa sehemu husika na baina ya Marjaa wa kufuatwa katika fatwa, Marjaa anaweza kutoka nje ya nchi katika Hawza kuu ya elimu, kama vile Najaf Tukufu na Qum Tukufu, kwa kuwa ametimiza sifa ya kielimu ya mjuzi zaidi, lakini akawepo pia mwanachuoni wa fiqhi katika jamii husika hata kama si mwenye kufuatwa katika fatwa, ambaye atakuwa ni mtendaji na msaidizi wa Marjaa, ambaye anategemewa katika kupembua maudhui na kutathmini mazingira, na kutoa ufumbuzi, ambaye inategemezwa kwake kazi ya ukadhi na kusimamia mambo mengine, na hali hii ilikuwepo wakati uliopita na bado inaendelea katika baadhi ya nchi na jamii.

Na mfano na ushahidi mwingine ni nafasi ya Sayyid Musa Swadir aliyezaliwa 1928 na kufariki 1978 Hijiria, na Sheikh Muhammad

Mahdiy Shamsi Diyn aliyezaliwa 1350 na kufariki 1421 Hijiria, nafasi waliokuwa nayo huko Lebanon, walikuwa ni wanachuoni wawili wa fiqhi na kila mmoja alisimama katika nafasi ya uongozi katika uwanja wa Lebanon na wakatoa ufumbuzi wenye manufaa kwa matatizo ya jamii ya huko, na walikuwa na mawasiliano na uhusiano na Marjaa wa kidini. Na kwa Qatif tunaweza kuashiria nafasi ya faqihi Sheikh Ali al-Jashiy aliyezaliwa 1296 na kufariki 1376 Hijiria, ambaye aliongoza ukadhi na alikuwa mahala pa kuaminiwa na Marjaa na kutegemewa. Na Faqihi Sheikh Muhammad al-Haajiriy aliyezaliwa 1344 na kufariki 1325 Hijiria, alikuwa ni mfano wa hali hii katika uwanja wa al-Hisaai na kuna mifano mingi katika maeneo mengine.

**Je, Hukumu ya Kisharia Inaathirika na Mazingira?**

Kutofautiana kwa hali na mazingira ya jamii kunaweza kuathiri katika utoaji wa hukumu ya kisharia kwa Faqihi, au katika namna ya utekelezaji wake, na hilo litabainika vizuri kupitia sehemu zifuatazo:

1. Kubadilika anwani za maudhui kutokana na kubadilika zama, na kutokana na kubadilika mazingira, na miongoni mwa mifano iliyopo baina ya wanachuoni wa fiqhi ya mabadiliko hayo, ni bidhaa kusadikika kuwa ni ya thamani, au ya kawaida, ambapo hapo zamani mavazi na vyombo ni bidhaa zilizokuwa zinahesabika kuwa ni za thamani, kwa sababu utengenezaji wake wa mkono ulikuwa unasababisha tofauti katika sifa zake ambazo zilikuwa zinaathiri thamani yake, lakini sasa hivi bidhaa hizo zinahesabika ni kati ya bidhaa za kawaida, ambapo zinazalishwa na vyombo na viwanda, hivyo zinafanana na zinashabihiana.

   Bidhaa ya thamani katika isitilahi ya kifiqhi ni ile ambayo haina mfano wake katika soko, au ukipatikana lakini ni kwa

tofauti iliyozoeleka katika thamani. Ama bidhaa ya kawaidani ile ambayo unapatikana mfano wake katika soko bila tofauti iliyozoeleka.

Na kuna baadhi ya mas'ala ya kisharia ambayo yanahusiana na mabadiliko haya ya kusadikika kuwa bidhaa hii ni ya thamani au ni ya kawaida, kwa mfano tu ni katika dhamana ya kurejesha mali iliyoporwa, kurejesha mfano wake ikiwa iliyoporwa ni ya kawaida, na kurejesha thamani yake ikiwa iliyoporwa ni ya thamani. Na mfano mwingine ni katika kukopesha bidhaa ya kawaida na ya thamani na ni badala ipi inayothibiti katika dhima (yaani ni kipi unachotakiwa kurejesha).

Na kati ya mifano ya kubadilika anwani ni suala la kusadikika kuwa bidhaa hii inapimwa kwa kilo au ujazo, ambapo hukumu ya kisharia ya kuuza ni kilo kwa kilo na ujazo kwa ujazo, na sio kilo au ujazo kwa idadi, lakini hii inatofautiana kulingana na kutofautiana mazingira na jamii, na kila moja inakuwa na hukumu yake. Kwa mfano tu mayai yanaweza kuuzwa kwa kilo katika baadhi ya sehemu na kuuzwa kwa idadi katika sehemu nyingine, kama atauza kwa idadi katika sehemu ya kwanza au kwa kilo katika sehemu ya pili basi uuzaji huo hautokuwa sahihi, na vilevile kama atauza yai kwa mayai mawili na nazi moja kwa nazi mbili katika sehemu ambazo huuzwa kwa idadi, ziada hiyo haihesabiwi kuwa ni riba, wakati ambapo inakuwa ni riba katika sehemu ambayo inauzwa kwa kilo kama kilo zitatofautiana.

Vivyo hivyo hakika uhalisia wa nje wa baadhi ya anwani ambazo zinahusiana na hukumu za kisharia zinaweza kuto-

fautiana kwa kutofautiana mazingira, na hivyo hukumu zake nazo kutofautiana kulingana na tofauti hiyo ya mazingira, na hivyo hata uwezo, ufakiri, utajiri, kiwango cha matumizi na kumtendea wema mke, uhalisia wake na mipaka yake inatofautiana kati ya jamii hii na nyingine kutokana na tofauti za kijamii.

2. Kutofautiana makusudio na lengo, hukumu za kisharia zina malengo na madhumuni kufuatana na masilahi na uharibifu, na madhumuni na malengo yanapokuwa wazi mbele ya mwanachuoni wa kifiqhi, basi anayachukulia kwa mazingatio, na pindi yanapo tofautiana mazingira, na malengo nayo hubadilika na hapo hukumu hubadilika kufuatana na mabadiliko hayo. Mfano: Kuuza damu ilikuwa ni haramu wakati uliopita kwa kutokuwepo manufaa halali ya kufanya hivyo, lakini kuuza damu sasa hivi sio haramu tena kwa kuwepo haja ya kufanya hivyo, kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa.

   Na ilikuwa ni haramu kutumia mwili wa maiti kwa kukata viungo vyake, kwa sababu katika zama hizo kitendo hicho kilikuwa kinafanywa kwa dhamira ya kuutesa mwili na kulipiza kisasi, lakini sasa hivi imekuwa ni dharura (ya kitabibu) katika baadhi ya nyakati kupanda kiungo ili kuokoa maisha ya mtu anayekaribia kufa, na hivyo haizingatiwi kuwa ni haramu kwa ajili ya lengo hili.

3. Kubadilika kwa njia za maisha ni kati ya mambo yanayoathiri namna ya utekelezaji wa hukumu za kisharia, ikiwa ngawira za kivita zamani zilikuwa zinakomea katika upanga, mkuki, farasi na mfano wake, na ni fungu la wapiganaji baada ya kutoa khumsi yake, lakini ngawira za kivita za leo zimekuwa katika kiwango cha vifaru, magari ya deraya, makombora na

maroketi, sasa vipi itatekelezwa hukumu hii ya kisharia ya kuzigawa kwa wapiganaji leo hii?

Na hali ni hiyo hiyo katika hukumu ya mwanadamu kumiliki madini ambayo ameyagundua katika ardhi, ni namna gani inaweza kutekelezwa hukumu hii katika visima vya mafuta, je utajiri huu mkubwa unaweza kuwa ni milki ya watu ambao wameyagundua mafuta hayo katika ardhi yao?

4. Kuchunga masilahi ya jamii na kukadiria mahitaji na dharura: Katika fiqhi ya Kiislamu kuna zaidi ya anwanimoja zinazompa mamlaka faqihi mwenye jukumu la kutoa fatwa, kutoa fatwa kwa kuzingatia kipaumbele pindi hukumu moja ya kisharia inapogongana na hukumu nyingine, na atoe fatwa kwa kuziacha baadhi ya hukumu chini ya anwani ya pili, kama vile dharura na kudhuru, madhara na kujidhuru, shida na dhiki, muhimu na muhimu zaidi, wasila wa wajibu na haramu, na manufaa ya jumla ya ummah. Nazo ni anwani zinazotoa nafasi kwa faqihi kuondoa mgongano baina ya hukumu na matatizo ya kijamii.

   Hakika sehemu hizi na mfano wake zinatilia mkazo uwepo wa nafasi ya sheria yenye kuathirika kutokana na tofauti za zama, sehemu na mazingira, na ni juu ya faqihi kuchunga hayo wakati wa kutoa kwake hukumu ya kisharia, na huenda kati ya sababu zinazohalalisha uwepo wa faqihi na sharia tukufu kuiwajibisha jamii kutafuta elimu kwa namna ya wajibu wa kifai, ni ili mafaqihi waweze kuchukua jukumu hili kwa kujadidisha utafiti na uchunguzi katikahukumu za kisharia ambazo inawezekana zikaathirika kutokana na kutofautiana mazingira na mabadiliko ya maisha.

**Nususi na Ushahidi:**

Imekuja katika *Nahjul-Balaghah* kwamba Imamu Ali (as) aliulizwa juu ya kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Badilisheni ndevu na wala msifanane na Mayahudi." Akasema (as): "Hakika alisema hayo wakati dini ni finyu, ama sasa hivi dini imeshapanuka na imeenea pande zote, hivyo basi mtu ni yeye na atakachochagua."[8]

Sheikh Muhammad Jawad Mughniyah amesema katika kusherehesha kwake neno hili: "Nabii (s.a.w.w.) alikuwa amewaamuru wazee kati ya Masahaba wake wafunike mvi mbele ya adui kwa kupaka hina ili waonekane mbele ya adui kwa umbo la mwenye nguvu. Imamu Ali (as) amesema: Hiyo ni kwa kuwaUislamu ulikuwa dhaifu kwa uchache wa wafuasi wake, ama leo dini imeshadhihiri yote hivyo hakuna tena maudhui ya hukumu hii, mwenye kutaka basi aache kupaka hina na mwenye kutaka basi naapake.

Na unaweza kuuliza: Je haya hayapingani na hadithi mashuhuri kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): 'Halali ya Muhammad ni halali hadi Siku ya Kiyama na haramu yake ni haramu hadi Siku ya Kiyama.'?

Jibu: Hakika hukumu za kisharia zina namna mbili:

**Ya kwanza:** Inafungamana na tabia ya mwanadamu na maumbile yake kama mwanadamu, na aina hii ya hukumu haigeuki wala haibadiliki kabisa, kama vile mfumo wa ulimwengu na sayari katika harakati zake za kutembea, na aina hii ndio inayokusudiwa katika Hadithi mashuhuri.

**Aina ya pili**: Inafungamana na maisha ya kijamii, na hii hukumu yake inabadilika kulingana na mabadiliko ya jamii kutoka hali moja kwenda hali nyingine, ambapo maudhui ya hukumu yanabadilika na

8 Sharifu Ridhaa al-Musawiy katika *Nahjul-Balaghah*, chapa ya kwanza 1967 Beirut chapa ya Darul-Kitabi, Lebanon, Qiswaaril-Hikam: 17.

pia sababu yake inayowajibisha."[9] Na katika mtiririko huu ni yanapatikana yale yaliyopokewa katika *Wasail* kutoka kwa Muhammad bin Muslim na Zurara kwamba wao walimuuliza Imamu Muhammad al-Baqir (as) juu ya kula nyama ya punda wa nyumbani? Akasema (as): "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikataza kuila siku ya Khaibar, bali alikataza kuila katika wakati huo, kwa sababu ilikuwa ni kipando cha watu, na haramu ni aliyoiharamisha Mwenyezi Mungu katika Qur'ani."[10] Na katika nususi nyingine: "Bali alikataza kwa sababu ya kudhihiri hofu ya kutoweka (kwa punda hao), na punda sio haramu."[11]

Na ameashiria katika ukweli huu mhakiki al-Ardabiliya liyefariki mwaka 993 Hijiria ambapo amesema: "Na haiwezekani kusema kwa ujumla wa jambo bali hukumu zinatofautiana kwa kuzingatia khususia, hali, zama, sehemu na watu, na ndio dhahiri, na ni kwa kugundua tofauti hizi na kuzioanisha na vipengele vilivyochukuliwa katika sharia tukufu, ndio wamepata ubora wenye elimu na mafaqihi."[12]

Na Imamu Khomeni (r.a.) amezungumzia maudhui haya katika neno ambalo limekuwa mashuhuri kwake ambapo amesema: "Hakika mimi kimsingi nina imani na fiqhi iliyoenea baina ya mafaqihi wetu na ijtihadi iliyopo, na hili ni jambo la lazima, lakini hiyo haimaanishi kwamba faqihi wa Kiislamu haendani na mahitaji ya zama husika, bali kipengele cha zama na sehemu kina taathira katika ijtihadi, inawezekana tukio likawa na hukumu fulani lakini likachukua hukumu nyingine kutokana na misingi inayotawala jamii, siasa yake na uchumi wake."[13]

[9] Muhammad Jawad Mughniyah katika *Dhilaali Nahjul-Balaghah*, juz. 4, chapa ya kwanza 1973 Beirut chapa ya Darul-Ilimi lilimalaayiin uk: 226

[10] Muhammad bin Hassan al-Hurul-A'amily katika *Wasa'ailu Shi'ah* chapa ya kwanza 1993 (Beirut Muasastu Aaalil-Bait liliihiyaai turaathi) Hadithi namba 30120.

[11] Rejea iliyotangulia Hadithi namba 30125

[12] Ahmad al-Ardabiliy katika *Majmaul Fawaaidi wal-Burhaan*, Juz. 3 chapa ya pili 1419 Qum, Muasasatu Nashiril-Islaamiy uk. 436.

[13] Sayyid Ruhullahi al- Musawiy al- Khomainiy katika Swahifatu Nuur, juzuu 21 uk. 98.

Na Faqihi wa sasa Sheikh Ja'far Subhaniy ana risala fupi na nzuri chini ya anwani: Jinsi wakati na sehemu vinavyochangia katika kutoa hukumu za kisheria na kiserikali (*Taathiruz-Zamaani Wal-MakaaniAlaa Istinbaatil-Ahkaami ShariiyyahWal-Hukumiyyah*)[14], tumefaidika sana na risala hiyo katika utafiti wetu huu.

## MARJAA WA KIDINI NA UTAIFA

Kuna vikwazo vya kisiasa na kijamii, na ili kuvijua inahitaji kuishi navyo na kuamiliana navyo moja kwa moja, navyo zaidi huacha athari zake kwa mwanadamu na katika fikra zake pindi anapoamiliana navyo, kuliko pale atakapoishia kuvijua tu na kuvifahamu (bila kuamiliana navyo). Hakika Faqihi kwa kuamiliana kwake kivitendo na jamii anakuwa ni mwenye kuifahamu zaidi na mwenye uwelewazaidi juu ya dharura zake na mahitaji yake, na ni mtathimini bora zaidi na mwenye kubaini vizuri uhalisia wake na hali yake ya kisiasa na kijamii kiundani zaidi, na imesemwa tangu zamani:"Aliyepo huona asiyoyaona asiyekuwepo."

Bali Shahidi wa pili Zainu Diyn bin Ali al-Aamiliy aliyezaliwa 911 na kufariki 965 Hijiria ametaja katika jumla ya hukumu za mufti na adabu zake kwamba: "Haijuzu kutoa fatwa za mambo yanayohusiana na matamko ya yamini, kukiri, wasia na mfano wake isipokuwa yule ambaye ni mtu wa nchi ya yule aliyetoa tamko au awe ni mjuzi wa makusudio ya ada zao."[15]

Kama ambavyo mazingatio ya kisiasa yanamjengea Faqihi mkazi wa nchi husika uwezo mkubwa wakutoa rai na kuchukua msimamo

[14] Sheikh Ja'fari Subhaaniy katika *al-Bulughu*, chapa ya kwanza 1318 Hijiria, Qum Muasasatu Imami Swaadiq.

[15] Zainu Diyn bin Ali al- A'amiliy, shahidi wa pili, katika *Muniyatul-Muriid fiy Adaabil-Mufiid wal-Mustafiid*, chapa ya kwanza 1409 Hijiria, Qum, Maktabul-I'ilaamil-Islaaamiy, uk. 92.

unaohusu hali ya nchi yakekuliko uwezo wa faqihi ambaye yuko katika nchi nyingine, na pia unamfanya akubalike zaidi, ingawa vigezo vya kisharia ndio asili katika mambo ya kidini. Na uwepo wa Faqihi katika jamii una manufaa na athari zingine nzuri ambapo anaweza kunyanyua kiwango cha harakati za kielemu na kidini katika nchi husika, kwa njia ya kufundisha katika hatua mbalimbali za kielimu, na kuwalea wanafunzi katika viwango vya juu kama vile *Bahthil-Khaarij* kama inavyojulikana katika istilahi ya Seminari za Masomo ya Dini.

Vilevile hakika watu watamwitikia zaidi na watamtii zaidi faqihi mujtahidi jambo ambalo litatia nguvu hali ya kidini na kuimarisha umoja wa jamii na mshikamano wake. Na hapa inaweza kusemwa kwamba uwepo wa Mujtahidi faqihi ni jambo linalotakiwa katika kila mazingira ya kijamii, na hivyo hayako mbali yale aliyoyasema Sheikh Muhammad Mahdiy Shamsi Diyn kuwa kwa mujibu wa aya hii:

۞ وَمَا كَانَ ٱلْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُوا۟ كَآفَّةً ۚ فَلَوْلَا نَفَرَ مِن كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَآئِفَةٌ
لِّيَتَفَقَّهُوا۟ فِى ٱلدِّينِ وَلِيُنذِرُوا۟ قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوٓا۟ إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ ﴿١٢٢﴾

**"Wala haiwafalii waumini kutoka wote. Kwa nini kisitoke kikundi katika kila kundi miongoni mwao kujifunza dini na kuwaonya watu wao watakapowarudia, ili wapate kujihadhari." (Surat Tawba: 122)**, ni wajibu kuwepo faqihi katika kila jamii kwa namna ya wajibu wa kifai: Amesema: "Imeonyesha wajibu wa kujifunza kwa ajili ya kufikisha hukumu za kisharia, na imeonyesha kwamba wajibu huu ni thabiti kwa ummah wa Kiislamu kwa namna ya kifai, ni wajibu unaotakiwa kutekelezwa na kikundi kutoka kila kundi, hivyo ni wajibu kwa ummah wa Kiislamu pamoja na angalizo la mgawanyiko wake katika makundi,

na wajibu huu unayaenea makundi ya ummah kwa namna ya kifai kwa kila kundi, na utekelezaji wake unatimia kwa kila kundikuwa na kikundi kilichotoka na kujifunza.

Je, unazingatiwa umoja wa kitaifa baina ya kundi na wale wenye kutoka kwenda kujifunza? Kutokana na tuliyoyataja tunapata kuwa uwepo wa Mujtahidi katika taifa fulani miongoni mwa mataifa ya Kiislamu hautoshi kuondoa wajibu wa wananchi wa mataifa mengine ya Kiislamu kujifunza, bali ni wajibu katika kila taifa ambalo ni kundi la Kiislamu kiwepo kikundi cha watu waliotoka na kwenda kujifunza ambao ni mafaqihi na mujtahid, kwa sababu amri katika aya hii tukufu imekuja kwa namna ya mjumuisho wenye kuenea: 'Kila kundi' na utekelezaji wake hautimii kwa kutoka kikundi kutoka katika kundi moja au mengi ikiwa havijatoka vikundi kutoka katika makundi yote.

Na kwa msingi huu je inazingatiwa pia kwamba wenye kutoka kwenda kujifunza wawe ni kutoka katika kabila lile lile la walioamrishwa kutoka, hivyo kwa mfano Bani Tamiym hawatakuwa wametekeleza wajibu ikiwa waliotoka na kwenda kujifunza ni kikundi kutoka katika kabila la Twai (ijapo makabila yote mawili ni taifa moja), wala Wairaki kwa mfano, hawatakuwa wametekeleza wajibu ikiwa waliotoka na kwenda kujifunza ni Wamisri, hivyo haitoshi wote kuwakilishwa na anwani ya uarabu au uajemi au uturuki bali ni lazima hao wenye kutoka kwenda kujifunza wawe ni kutoka katika kundi ambalo ni anwani finyu zaidi na wala haitoshi kushirikiana tu katika sifa ya jumla ya uarabu au uajemi au uturuki? Au inatosha tu kuwakilishwa na anwani ya jumla ya kundi.

Hakika madhumuni ya kauli yake (swt): **"kikundi katika kila kundi miongoni mwao"** ni kutizama kundi ambalo ni anwani finyu zaidi na haitoshi kushirikiana tu katika sifa ya jumla, hivyo kwa mfano tu hakika Bani Tamiym ni kundi, na kama kitatoka kikundi

kutoka kabila la Twaibasi hakika hapo kijamii haitasadikika kwamba watu wa kikundi hicho ni miongoni mwao wao Bani Tamiym. Na piaWamisri – kwa mfano – ni kundi, kama kitatoka kikundi cha Wairaki basi hakika hapo kijamii haitasadikika kwamba watu wa kikundi hicho ni miongoni mwao wao Wamisri. Na vivyo hivyo, mas'ala yanahitaji uzingativu wa ziada."[16]

**Mafaqihi na Marajii Kutoka Nchini:**

Historia ya al-Ahsaai na Qatif imejaa idadi kubwa ya Marajii wa kidini na mafaqihi mujtahidi na wakazi wa maeneno haya katika karne mbalimbali, jukumu la umarjaa wa kidini wa maeneo haya lilikuwa linabebwa na mafaqihi wazawa wa maeneno haya. Na Marjaa wa mwisho wa kidini ambaye alikuwa anafuatwa al-Ahsaai ni Sheikh Habib bin Swalih bin Qariin ambaye alifariki mwezi 21 Muharram 1363 Hijiria, na kabla yake umarjaa ulikuwa wa Sayyid Naaswir bin Sayyid Hashim Salman aliyefariki 1358 Hijiria, kama ambavyo Marjaa wa mwisho wa kidini aliyekuwa anafuatwa Qatif ni Sayyid Majid bin Sayyid Hashim al-Awaamiy aliyefariki mwezi 7 Rabiul-Akhir 1367 Hijiria, na kabla yake umarjaa ulikuwa ni wa Sheikh Ali Abu Hasan al-Khaniiziy aliyefariki 1363 Hijiria.

Bali umarjaa wa baadhi ya mafaqihi wazawa wa maeneo haya ulifika hadi katika nchi nyingine kama vile Iraki, Iran, Kuwait na Bahrain. Sheikh Ahmad bin Zainu Diyn al-Ahsaaiy 1166 – 1241 Hijiria alikuwa akifuatwa na baadhi ya Wairaki na wengi miongoni mwaWairan, na miongoni mwao ni Mfalme wa Iran wa wakati huo Fatihu Ali Shaha na familia yake, Mawaziri wake na Wakuu wa dola yake. Na Dkt. Mirza Mahdi Khaan ameandika katika historia yake kwamba: "Hakika robo ya wananchi wa Iran walikuwa

[16] Muhammad Mahdiy Shamsi Diyn katika *al-Ijitihadi wa Taqlid* chapa ya kwanza 1998 (Beirut Musasatu duwaliyati lidirasaati wanashiri) uk. 91- 92

ni wenye kumfuata na ni wafuasi wake."[17]Na Sheikh Muhammad bin Ali Aali Abdul-Jabaar al-Qatifiy aliyefariki baada ya mwaka 1250 Hijiria, alikuwa anafuatwa na wengi miongoni mwa watu wa Iraki, watu wa Qatif na al-Ahsaai, na walimridhia Maulamaa wa Najaf kuhukumu baina yao na baina ya Sayyid Kaadhim Rashitiy siku za mzozo baina yao, na kuridhiwa na Sayyid aliyetajwa kunatosha kuwa ni fadhila.[18]Ama mafaqihi mujtahidina ambao hawajabeba jukumu la umarjaa wao ni wengi sana katika historia ya maeneo haya.

**Maswali na Majibu:**

Katika baadhi ya jamii za kisiasa na za vyombo vya habari kuna maswali yanayoendelea kuulizwa kuhusu mafungamano ya Shi'ah na umarjaa wa kidini wa nje ya nchi zao, na hususan wanapowatazama Shi'ah baada ya kuanguka utawala wa Iraki. Na ndani ya kila jamii ya Kishia zinaendelea kuongezeka hisia za dharura ya kuwepo Mafaqihi watakaobeba jukumu la kuendesha hali ya kidini katika jamii, na watakao imarisha hali ya kuaminiwa na watu na kufuatwa katika mambo ya kidini na kitaifa.

Na inafaa maswali kama haya yaulizwe bayana na kwa uwazi, na yajadiliwe kwa uzuri na kimaudhui. Kwa mfano baadhi ya watu wanajaribu kuwasilisha maudhui ya Shia kufungamana na Marjaa wa kidini wa nje ya nchi, kana kwamba ni udhihirisho wa Shia kukosa na kutokuwa na mapenzi na nchi yake, na hakika uwasilishaji huu unatokana na udhaifu wa kutokuwa na maarifa kamili kuhusu uhalisia wa mafungamano ya Shia na umarjaa wa kidini. Na inawezekana uwasilishaji huo ukatokana na mzozo wa kimadhehebu na kutaka kuchafua sura ya raia walio Mashia.

[17] Sayyid Hashim amebainisha katika: *A'alaam Hijir*, Juz. 1 chapa ya pili 1416 Hijiria Qum Muasasatu Ummul- Quraa uk: 173

[18] Sheikh Ali al-Biladiy al-Bahraaniy katika *Anuwaaru al-Badiriina* chapa ya pili 1407 Hijiria Qum, Maktabatu al-Mar'ashiy an-Najafiy uk. 317.

Hakika umarjaa wa kidini kwa Shia hauingilii mambo ya kisiasa ya jamii za kishia, ya ndani ya nchi zao mbalimbali, bali unahusika na mambo yao ya kidini na mas'ala yao ya kisharia, ama mambo ya kisiasa ya ndani na ya kijamii hayo jukumu lake linabebwa na viongozi na maulamaa wa nchi husika. Na sira ya Marajii inathibitisha kwamba wao wako katika kiwango cha juu kabisa katika kutoa nasaha na kujali masilahi ya nchi za Kiislamu, na kwa ajili hiyo wana waelekeza wafuasi wao katika kujihusisha na mambo ya nchi zao na kuamiliana na mazingira yao na kuhifadhi umoja wao wa Kiislamu na wa kitaifa.

Na Marjaa anaweza kubeba jukumu la kisiasa katika nchi yake kama vile Iran au Iraki kulingana na mazingira yanavyohitaji au kulingana na masilahi yanavyotaka. Ama suala la Marjaa kujenga misimamo ya kisiasa ya ndani ya nchi nyingine isiyokuwa nchi yake hili ni jambo ambalo halijatokea katika sira ya Marajii wa Kishia, na historia yao iko wazi na dhahiri shahiri.

Na kuwa na mafungamano na Marjaa wa kidini wa nje ya nchi sio suala makhususi kwa Shia tu, bali hata Ahlus-Sunna katika nchi nyingi wanafungamanisha mambo yao ya kidini na Chuo Kikuu cha Azhari cha Misri, na kuna nchi za Kiislamu ambazo zinachukua rai za mufti na maulamaa wakuu wa Saudia Arabia, je kufanya hivyo ni alama ya watu hawa kutozipenda nchi zao? Kama ambavyo jamii ya kikristo katika dola za ulimwengu zinamtukuza Papa ambaye anawakilisha uongozi wa dini kwa Wakristo, na yanafungamana naye makanisa yao na taasisi zao za kidini, na hakuna yeyote anayezingatia hilo kuwa ni kukosa mapenzi na nchi.

**Umarjaa wa Eneo na Vigezo vya Kisharia:**

Jamii ya Kishia inafuata vigezo na masharti ya kisharia katika kuchagua Marjaa wa kidini, na wala hawakubali kutia kasoro katika

masharti hayo eti kwa kufuata vipimo vya kisiasa na kimaada. Marjaa anachaguliwa kwa matakwa ya wananchi mbali na maamuzi na misimamo ya serikali, na kwa njia ya upole kwa mujibu wa ushahidi wa wajuzi miongoni mwa maulamaa wa Seminari za Masomo ya Dini na jamii mbalimbali za Kishia. Na kitendo cha Shia wa Iraki-ambao ni Waarabu asili, kujongea na kumfuata kwa hisia zao za kizalendo na za kitaifa Sayyid Sistaaniy ambaye asili yake ni Mwiran, inatoa ushahidi mzuri kuthibitisha ni kwa kiwango gani vigezo na masharti ya kisharia yanafuatwa katika kuchagua Marjaa wa kidini.

Kama ambavyo misimamo ya Marjaa Sistaaniy katika kina cha mkanganyiko na matatizo yanayotokea Iraki yanayotokana na uvamizi wa Marekani, inadhihirisha uhuru wa Marjaa, upevu wa rai zake na ukweli wa ikhilasi yake katika kulinda na kujali masilahi ya dini na ummah, kwa kuwa mbali na ushawishi wowote wa siasa za nje au za ndani.

Hakika uwepo wa Marjaa wa kidini ambaye ni mzawa wa nchi husika ambaye ana sifa zote za kisharia zinazotakiwa, unatengeneza chaguo bora zaidi, na hii ndio hali iliyokuwepo katika jamii nyingi za Kishia huko Iran, Iraki, Lebanon, Bahrain, al-Ahsaai na Qatif. Lakini udhaifu wa hali ya kielimu katika baadhi ya nchi hizi ndio uliowanyima neema hii katika zama za mwisho. Na hali ya kisiasa iliyopita katika nchi hizi ina mchango mkubwa katika kutengeneza udhaifu huu. Na kama serikali za nchi hizi zingejenga siasa ya kushajiisha elimu katika jamii za Kishia katika nchi hizo, na kuondoa vikwazo na vizuizi katika njia yake, ingewezekana kabisa kupatikana idadi kadhaa ya Mafaqihi na Mujitahidi na wazawa wa nchi hizo na kisha wangejitokeza miongoni mwao Marajii wazalendo kama ilivyokuwa wakati uliopita.

Kama ambavyo jamii za Kishia nazo zinabeba sehemu kubwa ya uwajibikaji huu, kwa sababu ni juu ya jamii hizo kuunga mkono na kusaidia uwepo wa Seminari za Masomo ya Dini katika nchi zao,

na ziwashajiishe wenye kupenda kutafuta elimu miongoni mwa wananchi wa nchi zao, na ziandae mazingira ya kupeleka vikundi baada ya vikundi kwenda kuendelea na masomo ya juu katika Seminari kubwa za Masomo ya Dini. Lakini kinachosikitisha ni kwamba wanafunzi wa elimu ya dini katika jamii zetu hawana anayewaunga mkono au anayewajenga, bali kila mmoja wao anategemea uwezo wake binafsi na msaada wa familia yake na posho ndogo anayoitoa Marjaa kwa wanafunzi wa Seminari za Masomo ya dini. Na aghlabu wengi wao wanalazimika kurejea katika nchi zao kwa kushindwa kuendelea na masomo ya juu, kwa sababu ya kikwazo cha hali ya kiuchumi na mahitaji ya maisha ya kifamilia.

Pamoja na kujua kwetu ugumu huu ambao unawakabili wanafunzi wanaosoma dini isipokuwa sisi tunataraji uvumilivu na juhudi zao, wapambane na vikwazo na vizingiti, kwani radhi za Mola, kuitumikia jamii na utukufu wa elimu vinastahiki kujitolea, na magumu yote huwa mepesi mbele yake, na imepokewa kutoka kwa Imamu Zainul-Abidin (as) kauli yake: “Watu wangejua yanayopatikana katika kutafuta elimu wangeitafuta hata kama ni kwa kutoa roho na kuzama ndani ya bahari.”[19] Kwanini mwanafunzi wa Kiiran au wa Kiafghanistan au wa nchi nyingine anavumilia maumivu ya miaka mingi ya kuwa ugenini huko Najaf tukufu kwa mfano, kutengana na ahali zake na nchi yake, na anavumilia hatari ya mazingira yaliyopo huko na ugumu wa maisha hadi anafikia daraja ya ijtihadi na umarjaa, wakati wanafunzi wetu wengi wanatosheka kiwango kidogo tu cha elimu kisha wanaharakisha kurejea kwenye nchi zao?

Tunasema kwa ujumla wanafunzi wetu wengi wanaharibika lakini miongoni mwao wamo wanaotarajiwa na wana mustakabali mzuri inshallah.

---

[19] Muhammad bin Yaaqub al-Kulaiyniy katika *al-Kaafiy* Juz. 1, chapa ya 1985 Beirut Darul-Ahiwaai uk. 35

**Kukuza Uelewa Juu ya Masuala ya Kifiqhi:**

Haja ya jamii ya kuwa na faqihi mujtahid mkazi wa jamii husika sio kwa ajili ya kurudisha na kurejesha utafiti wa maudhui ya misingi ya sharia na fiqhi ambayo utafiti wake umeshatimia, ingawa ni muhimu kuyafanyia utafiti kwa lengo la kukuza uwezo wa kielimu na ijtihadi, nayo ni yale maudhui ambayo haiwezekani kuyaepuka au kuyapuuza, lakini watafiti wake ni wengi na kunufaika na watafiti wa maudhui hizo hailazimu sifa ya wao kuwa wakazi wa eneo lako. Bali haja ya muhimu zaidi inayotufanya tuhitajie mafaqihi wakazi wa maeneo husika inajipambanua katika ulazima wa kujua matatizo ya jamii zao na mazingira yake na kutoa ufumbuzi wa kielimu unaofaa katika mazingira husika. Kwani hali ya kisiasa katika kila jamii, mambo ya kijamii yaliyopo humo, changamoto za kitamaduni, na uhusiano baina ya jamii husika na zile zinazoizunguka, yote haya ni mambo yanayohitaji utafiti na ufumbuzi wa kila jamii kulingana na sifa zake na mazingira yake, kwa uongofu wa sharia ya Kiislamu.

Na mwonekano wa kushindwa kushughulikia mambo ya eneo husika kupitia utafiti wa kielimu wa kifiqhi, unafichua udhaifu wa kutokuhisi majukumu ya kijamii ya kitaifa au kuogopa kujiingiza katika utafiti usiozoeleka au kuhofia kutoa rai na mtazamo. Na hapa lazima tulete baadhi ya mifano ya mafaqihi ambao wamejitofautisha kwa kushughulikia matatizo ya jamii zao na wameiletea miradi na mapendekezo kutoka kwenye vyanzo vya kielimu vya kifiqhi, watu hao ni kama vile Sayyid Musa Swadir, na Sheikh Muhammad Mahdi Shamsu Diyn huko Lebanon, ambao waliweza kuikomboa jamii yao na hali ya kudidimia, kunyimwa na kudharauliwa, na wakaisaidia kupangilia hali yake ya ndani na kuboresha uhusiano wake na jamii nyingine zinazoizunguka, na kuleta ushirikiano na kutoa mchango wake katika kiwango cha taifa kwa ujumla.

Na hutoba zao na maandishi yao ambayo yameasisi hali hii na yamelea ukuaji wake na kuendelea kwake, yamechapishwa na kusambazwa na ni maarufu, hususani tafiti za thamani ambazo alizifanikisha Sheikh  Shamsi Diyn ambazo ni: Mfano wa Kijamii na Kisiasa Katika Uislamu, Mfumo wa Serikali na Idara Katika Uislamu na Nje ya Uislamu, Sharia ya Nguvu ya Silaha Katika Uislamu, Mas'ala Magumu katika Fiqhi ya Mwanamke, Dharura ya Kuwepo Serikali, Uhuru wa Mataifa, Majadiliano ya Kiislamu na Kikristo, Uislamu na Umagharibi, Jamii ya Kimaendeleo ya Kiislam, na Mapendekezo Katika Fikra ya Kimaada na Fikra ya Kidini.

Na alipopatwa na maradhi yasiyotibika na akahisi kukaribia kuondoka duniani alirekodi wasia wake kwa watu wa jamii yake katika kaseti na ukachapishwa na kusambazwa baada ya kufariki kwake chini ya anwani ya '**Wasia'**:Nao ni maandishi ya kielimu ya asili yanayoshughulikia mambo yanayotokea katika sekta kwa ujumla, na yanaakisi katika medani ya Lebanon. Ukiongezea rai zake alizowasilisha katika jamii kupitia mihadhara, mahojiano na mikabala mbalimbali aliyoifanya na vyombo vya habari kuhusu suala la kisiasa na kijamii huko Lebanon, kwa mtazamo wa Kiislamu na katika misingi ya kifiqhi.

Na mfano mwingine unaonekana kwa Marjaa Shahidi Sayyid Muhammad Swaadiq Swadir aliyezaliwa 1362 na kufariki 1419 Hijiria, ambaye aliweza kuhuisha hali ya kidini huko Iraki katika kipindi cha serikali ovu ya utawala wa Sadam, na akatoa ufumbuzi wa kisharia wa mambo mengi ya kimaisha ndani ya jamii ya Iraki, na enklopedia yake ukiachia mbali fiqhi, imekusanya pia baadhi ya tafiti zake nyingine, na tayari baadhi yake zimeshachapishwa, na nyingi bado zingali ni tafiti za maneno yaliyorekodiwa. Na kati ya tafiti zake ni utafiti kuhusu kundi la Ghajar ambalo linaishi Iraki, na utafiti mwingine unaofanana na huo.

Hakika medani ya Lebanon iko wazi, kwani unapatikana humo uhuru wa kufanya utafiti na kutoa maoni, lakini ina changamoto zake na vikwazo vyake vyenye kutatiza, kama ambavyo medani ya Iraki wakati wa serikali ya utawala wa Sadam ilikuwa inawakilisha hali mbaya zaidi ya ukandamizaji na ukatili, hivyo kuwepo kwa mifano ya watu kama hawa wenye kupasua njia katika mazingira hayo magumu na wenye kujitolea kutatua matatizo na mishkeli ya ndani katika medani hizo mbili, ni ushahidi tosha kwamba katika mazingira yoyote yale na katika jamii yoyote ile upo uwezekano wa kutekelezwa wajibu huo wa kuelekeza.

Hakika mimi nawashauri wasomi wenye vipaji vya elimu miongoni mwa wanajamii yetu, waelekeze uwezo wao wa kiutafiti katika kutatua mambo ya jamii yao, na wachangie katika safari ya kujenga na kuendeleza nchi zao, faqihi wa Kishia yeye katika nchi yake ni mkazi mwislamu hivyo ni wajibu juu yake kubeba majukumu yake katika nchi yake, jamii yake na dini yake, na wala asiifunge nafsi yake ndani ya duara la kabila na madhehebu ambalo linazuia kujishughulisha na mabadiliko ya wakati na mambo ya nchi.

# FASLU YA PILI

## MAELEKEZO YA KIDINI, CHANGAMOTO NA VIPAUMBELE

**Maelekezo ya Kidini naUtandawazi:**

Maelekezo ya Kiislamu yameingia katika utandawazi bila ya matakwa yake na bila ya azima au mipango ya awali, lakini harakati za utandawazi wenye kukokoteza umejiingiza wenyewe katika kila kitu. Matukio makubwa yanatokea katika sehemu mbalimbali za ulimwengu naWaislamu wanajikuta ni sehemu ya matukio hayo, ima kwa kushiriki kwa maamuzi binafsi ya baadhi ya watu au kwa mikakati ya uadui kwa kuwaingiza Waislamu na kuwatumbukiza katika mapambano mbalimbali ili kutimiza msemo wa mapambano ya kimaendeleo au kwa propaganda tu inayojitokeza ya kutengeneza uchochezi wa vyombo vya habari au kwa sababu yoyote nyingine.

Na inatosha kwamba tukio muhimu sana lililotikisa ulimwengu wa kileo la tarehe 11 Septemba 2002 la kulipua New York na Washington, lilikuwa na sura ya Kiislam yenye kufifia. Hakika ni tukio la mabadiliko katika historia ya ulimwengu mpya, kupitia tukio hilo yameanzishwa mengi kati ya mabadiliko na matukio makubwa ya kiulimwengu, hususan katika yanayohusiana na hali ya Waislamu na harakati ya uwepo wao na kiwango cha uhusiano wao na ulimwengu. Na inakaribia kutopita siku isipokuwa wakala mmoja au zaidi wa habari na vyanzo vya taarifa, ni lazima atoe habari inayohusiana na mambo ya Waislamu, tena ni aina za habari ambazo zinachochea uzingativu, habari kama vile mlipuko mkubwa wa kigaidi au uharamia

mbaya wa utekaji nyara au picha za kuua kwa kuchinja na kuteketeza kunakotisha.

Kikawaida matukio kama haya huhitaji kuwepo au kujitokeza maelekezo ya Kiislamu kulingana na misimamo na mielekeo mbalimbali katika medani yake. Katika upande mwingine nyasila za mawasiliano zimeendelea na chanel za matangazo ya satalaiti za kisasa zinapatikana kwa watu wote, hivyo ni soko kubwa la uzalishaji faida wa kimataifa, na hivyo ni lazima wamiliki wake wajiingize katika shughuli za uzalishaji wake, kama ambavyo zinakidhi mahitaji muhimu kwa kila upande wenye malengo mbalimbali ya kisiasa au ya kidini au  ya kiuchumi.

Waislamu wamevamia ulimwengu huu uliondelea na wamekuwa na makumi ya chanel za Kiislamu na maelefu ya vituo vya tovuti, ukiongezea idadi kubwa ya magazeti na majarida. Uwepowa Waislamu hauishii tu kwenye mimbari mahususi kwao, bali wana uwepo wao na upatikanaji wao ambao unalazimishwa na matukio kupitia mimbari na chanel mbalimbali. Lakini ambayo ni wajibu kuyatafiti na kuyajadili ni kiwango na mwelekeo wa utandawazi katika maelekezo ya Kiislamu, je yapo katika kiwango cha kujibu mashambulizi na kutoa majibu ya taathira za matukio au yanavuka hapo na kwenda kwenye kiwango cha kuwasilisha mapendekezo na kupanga anwani na nembo zinazokubali kubadilika na kunyumbulika katika kiwango cha ulimwengu. Je, hali ya utandawazi wa Kiislamu inaishia tu katika kutumia njia zilizoendelea na ufanisi wa kiteknolojia ya kisasaau inavuka hadi kwenye kujadidi madhumuni na kuboresha mazingatio na kuendeleza malengo?

Utandawazi sio tu vyombo na njia, bali ni wigo wa mazingatio ya kiulimwengu ambao unavuka vikwazo na umakhususi, nao ni medani ya mapambano na ushindani baina ya tamaduni na yanayotokana na tamaduni hizo miongoni mwa nyendo na mbinu za

kuishi. Utandawazi umeweka dini zote za kiroho na mifumo mizuri ya tabia njema mbele ya changamoto ngumu na kali, na ni kana kwamba unataka kuunda upya maisha ya mwanadamu katika sekta zake mbalimbali ndani ya vipimo na uzani mmoja wa kiulimwengu unaokubaliwa na pande zenye uwezo mkubwa katika mambo ya ulimwengu. Maelekezo ya Kiislamu yanaangukia wapi katika kipimo cha utandawazi huu?

Hakika sehemu kubwa ya maelekezo haya yameuingia utandawazi katika mpaka wa muonekano na umbo tu, kwa kutumia njia zake na teknolojia yake, lakini madhumuni ya maelekezo na malengo yake bado yangali ni ya mji au kijiji kidogo kilichojitenga na sio kijiji cha ulimwengu ambacho kinafunika ardhi yote. Hakika maelekezo hayo yanaelezea malengo na mazingatio ya sehemu tu ya jamii katika kijiji kidogo bila ya kupiga hatua hadi kufahamu chochote katika malengo ya binadamu katika kiwango cha ulimwengu.

Na mambo yanayotatuliwa na maelekezo haya yanaonekana ni duni ukilinganisha na yale yanayoshughulisha akili ya mwanadamu wa zama hizi miongoni mwa matatizo makubwa yanayotishia kwa hatari kubwa mustakabali wa mazingira ya mwanadamu.

Hakika ni maelekezo yanayotosheka na kutukuza yaliyopita ilikuimarisha kwa hilo hali ya kutoendelea, na badala ya mtu kuhamasisha watu wake kwenye mustakabali wa maendeleo, anawashughulisha na mizozo ya historia yao iliyopita, ili wagawanyike katika makundi, baadhi wanamtukuza khalifa huyu, na wengine wanamfanyia uadui, licha ya kwamba ukhalifa ulishapita na kumalizika tangu muda mrefu. Au anahuisha tena unyanyapaa na mtengano kwa msingi wa ikhitilafu kuhusu misemo ya kinadharia iliyozalishwa na zama za mizozo ya theiolojia kabla ya karne nyingi, na wala haina faida katika uhalisia wa maisha ya leo.

Na lililo baya zaidi kuliko hayo ni maelekezo haya kung'ang'ania katika kuugawa ulimwengu sehemu mbili, sehemu ya amani na sehemu ya vita, bila kujua mabadiliko ya kijografia, kisiasa na kifikra, ambayo ulimwengu unaishi nayo. Hivi ndivyo yanavyoonekana maelekezo ya Kiislamu yanayoshughulika na watu wa kijiji chake kidogo ambao ni kundi la Waislamu, bali ni kundi la waumini wa madhehebu yake katika kijiji chake, bali ni wafuasi wa mfumo wake maalum ndani ya madhehebu yake, hata kama atatumia njia za utandawazi zilizoendelea na teknolojia yake. Vipindi vingi katikachanel za Kiislamu, na maelekezo ya vituo vingi vya tovuti za kidini, zinafichua wazi ukweli huu mchungu.

Kwa hakika kiwango hiki cha mapendekezo na utekelezaji wa maelekezo ya Kiislamu katika zama za utandawazi na kupitia vyombo vyake, kinatoa picha mbaya kwa Uislamu, na kinatoa nafasi ya watu kutilia shaka uwezo wa Uislamu katika kukabiliana na changamoto za maendeleo na tamaduni nyingine, na katika kufaa kwake kuelekeza maisha ya mwanadamu wa kileo.

Hakika kwanza juhudi kubwa za msingi ni wajibu zitolewe ili kuweka kanuni na kuimarisha miundo mbinu ya maarifa ambayo ndio yanafaa kuwa chimbuko la maelekezo ya Kiislamu ya mtu wa kisasa, huenda katika vipaumbele vya mwanzo ni kupata mtazamo sahihi na kamili kuhusu hali ya ulimwengu mpya, na kusoma maudhui ya mabadiliko ambayo jamii ya kibinadamu inaishi nayo leo.

Pili, ni kufikiri kwa akili ya kibinadamu muwazi inayozingatia masilahi ya jinsia ya kibanadamu, na inayofahamu mwingiliano wa kimasilahi baina ya wanafamilia ya kibinadamu, na kupata ufumbuzi na utatuzi wa changamoto ambazo zinawakabili wote.

Tatu, ni kujadidisha mtazamo na ijtihadi katika fikra na fiqhi ya Kiislamu kwa ajili ya kuchambua rai na hukumu kuhusu mambo

mapya, na katika mwanga wa mabadiliko ya kimaarifa, hiyo ni kwa sababu fikra na fiqhi ni zao la uzalishaji wa binadamu, inaathirika na kiwango cha mzalishaji wake na fahamu yake, na kwa athari ya mazingira ambayo waliishi humo na wakashughulika nayo.

Hakika nususi za kisharia ni thabiti hazidhibitiwi na zama wala sehemu wala mipaka ya mazingira ya kijamii, lakini kuzifahamu nususi hakuko hivyo, na waliyotuachia watangulizi wetu miongoni mwa maulamaa na mafaqihi (r.a) Mwenyezi Mungu awalipe kheri kwa juhudi na huduma zao, miongoni mwa rai za kifikra na kifiqhi, yanaonyesha juhudi zao na uelewa wao, na wala hayaondoshi kwetu wajibu wa ijtihadi, ambapo ni wajibu kwa ummah katika kila zama kuzalisha mujtahidina wenye uwezo, watakaofanya kazi ya kutazama na kuchambua, na lau kama tungekuwa tunalazimika kung'ang'ania ijtihadi za waliotangulia au ingekuwa inasihi kwetu kutosheka na ijtihadi hizo na kusimama hapo, basi wajibu wa ummah kufanya ijtihadi katika kila zama na kila kizazi, kwa namna ya wajibu wa kifai (kutosheleza) kama walivyokiri mafaqihi, usingekuwa na maana yoyote.

Nne, nikuwa na mawasiliano na ummah na mataifa mengine na kufunguka mbele yao ili kunufaika na mataifa hayo na kuamiliana nayo, kwa kuitikia wito wa Qur'ani unaotaka wanajamii ya kibinadamu wajuane:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقۡنَٰكُم مِّن ذَكَرٖ وَأُنثَىٰ وَجَعَلۡنَٰكُمۡ شُعُوبٗا وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوٓاْۚ
إِنَّ أَكۡرَمَكُمۡ عِندَ ٱللَّهِ أَتۡقَىٰكُمۡۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٞ ﴿١٣﴾

**"Enyi watu! Hakika Sisi tumewaumba kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumewafanya mataifa na makabila ili mjuane. Hakika mtukufu zaidi yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni aliye na**

**takua zaidi yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye habari.”** **(Surat Hujurat: 13)**.

Na kuchukua wasia wa Nabii wetu Mtukufu(s.a.w.w.) katika kauli yake: “Tafuteni elimu hata kama ni china.”[20] Na kauli yake (s.a.w.w.): “Neno la hekima ni kipote cha muumini popote atakapoikuta basi ndio mwenye kuistahiki zaidi.”[21]

Tano, ni uwasilishaji mzuri na kuwasilisha misingi ya Uislamu na mafunzo yake, hiyo ni kwa sababu usahihi wa malengo na madhumuni hayaachi kuhitajia njia nzuri ya uwasilishaji, na hapa Qur’ani Tukufu inatilia mkazo juu ya kujitahidi kuchagua njia bora zaidi na wasila mzuri zaidi wa kulingania kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu:

ٱدۡعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلۡحِكۡمَةِ وَٱلۡمَوۡعِظَةِ ٱلۡحَسَنَةِۖ وَجَٰدِلۡهُم بِٱلَّتِي هِيَ أَحۡسَنُۚ
إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعۡلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِۦ وَهُوَ أَعۡلَمُ بِٱلۡمُهۡتَدِينَ ١٢٥

**“Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako ndiye anayemjua zaidi aliyepotea njia yake na Yeye ndiye anayewajua zaidi walioongoka.”** **(Surat Nahli: 125).**

## KUENDANA NA WAKATI

Katika zama hizi chemchem za maarifa zinabubujika mbele ya mwadamu wa leo, huku mafuriko ya maalumati kutoka kila pande na kutoka katika kila kitu yakizidi kumzunguka. Na hali ya kutojua kusoma inakaribia kumalizika, kwani baada ya hapo zamani

[20] *Wasa’ilus-Shia’ah*, Juz. 27 uk. 27 Hadith namba: 33119.

[21] Muhamamad bin Isa bin Surati Tirimidhiy katika *Sunan Tirmidhiy*, Juz. 3 uk. 479 chapa ya kwanza 2000 Beirut Darul-Qutubil-ilimiyyati hadithi namba 2678

idadi ya wanaoweza kusoma na kuandika kuwa kubwa miongoni mwa watu, kiasi cha kuhesabika kwa vidole katika kila jamii, sasa idadi ya wasiojua kusoma imekuwa ni ndogo sana na inapungua kila mwaka katika kiwango cha kimataifa. Na hata wasiosikia au wasioona wameandaliwa mazingira ya kujifunza na zimeandaliwa njia na nyenzo za kumaliza hali ya kutojua kusoma.

Na wigo wa elimu za ardhi na anga umefunguka mbele ya wanadamu kutoka kwa aina mbalimbali za wanadamu, kutoka kona zote, katika kila tabaka na kila kabila, na elimu sio tena jambo la watu au kundi la watoto wa masultani, matajiri na wenye nacho. Sasa ulimwengu kwa matukio yake na mabadiliko yake umewekwa mbele ya mwanadamu huku yeye akiwa amelala kitandani au ameegemea katika kochi lake anashuhudia kila habari au kutizama tukio muhimu wakati wa kutokea kwake, tena kwa picha ya rangi na sauti iliyowazi na kwa lugha yoyote anayoijua.

Ama mashine ya hesabu na tovuti, hiyo ni fimbo ya ajabu ambayo anaitumia kila mtu katika zama hii ili kupata maalumati yoyote anayoyataka na fikra yoyote anayoitafuta, na kwa njia hiyo anafungua kila mlango kati ya milango ya hazina ya elimu na maarifa katika nyanja mbalimbali na ubobezi wa fani mbalimbali, na idadi ya watumiaji wa tovuti ulimwenguni imefikia bilioni moja katika mwaka 2011.

Kabla ya miaka kadhaa nilisoma katika ripoti moja kwamba: Hakika ndani ya miaka 30 iliyopita ulimwengu umezalisha maalumati mengi kushinda ambayo ulizalisha ndani ya miaka elfu tano ya hapo kabla. Na nakala moja ya toleo moja la gazeti la *New York Times*, hukusanya maalumati ambayo katika karne ya kumi na saba angeweza kuyaandika mtu wa Ulaya katika maisha yake yote. Na kila siku kuna maneno milioni ishirini yanayoandikwa kwa njia ya vyombo vya habari na vifaa vingine vya kutunzia taarifa. Na mso-

maji ambaye anaweza kusoma maneno elfu moja kwa dakika, itamchukua mwezi na nusu kusoma yaliyoandikwa katika siku moja tu, na mwisho wa muda huu atajikusanyia anayoyahitaji kuyasoma kwa muda wa miaka mitano na nusu.[22] Na kabla ya miaka kadhaa, takwimu za Unesco na Umoja wa Wachapishaji wa Kimataifa ziliashiria kwamba ulimwengu kila mwaka huchapisha:

Vitabu milioni moja na robo takriban,

Nusu milioni takriban ya machapisho ya kawaida,

Na ripoti milioni tano za taaluma na fani mbalimbali,

Na robo milioni ya tafiti za Shahada ya Pili na Ph.D,

Na robo milioni ya vitabu na jozi za machapisho ya elektoronia.[23]

Katika zama hizi ambazo fikra zimesongamana kwa mwanadamu na yanarundikana kwake maarifa na maalumati, ni namna gani maelekezo ya kidini yanaweza kupenya hadi katika akili ya mwanadamu huyu wa kileo? Na ni namna gani yatapanda hadi katika kiwango cha ushindani na cha kutoa changamoto? Hakika sharti la kwanza linalomuwezesha kukubali maelekezo ya kidini limejificha katika mahusiano yake na zama hizi zilizopo, inapasa mwasilishaji atumie lugha yake na aamiliane na mambo yake, mazingatio yake, na anufaike na mbinu zake na ufanisi wake.

Hakika maendeleo ya elimu na mabadiliko ya maarifa na urahisi wa kuenea maalumati na kusambaa kwake, sio tatizo na wala si kitenda kazi cha changamoto mbele ya maelekezo ya Kiislamu, bali katika uhalisia maendeleo hayo ni mtaji mkubwa kwa mwanadamu na msaada mkubwa kwa uhalisia wa dhana za dini unaoafikiana na maumbile na taratibu za Mwenyezi Mungu Mtukufu zilizopo katika

[22] Jarida: Jarida linalotolewa kila wiki London tolea namba 928 la tarehe 29/ 11/ 1997.

[23] *Wujhaatu Nadhar*: ni jarida linalotolewa na shirika la kimisri linasambazwa katika nchi za kiarabu na kimataifa, Cairo toleo namba 37 February 2002

mazingira na maisha. Ujahili ndio kikwazo kikubwa kinachomzuia mwanadamu kufuata dini, na ndio sababu ya mwanadamu kuporomoka katika maporomoko ya ukafiri, shirki na upotovu, na kwa sababu hiyo, muumini anajikinga kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kutokana na ujahili:

قَالَ أَعُوذُ بِٱللَّهِ أَنۡ أَكُونَ مِنَ ٱلۡجَٰهِلِينَ ٦٧

**"Akasema: Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kuwa miongoni mwa wajinga."** **(al-Baqarah: 67)**.

Na Mwenyezi Mungu anamhadharisha Nabii wake na kiwango cha chini cha fikra za wajinga, anasema (swt):

فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ ٱلۡجَٰهِلِينَ ٣٥

**"Basi usiwe miongoni mwa wajinga."** **(An'am: 35)**.

**Na anasema (swt):**

خُذِ ٱلۡعَفۡوَ وَأۡمُرۡ بِٱلۡعُرۡفِ وَأَعۡرِضۡ عَنِ ٱلۡجَٰهِلِينَ ١٩٩

**"Shika usamehevu na amrisha mema na achana na wajinga."** **(Surat A'araf: 199)**.

Na kama anavyosema Imamu Ali (as): "Ujinga ni chanzo cha kila shari."[24] Na Imamu Ali (as) anaeleza sababu ya watu kuchukia matukio na kweli nyingi kuwa inatokana na ujahili, anasema: "Watu ni maadui wa yale wasiyoyajua."[25]

[24] *Ghurarul-Hikam wa Durarul-kalim*
[25] *Nahjul-Balaghah*, hekima namba 172

Ama elimu hakika ni njia ya imani, uongofu na uvumbuzi wa haki, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَيَرَى ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْعِلْمَ ٱلَّذِىٓ أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ هُوَ ٱلْحَقَّ وَيَهْدِىٓ إِلَىٰ صِرَٰطِ ٱلْعَزِيزِ ٱلْحَمِيدِ ﴿٦﴾

**"Na wale ambao wamepewa ilimu wanaona kuwa uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako ni haki na huongoza kwenye njia ya Mwenye nguvu, Mwenye kusifiwa." (Surat Sabai: 6)**.

Na imepokewa kutoka kwake (s.a.w.w.) kwamba amesema: "Elimu ni uhai wa Uislamu na ni nguzo ya imani." [26]

Kufuatana na ukweli huu hakika maendeleo ya kielimu yanatumikia misingi ya dini na kuwafanya watu ni wenye kumiliki maandalizi mengi zaidi ya kuikubali dini na kuamiliana nayo, kama ambavyo kuendelea kwa mbinu za maarifa kunatoa fursa bora zaidi kwa lengo tukufu la Uislamu, kunauwezesha kufikisha sauti yake kwenye masikio na akili.

Lakini tatizo linatokana na uelewa wa walinganiaji wa Uislamu katika kujua uhalisia wa zama zilizopo, na uwezo wao katika kufikisha dhana za Uislamu na maadili yake katika uhalisia wa maisha ya kileo. Hiyo ni kwa sababu kundi kubwa miongoni mwao linaishi katika zama hizi kwa viwiliwili tu, lakini kiakili, kilugha na kimawazo linaishi katika zama zilizopita, linaangalia matatizo ya zama hizo zilizopita na linashughulika na mizozo ya kifikira na kisiasa iliyopita, na linashikamana na mazingatio ya waliotangulia na limekosa uwezo wa uvumbuzi wa kifikra na ujasiri wa ijtihadi ya kifiqhi.

[26] *Kanzul-Umaal*, Hadith namba 28944

Hakika sehemu ya maelekezo ya kidini inaleta istihizai na dharau kwa kukhalifu kwake uhalisia wa zama zilizopo na kutojua kwake masharti ya wakati na sehemu, na kutokuafikiana kwake na mazingira ya jamii husika.

Katika makala yenye anwani 'Matatizo ya Hotuba za Ijumaa' (*Azimatu Khutubatul-Jum'ati*) Dkt. Khalis Jalabiy ameandika ukosoaji mkali wa aina hii ya hotuba kwa kutoa baadhi ya ushahidi na mifano yake, ambapo zimekuja katika makala ibara zifuatazo:-

Tangu zama za Yazid bin Muawiya, siku ya Ijumaa hupanda mimbari khatibu yule yule, hukariri mtindo uleule na hurudia dua ile ile ya kumlinda na kumhifadhi mtawala. Na anakabiliana na watu bubu, wakimya, waliofungwa midomo kwa kufuli kubwa kuliko mkanda wa tumbo, ili wasikie mazungumzo ya mwenye kuwaidhi mambo ambayo hayastahiki mkusanyiko, hazungumzii hapo zaidi ya matunda ya peponi, kuhusu Akhera na kuhusu Firaun mwenye vigingi.

Na amenisimulia mtu mmoja kutoka katika nchi moja ya Kiarabu kwamba hotuba za Ijumaa huandikwa na afisa makhususi aliyepewajukumu la kuchezea akili za watu, na kisha zinatumwa kwa faksi kwenda kwa makhatibu wa misikiti yote ili wasome hotuba moja ya pamoja iliyoelekezwa, na hili ni zuri zaidi kwao kuliko kumiza kichwa.

Na katika mji wa Montreal Canada nilihudhuria hotuba na Swala ya Ijumaa, mara nikadhani niko katika msikiti wa Waturuki katika mtaa wa Qasiyun huko Damascus, kwani khatibu hakuzidisha zaidi ya mawaidha ya Uthmaniyyah na dua za uadui, kwamba "Mwenyezi Mungu awateketeze makafiri wote na familia zao." Wakati ambapo Wa-Canada wamewapa Waislamu uraia, riziki ya kutosha, masomo bure na amani ya kutosha bila kunyanyaswa na wapelelezi wala kusakamwa na taarifa za majasusi. Na katika sehemu fulani nilihudhu-

ria hotuba katika msikiti, mara khatibu akabadilisha hotuba na kuwa maudhui ya kifiqhi inayohusu kustanji na kufanya istibrai kwa kutumia mawe, hiyo ni licha ya kwamba watu hawatumii tena mawe katika vyoo vyao vya kisasa tangu zama za ukoloni wa Kifaransa.

Na katika mji wangu ambao nimeishi tangu utoto wangu, imamu alikuwa anahutubia kwa kusoma hotuba za Ibn Nabata, hotuba za tangu zama za Mtawala Qalaawun, na humo kuna hotuba 52 za mwaka mzima na kulingana na misimu. Tulikuwa katika msimu wa funga mara akazungumzia Hija kisha akazinduka na kugundua kuwa amebadilisha msimu hivyo akawa anageuza haraka haraka kurasa kutafuta hotuba ya msimu husika baada ya kupoteza mwelekeo.

Na katika nchi moja ya Kiarabu khatibu alikuwa anaomba dua isiyo na mwisho ya kuyateketeza kabisa makabila na kuyaangamiza moja kwa moja, na kuwafanya watoto wawe mayatima na wanawake wawe wajane, na kwamba Mungu aoneshe maajabu ya viumbe vya Mwenyezi Mungu kupitia kwao. Na alikuwa na hamasa kubwa pindi alipokuwa anawaombea wasio na dini, kwamba wauliwe kabisa na wahilikishwe kabisa na wala asibakishwe yeyote miongoni mwao, alikariri hayo mara tatu na sauti yake ikakatishwa kwa kilio.[27]

Kama makhatibu hawa wanakabiliwa na udhuru wa kutokuwa na maarifa kamili na uwelewa sahihi kuhusu zama zao, na kutokujua ujumbe wao, basi hakika sehemu nyingine ya makhatibu wanafanya uzembe, wao hawatumii juhudi za kutosha katika kuandaa hotuba zao na kuzitayarisha. Pamoja na kuenea kwa mbinu na vyombo, kwani kamusi za faharasa zipo katika kompyuta, na vituo vya kutafutia taarifa katika tovuti vinakupa maalumati na taarifa yoyote au rejea yoyote anayoihitaji khatibu kwa ajili ya kuandaa anayotaka

[27] *Sharqil-Ausat*: Jarida la kila siku linalotolewa London la tarehe 26 /6 / 2002.

kuzungumzia. Kama ambavyo vyombo vya habari vya ndani na vya nje vinavyotoa fursa ya kujua mambo mbalimbali na matatizo yaliyopo katika jamii ya leo.

Na katika jamii yetu ya leo kuna idadi kubwa ya wabobezi na wenye ubobezi ambao inawezekana kuwaomba ushauri na kanufaika na maoni yao katika kutatua mambo yanayohusiana na ubobezi wao. Hakika udhaifu wa maandalizi ya khatibu katika kuandaa hotuba unafanya utatuzi wa khatibu uwe ni wa juu juu na mwepesi, kama ambavyo uhandisi wa maudhui na mfumo wa kuwasilisha unavyokuwa na mkanganyo na usio na umakini wala ufanisi. Wakati ambapo khatibu mwenye juhudi katika kuandaa hotuba, huwa ni mwenye kudhibiti maudhui ya utafiti wake, mwenye mtiririko mzuri wa nukta zake, na hukinaisha fikra zake kwa hoja na ushahidi wenye kuathiri, jambo ambalo huifanya hotuba yake iwe na faida nyingi na iwe na uwezo wa kukinaisha na kuathiri.

## UBINADAMUWA MAELEKEZO YA KIDINI

Maelekezo ya kidini yanachukua nafasi muhimu sana katika jamii zetu za Kiislamu katika kuathiri na hakuna maelekezo yoyote yenye kulingana nayo katika hilo, yenyewe ndio yanayotengeneza fikra za jamii na kuelekeza nyendo zao, hiyo ni kutokana najamii zetu kufungamana na dini, na maelekezo hayo kuelezea amri za dini na hukumu zake. Katika upande mwingine, hakika maelekezo ya kidini yamekuwa ni kioo cha sura zetu mbele ya ummah na tamaduni nyingine, kupitia kwayo inajitengeneza picha na sura ya ummah wetu, dini yetu na utamaduni wetu.

Na pindi tunapokuta hali ya kushindwa katika akili ya mkusanyiko wa ummah, na hali ya upungufu katika nyendo za wana-

jamii wake, na pindi inapotikisika sura ya ummah katika medani ya mtazamo wa jamii ya kimataifa, basi wakati huo ni wajibu tuyarejelee maelekezo yetu ya kidini, nayo ni ima yawe ndio chanzo chenye kuwajibika na upatikanaji wa hali hii mbaya au yawe ni yenye kuikaribisha na kuimarisha uwepo wake.

Hakika ni wajibu wetu kutofautisha baina ya mambo ya kidini na nususi za kisharia za kidini, kwani nususi za kidini ni yote yaliyothibiti kwa kupokewa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kutoka kwa Mtume Wake Muhammad (s.a.w.w.), yaani Kitabu na Sunnah. Qur'ani Tukufu hakuna shaka imepokewa kwa tawaturi, yote yaliyomo baina ya jalada mbili za msahafu mtukfu yameepukana na ziada na upungufu. Ama Sunnah tukufu ni ile ambayo umethibiti usahihi wa kupokewa kwake kwa udhibiti wa vigezo vya kielimu vinavyokubaliwa na mafakihi wa ummah.

Nususi hizi za kidini (Kitabu na Sunnah)hazina nafasi ya kukosolewa na kutuhumiwa, kwani hakika zimefunuliwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kutoka kwenye wahyi Wake mtukufu na kutoka kwenye chanzo kilichotakasika, na wala haiwezi kupenya katika moyo wa Mwislamu chembe ya shaka kuhusu ukweli wake na utukufu wake.

Ama maelekezo ya kidini yenyewe ni jambo ambalo ameling'amua na kulifahamu faqihi, mwanachuoni na mwanafikra, kutoka katika nususi za kidini au kutoka katika vyanzo vya ijtihadi na uchambuzi unaotegemewa. Na hivyo maelekezo ya kidini yanapatikana katika fatwa za Mafaqihi, maandishi ya Maulamaa, mazungumzo ya makhatibu, na katika rai na misimamo ya viongozi na shakhsiya za kidini.

Na hapa katika maelekezo ya kidini hakuna utukufu wala umaasumu, kwani ijtihadi inaweza kupatia na kukosea, na mujtahidi anaeleza kiwango cha ufahamu wake na uwelewa wake, kama am-

bavyo anaweza kuathirika na hali ya kinafsi na kijamii, hali ambazo huakisi rai zake na mawazo yake. Kama ambavyo sehemu kubwa ya maelekezo ya kidini ya kileo hayatoki kwa mafaqihi wenye ijtihadi bali ni kutoka kwa watoa mawaidha na makhatibu wa kawaida tu, na kutoka pande zinazojitolea kuendesha mambo ya kidini, bila kujali uwezo wao, usafi na utakasifu wao. Na kwa hiyo maelekezo ya kidini yanakubali kukosolewa na kusawazishwa kwa sababu ni zao la mwanadamu na matokeo ya binadamu, ama nususi za kidini zenyewe ni wahyi wa Mwenyezi Mungu au ni maneno kutoka Kwake.

Ni sahihi kwamba maelekezo ya kidini yanategemea nususi za kidini na hoja zake hutolewa humo. Lakini hilo linatimia kupitia ufahamu na tafsiri ya nasusi. Fahamu hii na tafsiri hii inakubali kuchukuliwa na kuachwa. Kuna tafsri za baadhi ya nususi za kidini hazina maudhui na umakini, au zinazitoa nususi kutoka kwenye fuo lake na mtiririko wake na kuzipeleka nje ya mshikamano wake mzuri wa ujumbe na makusudio ya sharia. Kama ambavyo baadhi ya nususi za sunna zinazotegemewa katika tafsiri hizo zinahitaji kuhakikiwa na kupata matumaini ya kuthibiti kutokea kwake na usahihi wa kupokewa kwake.

Na kati ya muonekano wa kushindwa na kuwepo kasoro katika hali ya jamii zetu ni uduni wa nafasi ya mwanadamu, kuporomoka kiwango cha kuthamani heshima yake na haki zake, na kuhami utu wake, kiasi kwamba ummah wetu umekuwa unachukua nafasi ya kwanzakatika ripoti ya uvunjaji wa haki za binadamu katika kiwango cha kimataifa, sio tu katika upande wa utawala wa kisiasa, bali hata katika upande wa kijamii kwa ujumla. Kuna ugaidi wa kifikra unaopora uhuru wa kutoa rai na mawazo, kuna ubaguzi dhidi ya mwanamke unaofanya kuwa ni mtu wa daraja la pili, kuna ukatili dhidi ya watoto unaokandamiza utu wao, na kuna mtazamo duni wa kumdharau tunaye tofautiana naye katika suala lolote kati ya mas’ala yenye tofauti.

Na kutokana na mazingira haya imechipuka mielekeo ya kigaidi yenye kutisha inayotumia mabavu na ukatili kwa kuangamiza nafsi, kukata vichwa, kuwateka wasio na hatia na kuwadhuru raia, yote hayo kwa jina la dini na chini ya nembo ya Uislamu na kwa anwani ya kutetea matukufu ya ummah.

Uvunjaji huu mbaya wa haki za binadamu katika jamii za Kiislamu, na ujahili huu wa kutokuthamini na kuheshimu heshima ya binadamu na thamani yake, yanapotokea yote hayo kwa maneno na visingizio vinavyonasibishwa na dini, ni jambo la kawaida maelekezo ya kidini yawe katika kizimba cha kuhojiwa na kutuhumiwa.

Hakika hatuna shaka kwamba dini imetakasika na kuepukana na haya yote yanayotokea kwa jina lake na kunasibishwa kwake, kwani kusoma kwa usahihi nususi za kidini kunaweka wazi na bayana jinsi dini inavyojali kwa kina ubinadamu na utu wa mwanadamu, na jinsi inavyoheshimu kwa kina utu wake na haki zake, kwa kiwango ambacho hakuna mfano wake katika misingi mingine yoyote au tamaduni nyingine yoyote.

Na kisha hakika tunaweza kuyapima maelekezo ya Kiislamu ya kileo na kuyatathmini kwa mwanga wa nususi za kidini, kwa lengo la kutaka kujua kiwango cha kasoro na mapungufu yaliyo nayo katika suala la kujali ubinadamu wa mwanadamu na kuheshimu utu wake na haki zake.

Ni sahihi kwamba kutoa kwetu ushahidi kupitia nususi za kidini itakuwa ni kuelezea kwa namna nyingine juu ya ijtihadi kulingana na tulivyozifahamu na kuzifasiri nususi hizo, lakini ni ijtihadi inayokubalika kwa sababu inaafikiana na misingi ya ujumbe wa Mwenyezi Mungu na makusudio ya sharia, na inakubaliana na heshima ya ubinadamu na mantiki ya akili.

Hakika kuboresha maelekezo yetu ya kidini ya kibinadamu sio matakwa ya ukamilisho na wala sio kadhia ya pambizoni, bali ni dharura muhimu imo ndani ya kadhia ya ummah na mahitaji yake. Hakika njia ya kutekeleza majukumu ya kimsingi ya ummah ambayo ummah umechelewa sana katika kuyatekeleza na kuyatimiza, yanayoonekana zaidi ni haya yafuatayo:

Kwanza: Kuleta maendeleo katika kiwango cha kukuza ubinadamu katika jamii zetu ambazo mwanadamu anaishi katika hali duni, anakosa mambo ya msingi ya kujenga maisha matukufu na kuneemeka na haki zake za kibinadamu za kisharia.

Pili: Kuleta ufaulu katika kutengeneza uhusiano wenye amani baina yetu na wengine ndani ya ummah na ndani ya nchi, na baina yetu na wale walio nje ya ummah wetu na nje ya nchi zetu miongoni mwa ummah nyingine na tamaduni nyingine, ambapo jamii zetu zina kabiliwa na mkanganyiko wa uhusiano baina ya makundi yake na makabila yake, na ambapo ummah umeingia katika vita vya kugongana na tamaduni na mataifa mengine kwa sababu ya mielekeo ya ugaidi na kuchupa mipaka.

Tatu: Kuchangia katika kutumikia mambo ya kibinadamu katika kiwango cha kimataifa ili ummah uwe katika kiwango cha juu kitakacho jengwa kwa maadili ya Kiislamu, dhana zake, kaulimbiu zake za ujumbe wake mtukufu.

Hakika Qur'ani inaupatia Uislamu uhalali na ruhusa ya kuwahudumia binadamu wote:

وَمَآ أَرۡسَلۡنَٰكَ إِلَّا كَآفَّةٗ لِّلنَّاسِ بَشِيرٗا وَنَذِيرٗا وَلَٰكِنَّ أَكۡثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعۡلَمُونَ

**"Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mtoaji bishara na muonyaji, lakini watu wengi hawajui."** **(SuratSabai: 28)**.

**Na ni ujumbe wa rehema na amani kwa watu wote wa ulimwenguni:**

وَمَآ أَرۡسَلۡنَٰكَ إِلَّا رَحۡمَةً لِّلۡعَٰلَمِينَ ١٠٧

**"Na hatukukutuma ila uwe ni rehema kwa walimwengu wote."**
**(SuratAnbiyai: 107)**.

Na kwamba ummah wa Kiislamu ni wajibu uwe ni kiongozi wa kheri katika jamii ya kibinadamu:

كُنتُمۡ خَيۡرَ أُمَّةٍ أُخۡرِجَتۡ لِلنَّاسِ ١١٠

**"Mmekuwa ni umma bora mliotolewa kwa watu."** **(Surat Imran: 110)**.

Hivyo ni lazima maelekezo yawe yanauwezesha ummah kuwa katika nafasi hii, na Uislamu uupatie ulimwengu kwa kiwango hiki.

## NI KUTENGENEZA MATATIZO AU NI KULETA UFUMBUZI?

Jamii za Kiislamu zinasubiri maelekezo ya kidini, yatoe utatuzi naufumbuzi wa matatizo na changamoto ambazo zinazikabili. Nayo ni matatizo makubwa na changamoto za hatari, zinazoanzia kwenye ugumu wa malezi katika zama za utandawazi, ambapo umepungua uwezekano wa familia kuwaathiri watoto kutokana na athari za vyombo vya kisasa vya mawasiliano na matangazo ya chanel huru.

Zinapitia katika matatizo ya msambaratiko wa kifamilia, matatizo ya kiuchumi, kudidimia kwa uzalishaji, ukandamizaji wa ki-

siasa, kutoweka kwa ushirikiano wa wananchi, ukosefu wa utulivu naamani, na kuenea kwa mizozo na ugomvi.

Kisha zinajumuisha yale matatizo yanayozikabili jamii za Kiislamu kutokana na uadui wa kizayuni uliokalia moyo wa ummah tangu zaidi ya nusu karne, na vilevile jaribio la nguvu mbalimbali za ubeberu wa kiulimwengu kutaka kuutawala ummah na kupenyeza mamlaka yake. Changamoto na matatizo haya yanawajibisha ummah kuamka na kuandaa nguvu zake na uwezo wake na kuutumikisha uwezo wake ili kuivuka hali ya kutoendelea na kuungana na msafara wa ummah zilizoendelea, ambazo zinaneemeka kwa demokrasia na utulivu wa kisiasa, na zinashindana katika sekta za kielimu na maarifa, maendeleo na mabadiliko ya kiuchumi.

Na kuuamsha ummah na kuuandaa kwa ajili ya kupambana na matatizo na changamoto ni jukumu la msingi la maelekezo ya kidini. Lakini kwa masikitiko ni kwamba baadhi ya maelekezo ya kidini yanazalisha matatizo ya ziada kwa ummah, na kuuzuia kushughulikia na kukabiliana na changamoto za wakati wake uliopo, kwa kufukua na kuchochea matatizo ya kihistoria ya zamani ambayo yameuteketeza ummah.

Yalitokea katika historia yetu iliyopita, matukio na mizozo mingi ya kisiasa na kijamii, na mizozo ya kitheolojia na kifiqhi ikashamiri, na hali hiyo haikuwa mbali na ushawishi wa kisiasa. Ndio ni haki yetu kusoma historia na kusoma matukio yake na watu wake, na kujua vyanzo vya mielekeo na makundi ya kisiasa na kifikra ambayo yameasisiwa kwa misingi ya mgawanyiko wa madhehebu yaliyopo katika ummah. Lakini hiyo haimaanishi kwamba tubaki katika kibanda cha historia na kujificha katika handaki la mapambano na mizozo yake na kurejesha mfano wa vita vyake na mapigano yake kwa gharama ya maslahi ya leo na huzuni ya jamii iliyopo.

Hakika wafuasi wa kila madhehebu na fikra hujikuta wanajali suala la kuwalea watoto wao kulingana na ufuasi wao wa kidini na wa kimadhehebu, na wana haki ya kusema na kueleza rai zao na mielekeo yao na kuzalisha na kuendeleza utamaduni wa madhehebu yao. Kama ambavyo mijadala na midahalo baina ya mitazamo mbalimbali ni jambo la kisharia na linalotakiwa kwa ajili ya kukuza maarifa na kupevusha rai na kupembua ukweli. Lakini kuwalea watoto katika madhehebu haimaanishi kupanda chuki na mifundo katika nafsi zao dhidi ya watoto wa madhehebu mengine, na kuwahamasisha wao katika kuwachukia wengine, kama zinavyofanya baadhi ya silabasi za masomo ya dini, ambazo zinakiingiza kizazi kinachokua katika shimo la ikhitilafu za kimadhehebu, na kutengeneza katika nafsi zao hisia mbaya dhidi ya wengine, jambo ambalo linadhuru umoja wa taifa na usalama wa jamii.

Kama ambavyo sehemu kubwa ya hotuba za misikitini na Husainiya zinachukua mwelekeo wa kuwaandaa watu wa madhehebu dhidi ya madhehebu mengine. Na baadhi ya runinga na tovutizimeweka vipindi maalum vya kuchochea mijadala ya kimadhehebu kwa mwelekeo wa kueneza ubaguzi na kuendeleza ugomvi na mizozo kwa ajili ya kumwagia petroli katika moto wa fitina uliowashwa katika zaidi ya kituo kimoja. Hakika maelekezo ya kidini yamekuwa katika mwelekeo huu, ni chanzo cha matatizo ya ziada katika ummah, badala yakutoa ufumbuzi wa matatizo yake yaliyopo.

Hakika mkusanyiko mkubwa wa watu wa ummah unakusanyika katika minasaba ya kidini ili kusikiliza hotuba za makhatibu na walinganiaji ambazo pia zinarushwa kupitia chanel, jambo ambalolinatoa fusra nzuri ya kuwaelekeza watu katika mambo yatakayoimarisha misingi ya tabia njema katika maisha yao na kuwaongoza wao katika kuyashinda matatizo wanayokabiliana nayo katika sekta za malezi, katika uhusiano wa kifamilia na katika ugumu wa maisha,

na kuwahimiza wao kuelekea katika maarifa, kuzalisha na kujenga mustakabali uliobora.

Lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba hotuba nyingi ambazo zinatolewa katika mikusanyiko iliyojiandaa kinafsi kupokea na kuathirika na hotuba hizo, zinaelekea katika mwelekeo wa mambo ya ikhitilafu za kimadhehebu na kuhamasisha ubaguzi, jambo ambalo linatengeneza kwa watu mazingatio ya bandia, kwa kutoa kipaumbele katika vita vya kimadhehebu kabla ya changamoto zingine, na zinatengeneza katika nafsi zao hisia za uongo kuhusu dini, kwamba-hisia ya kuipenda dini na kuwa mfuasi mwaminifu wa itikadi haitimii isipokuwa kwa kuepukana na madhehebu mengine, kuwachukia, kuwabughudhi, na kuwalaani viongozi wake na shakhsiyati ambazo zinatukuzwa na madhehebu mengine, na kuwazingatia wao kuwa ni washirikina, wanabidaa, wapinzani au maadui wanyang'anyi wenye kuwafanyiauadui Ahlulbait (as).

Uhamasishaji huu wa kibaguzi unawazuia watu wa madhehebu mbalimbali kujishughulisha na yale yanayowakabili miongoni mwa ukandamizaji wa kisiasa, ufisadi wa kijamii na matatizo ya kimaisha. Hakika mienendo hatari inaendelea kusambaa katika jamii na kutishia amani yake ya kitabia na kijamii, kama vile kusambaa kwa mihadarati, makundi ya uhalifu, utumiaji wa mabavu, kusambaratika kwa familia, kushuka kwa kiwango cha elimu, kuongezeka kwa kiwango cha ukosefu wa kazi na ajira, na matatizo ya kitabia. Wakati hali ikiwa ndio hii bado maelekezo ya kidini yangali yanaishi katika medani nyingine kana kwamba hayahusiki na yanayobomoa misingi ya jamii miongoni mwa maradhi na milipuko yenye kuangamiza.

Na kilicho hatari kuliko hilo ni yale yanayoletwa na maandalizi haya ya ubaguzi ikiwa ni pamoja na kusambaa fitina na ukosefu wa utulivu na amani kama ilivyotokea katika nchi nyingi kama vile Pakistan na Iraki. Je, hawa wanaozalisha maelekezo

haya wanajua madhara na athari mbaya za maelekezo yao? Hakika baadhi yao wanatenda hayo kwa sababu ya ufahamu mbaya na mtazamo duni na finyu, wao wanadhani kwamba wanafanya vizuri na wanatenda mema. Na baadhi ya makhatibu hawana bidhaa isipokuwa mazungumzo haya ambayo wameyahifadhi na wamezoea kuyazungumza na wala hawapati wala hawajui kingine isipokuwa mazungumzo haya tu. Na baadhi wanasukumwa na malengo na maslahi na hivyo wanatekenya na kuamsha hisia za watu kwa uwasilishaji huu ili wapate wafuasi, ushawishi, umaarufu, na kutimiza malengo binafsi.

Na kuna anayewasilisha hotuba yake ya kibaguzi kwa agenda ya kisiasa ili kupata nafasi ya kisiasa au kutumikia chama au kundi, au kwa kuwa amesukumwa na nguvuya kisiasa ya ndani au ya nje, yenye maslahi katika kuchochea ikhitilafu na kuwasha moto wa fitina.

Pamoja na huzuni yote inayotusibu kwa kuongezeka hotuba za ubaguzi, isipokuwa ni wajibu wetu tuwekeze katika kukuza uelewa wa watu wa ummah wetu. Hakika watu wa Ulaya waliishi katika hali hii ambayo ummah wetu unaishi nayo hivi sasa, miongoni mwa ikhitilafu na mizozo ya kibaguzi, kikabilana kisiasa, lakini harakati za kukuza uelewa na maendeleo ambazo ziliongozwa na wanafikira, wataalamu na warekebishaji wa kidini katika jamii zao zimezaa matunda baada ya mapambano makali na kujitoa muhanga kukubwa, hatimaye wananchi wake wakavuka hali ya mapigano na kuuwana, wakaanzisha dola yao mpya juu ya msingi wa utaifa na ushirikiano wa wananchi, na wao hivi sasa wametengeneza umoja wao Umoja wa Ulaya, umoja mkubwa ambao unaunganisha nchi ishirini na saba ambazo mwelekeo wa wananchi wake ni wa kitaifa na wa kidini, ambapo lugha rasmi katika Umoja wa Ulaya zinafikia lugha 23, kama ambavyo pia

katika nchi zao kuna madhehebu yao kadhaa ya Kikristo ikiwa ni pamoja na madhehebuya Katholiki, Othodox na Prostanti, ukiongezea na wahamiaji wengine mbalimbali wana mielekeo yao ya kikabila, kitaifa na kidini.

Hakika ni juu ya viongozi wenye ikhilasi katika ummah huu kuingia katika mapambano ya kukuza na kusahihisha uelewa na kupiga vita ubaguzi kwa silaha ya kujiamini na kuwa na matumaini, na kuleta mabadiliko katika maelekezo yetu ya kidini ya kuelimisha, na tuwekeze juhudi nyingi katika kusambaza na kueneneza uwelewa sahihi ili mwelekeo wa ummah uelekee katika maendeleo na katika kujijenga, na kuvuka hali ya ukandamizaji na kudumaa.

Na njia haitakuwa imepambwa kwa mauaridi mbele ya maelekezo ya uelimishaji ya kukuza uelewa na kuleta umoja, kwa sababu nguvu zinazonufaika na hali ya kutoendelea na ikhitilafu zilizopo zitawasha moto kila upande na kila kona ili kuzingira na kuzuia maelekezo ya kurekebisha na kuelimisha yenye kukuza uelewa, hivyo haiwezekani kuepuka vita, na hilo ndio jukumu la warekebishaji katika kila zama na kila jamii.

## VIPAUMBELE VYA KUWASILISHA KATIKA MAELEKEZO YA KIDINI

Je, maelekezo ya kidini ni thabiti na katika nyakati zote nakatika jamii zote na wala hayabadiliki? Au hubadilika kulingana na wakati na sehemu, kwa maana ya kwamba wakati na eneo huakisi athari zake katika maelekezo haya? Hakuna shaka kwamba maadili na misingi ya Kiislamu katika asili yake inamiliki sifa thabiti na za kudumu lakini maelekezo ya Kiislamu yenyewe ni mfumo na mbinu za kuwasilisha misingi hiyo na kuieleza kwa watu.

Na kutokana na kutofautiana na kiwango cha maarifa ya watu na kutofautiana nyakati ambazo wanaishi nazo, ni lazima maelekezo nayo yabadilike na yawe tofauti upande wa vipaumbele vinavyopasa kutiliwa mkazo na kutatuliwa, na pia upande wa njia za kuwasilishia, kufikishia na kuelezea. Mazungumzo ya kuongea na watu wa kawaida yanatofautiana na mazungumzo na jopo la wenye elimu, na mazungumzo katika mkusanyiko wa kidini wa watu wenye kushikamana na dini yanatofautiana na unayozungumza katika mkusanyiko wa watu wasioshikama na na dini. Hali ya kivita na mapigano inalazimisha lugha maalumu kwa ajili ya kuhamasisha, wakati ambapo nyakati za kawaida na za amani zina lugha nyingine.

Na kila jamii ina matatizo yake yanayotokana na mazingira yake na hali yake, kama ambavyo kila zama ina mambo yake yanayotokana na kiwango cha mabadiliko ya maisha katika zama husika. Na haipasi khatibu na mwasilishaji wa maelekezo ya kidini kutojua matatizo na mambo hayo au kuwasilisha utatuzi wa tatizo lisilokuwepo katika zama husika au jamii husika. Ni sahihi kwamba kuna kiasi cha ushirikiano katika mambo na mahitaji ya kifikira na mwenendo baina ya jamii mbalimbali, lakini kuna tofauti pia inayolazimishwa na tofauti za nyakati na za mazingira. Na hata katika mambo ya kushirikiana ambayo kila jamii inayahitaji katika kila zama ili kuyatatua, kama vile mas'ala ya kiitikadi, hakika mfumo wa uwasilishaji na mbinu zake zinatofautiana kati ya zama na nyingine na kati ya jamii na jamii nyingine.

Mazungumzo ya Qur'ani tukufu kutoka katika maelekezo ya Manabii na Mitume kwa ummah zao na watu wao ni ushahidi na dalili bora, kwani wote wanalingania kwenye tauhidi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na ibada yake, lakini nukta ya kusisitizia na mfumo wa uwasilishaji unatofautiana kati ya Nabiii mmoja na mwingine

kulingana na kutofautiana hali ya watu na jamii. Nabii wa Mwenyezi Mungu Ibrahim (as) katika maelekezo yake kwa watu wakeanatilia mkazo juu ya upagani wao na kuabdu kwao masanam, kama yalivyokaririwa hayo katika sehemu nyingi katika Qur'aniTukufu, kama vile kauli yake (swt):

وَٱتۡلُ عَلَيۡهِمۡ نَبَأَ إِبۡرَٰهِيمَ ﴿٦٩﴾ إِذۡ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوۡمِهِۦ مَا تَعۡبُدُونَ ﴿٧٠﴾ قَالُواْ نَعۡبُدُ أَصۡنَامٗا فَنَظَلُّ لَهَا عَٰكِفِينَ ﴿٧١﴾ قَالَ هَلۡ يَسۡمَعُونَكُمۡ إِذۡ تَدۡعُونَ ﴿٧٢﴾ أَوۡ يَنفَعُونَكُمۡ أَوۡ يَضُرُّونَ ﴿٧٣﴾ قَالُواْ بَلۡ وَجَدۡنَآ ءَابَآءَنَا كَذَٰلِكَ يَفۡعَلُونَ ﴿٧٤﴾

**"Na wasomee habari za Ibrahim. Alipomwambia baba yake na kaumu yake: Mnaabudu nini? Wakasema: Tunaabudu masanamu nasi tutaendelea kuyanyenyekea. Akasema: Je yanawasikia mnapoyaita? Au yanawafaa au yanawadhuru? Wakasema: Bali tumewakuta mababa zetu wakifanya hivyo hivyo." (SuratShuaraa: 69 – 74).**

Ama Nabii wa Mwenyezi Mungu Musa (as) alipambana tangu mwanzo wa ulinganiaji wake kulingana na inavyonukuu Qur'ani Tukufu katika sehemu zaidi ya moja, katika kukabiliana na ukandamizaji wa Firaun na uasi wake, kama vile kauli yake (swt):

هَلۡ أَتَىٰكَ حَدِيثُ مُوسَىٰٓ ﴿١٥﴾ إِذۡ نَادَىٰهُ رَبُّهُۥ بِٱلۡوَادِ ٱلۡمُقَدَّسِ طُوًى ﴿١٦﴾ ٱذۡهَبۡ إِلَىٰ فِرۡعَوۡنَ إِنَّهُۥ طَغَىٰ ﴿١٧﴾

**"Je, imekujia hadithi ya Musa? Alipomwita Mola Wake katika bonde takatifu la Tuwaa: 'Nenda kwa Firauni. Kwani hakika yeye amepituka mpaka.'" (Surat Nazia'ti: 15 – 17).**

**Pamoja na kuwepo masanamu na wapagani katika zama za Nabii Musa (as) kama inavyoashiria hilo kauli yake (swt):**

وَجَٰوَزۡنَا بِبَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ ٱلۡبَحۡرَ فَأَتَوۡاْ عَلَىٰ قَوۡمٖ يَعۡكُفُونَ عَلَىٰٓ أَصۡنَامٖ لَّهُمۡۚ قَالُواْ يَٰمُوسَى ٱجۡعَل لَّنَآ إِلَٰهٗا كَمَا لَهُمۡ ءَالِهَةٞۚ قَالَ إِنَّكُمۡ قَوۡمٞ تَجۡهَلُونَ ١٣٨

**"Na tukawavusha bahari wana wa Israil na wakakawafikia waliokuwa wakiabudu masanamu yao; wakasema: Ewe Musa! Hebu nasi tufanyie waungu kama hawa walivyo na waungu. Akasema: Hakika nyinyi ni watu wafanyao ujinga."** **(Suarat al-A'araf: 138)**.

Isipokuwa mazingatio ya kulingania yalikuwa yanalenga katika kukabiliana na Firaun na ukandamizaji wake. Wakati tunakuta katika ujumbe wa Nabii wa Mwenyezi Mungu Lut(as) mazingatio ya msingi ni kupambana na uvukaji mipaka katika matamanio ya kijinsia na ufisadi wa kitabia. Hiyo ni kwakuwandio upotovu ulioenea katika jamii yake wakati huo. Anasema (swt):

وَلُوطًا إِذۡ قَالَ لِقَوۡمِهِۦٓ أَتَأۡتُونَ ٱلۡفَٰحِشَةَ مَا سَبَقَكُم بِهَا مِنۡ أَحَدٖ مِّنَ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٨٠
إِنَّكُمۡ لَتَأۡتُونَ ٱلرِّجَالَ شَهۡوَةٗ مِّن دُونِ ٱلنِّسَآءِۚ بَلۡ أَنتُمۡ قَوۡمٞ مُّسۡرِفُونَ ٨١

**"Na Lut alipowaambia watu wake: Je, mnafanya uchafu ambao hajawatangulia yeyote kwa hilo katika walimwengu? Hakika nyinyi mnawaendea wanaume kwa matamanio badala ya wanawake! Bali nyinyi ni watu warukao mipaka."** **(Surat al-A'araf: 80 – 81).**

Na katika kupamabna na ufisadi na dhulma ya kiuchumi ulioenea katika kaumu ya Madiyan ulinganiaji wa Nabii Shuaib ulitilia mkazo juu ya uadilifu wa kiuchumi:

وَإِلَىٰ مَدۡيَنَ أَخَاهُمۡ شُعَيۡبٗاۚ قَالَ يَٰقَوۡمِ ٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مَا لَكُم مِّنۡ إِلَٰهٍ غَيۡرُهُۥۖ قَدۡ جَآءَتۡكُم بَيِّنَةٞ مِّن رَّبِّكُمۡۖ فَأَوۡفُواْ ٱلۡكَيۡلَ وَٱلۡمِيزَانَ وَلَا تَبۡخَسُواْ ٱلنَّاسَ أَشۡيَآءَهُمۡ

**"Na kwa wa Madian (tulimpeleka) ndugu yao Shuaib akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, nyinyi hamna Mungu mwingine zaidi Yake. Hakika umewajia ubainifu kutoka kwa Mola Wenu. Basi kamilisheni kipimo na mizani, wala msiwapunje watu vitu vyao, wala msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kutengenea kwake. Hayo ndiyo bora kwenu ikiwa nyinyi mmeamini." (Surat al-A'araf: 85).**

Hakika huku kutofautiana kwa nukta za kusisitizia na kutilia mazingatio katika ulinganiaji wa Manabii (as) hakuna tafsiri isipokuwa ni kwa sababau ya kutofautiana kwa nyakati za jamii na mazingira yake ambayo yalikuwepo wakati ujumbe wao ukiteremka, na hivyo zikasababisha kila Nabii kukabiliana na kadhia iliyo muhimu zaidi na tatizo lililojitokeza zaidi katika zama zake na katika jamii yake.

Bali yanaweza kutofautiana maelekezo ya Nabii mmoja yanapobadilika mazingira anayoishi nayo. Mwanzoni ulinganiaji wa Nabii Musa (as) ulitilia mkazo katika kukabiliana na ukandamizaji wa Firaun na uasi na uovu wake, lakini baada ya kuhiliki Firaun na Nabii Musa kuwakomboa Bani Israil kutokana na dhulma yake na mabavu yake, maelekezo ya ujumbe wake yalielekea katika kuondoa mianya na nukta za udhaifu zilizojitokeza katika miundombinu ya jamii ya Kibani Israili.

Tunatuka hayo vilevile katika maelekezo ya ujumbe waUislamu ambapo zinagawanyika Sura za Qur'ani na aya zake katika sehemu mbili: Za Makka na za Madina. Kinachoonekana ni kwamba kuna tofauti kati ya aya zilizoteremka Makka na aya zilizoteremka Madina, katika upande wa aina ya mambo yaliyowasilishwa na njia ya uwasilishaji.

Maulamaa wamejitahidi katika kutafuta pande za kutofautiana baina ya aya za Makka na aya za Madina na kuweka vigezo na kanuni za kuzitofautisha. Zarkishiy anasema:

"Hakika kila Sura ambayo humo kuna: 'Enyi watu'na hakuna humo 'Enyi mlioamini'basi ni ya Makka. Na katika Hija kunatofauti. Na kila Sura ambayo humo kuna 'Hapana' basi ni ya Makka na kila Sura ambayo mwanzo wake kuna herufi za *Muujam*, basi ni ya Makka isipokuwa Surat al-Baqarah na AaliImraan, na katika Ra'adkunatofauti. Kila Sura ambayo humo kuna kisa cha Ibilisi na Adam basi ni ya Makka, isipokuwa al-Baqarah. Na kila Sura humo kuna kutajwa wanafiki basi ni ya Madina isipokuwa al-Ankabuti. Amesema Hisham al-Kalibiy kutoka kwa baba yake: 'Kila Sura kumetajwa humo adhabu na faradhi basi ni ya Madina. Na kila aya ambayo humo inataja karne zilizopita basi ni ya Makka.'"[28]

Na anatilia mkazo Sheikh Abdurahman Habnakatu al-Maydaniy suala la nususi za Qur'ani kuchunga mazingira ya kibinadamu yaliyokuwepo wakati wa kushuka kwake, anasema:

"Na tunaona kwamba muundo wa aya za Qur'ani zilizoshuka katika mazingira yazama za Madina umetofautiana na muundo wake katika mazingira ya zama za Makka, kwani ufafanuzi wa kidini umekusanyika katika aya ndefu na Sura ndefu na umekuwa kimbilio la kufafanua yaliyokuwa ni muhtasari katika zama za Makka, na kufafanua vipengele ambavyo vilikuwa vinakusanya mengi katika muundo wa Makka. Na muundo wa zama za Madina umeangalia njia za kumwezesha mtu kufikiri mazingira ya Madina ambayo humo kuna makabila matatu ya Ahlul-Kitab Mayahudi. Mwenye kutafakari katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu anaweza kwenda sambamba na hatua za kuteremka kwake na kugundua suraya kuoana baina ya nususi za Qur'ani na mazingira ambayo humo imeshuka, mazingira ya kibinadamu, kiwakati na kisehemu, na hali za kinafsi na kifikra, za mtu mmoja mmoja na jamii pia, hali ambayo haiwezekani ku-

[28] Muhammad bin Abdillahi Zarakishiy katika *Burhan fiy ulumil- Qur'an* Jz. 1 uk. 188 chapa ya 1988 , Beirut ya Darul Jiyl

tosheka na nadharia za jumla na sehemu za muhtasari zinazohitaji ufafanuzi."[29]

Kwa kujengea juu ya yaliyotangulia, hakika ni juuya walinganiaji wa Kiislamu kutizama hali za zama zao kwa jicho la uzingativu wa kina, wafuatilie mabadiliko yake ya kielimu na mielekeo yake ya kifikra na matatizo yake ya kijamii, ili wawe ni wenye kuweza kutoa maelekezo yanayofaa kwa watoto wa zama hizi na yanayoathiri kwao.

Na katika upande mwinginehakika pamoja na hali ya mawasiliano na utandawazi wa kiulimwengu uliopo baina ya jamii za kibinadamu, isipokuwa ni kwamba inawezekana baadhi ya mazingira na jamii zikawa na sifa maalum zinazohusu eneo husika, katika mambo yake na ada zake na katika matatizo yake na uelewa wake, hivyo maelekezo yanahitaji yaguse uhalisia wa jamii husika moja kwa moja na kutoa utatuzi na utaratibuwa yale wanayoishi nayo miongoni mwa maumivu na matarajio.

Na kati ya changamoto zinazozikabili baadhi ya jamii zetu ni kwamba hakuna walinganiaji na wanafikra wakatutosha wanaoishi katika mazingira husika, wanaoweza kupembua na kubainisha mahitaji ya kifikra na kiutamaduni ya jamii husika, ili kutoa hotuba na maelekezo yanayofaa, ambayo yatawezesha jamii hizo kukabiliana na changamoto zilizopo mbele yao, na kupasua njia kuelekea kwenye maendeleo na ufaulu.

Ni sahihi kwamba kuwepo kwa maelekezo ya kidini ya jumla yanayo jumuisha mawaidha na ukumbusho na mafunzo ya hukumu za kifiqhi ni jambo lenye faida. Lakini hilo halijazi wala kuziba pengo la haja ya uwasilishaji wa kifikra unaojibu changamoto ambazo zinakabili jamii katika hali yake ya kisiasa, kiutamaduni na kijamii, na

[29] Abdurahaman Hasan Habnakatu al-Maidaaniy katika *Qawaid Tadabur al-Amthali* chapa ya pili 1989 Damascus Darul-Qalam uk. 56- 58

kukidhi haja ya ratiba na mipangilio ya kazi inayomsaidia kuvuka nukta za udhaifu wake na kukuza humo sehemu za nguvu na maendeleo.

Na wakati mwingine pengo hili hujazwa kwa kunufaika na yale yaliyowasilishwa na kupendekezwa katika sekta za jamii nyingine, miongoni mwa fikra na ratiba, bila kuangalia umahususi wa sehemu na eneo, jambo ambalo husababisha aina za mgongano katika baadhi ya nyakati. Kwani pengine fikra inakuwa ni yenye kufaa sana katika hali ya jamii fulani, lakini haiendani pamoja na uhalisia wa jamii nyingine, au jamii hiyo inakuwa inahitajia zaidi fikra isiyokuwa hiyo, kama ambavyo baadhi ya ratiba na mipangilio inaweza kuwa inafaa kwa wakati fulani bila ya kufaa kwa wakati mwingine, na kufaa katika mazingira fulani bila yakufaa katika mazingira mengine.

Kwa hakika hapa tunakusudia yale mambo yanayotokana na umahususi maalum au yanayoathirika kwa kutofautiana mazingira. Ama fikra ya jumla na ratiba za jumla ambazo zinavuka umahususi, hizo ziko nje ya mtiririko wa angalizo hili.

## MAELEKEZO YA KIDINI NA CHANGAMOTO ZA NDANI

Changamoto kubwa mbele ya maelekezo ya Kiislamu katika muongo uliopita ilikuwa ni kupambana na makundi yanayounyemelea Uislamu.

Mwanzoni mwa karne ya tisa Miladia walinganiaji wa Kiislamu walitambua hatari ya wahubiri wa Kinaswara wa Ulaya ambao waliendelea kuteka nchi za Kiislamu, na pembezoni mwake kulikuwa na harakati nyingi za mustashiriqina ambazo zinalenga kuwa-

tia shaka Waislamu kuhusu dini yao na kuchochea shubhatikuhusu Qur'aniTukufu, sira ya Nabii (s.a.w.w.), dhana na sharia ya Uislamu, shubhati hizo zilijaa katika vitabu vingi vya mustashirqina na katika mafunzo yao.

Walijitokeza wenye ikhilasi wenye kutambua kati ya Maulamaa wa ummah, kwa ndimi zao na kalamu zao na roho zao wakajibu mashambulizi haya maovu na wakatoa juhudi zao zote kusimama dhidi ya mawimbi makali, pamoja na uwezo wao mdogo ukilinganisha na nguvu za wavamizi ambao wanategemea bajeti kubwa na nguvu ya kiaskari, kisiasa na vituo vya utafiti na mipango madhubuti.

Na katika miongo ya mwanzo katika karne ya ishirini Miladia kulikuwa na vita nyingine inawasubiria walinganiaji wa Kiislamu, nayo ni mbaya zaidi kuliko vita ya wahubiri wa Kikirisito na shubhati za mustashiriqina, nayo ni kupambana na nguvu ya kijamaa na makundi ya wasio na dini, yenye uadui na dini, hiyo ni kwa sababu makundi mengi ya wasio na dini ambayo yalidhihiri katika nchi za Kiislamu yalichukua mwelekeo wa wapiganaji na maadui wa dini, tofauti na makundi mengi ya wasio na dini yaliyokuwepo katika nchi za Magharibi ambayo yalijihusisha na upagani tu wa kukataa dini.

Makundi haya yenye uadui yametengeneza mazingira ya chuki na upinzani wa hali mbaya isiyo na maendeleo kwa watu wa ummah, na yamejenga kaulimbiu za mapinduzi na mwamko yakilingania kwenye upinzani dhidi ya dini na kuepukana nayo, kwa sababu(kwa mtazamo wao) ni chanzo cha kutoendelea kwa ummah na kuporomoka kwake. Na makundi haya yameweza kuyavutia na kuyateka makundi ya vijana wa ummah wetu na hatimae wakafikia katika nafasi za utawala na uongozi katika baadhi ya nchi za Kiarabu na za Kiislamu, kupitia mapinduzi ya kijeshi na harakati za vyama vingi.

Hivyo vikawa ni vita vikali vya mabavu katika nyanja mbili za kifikra na kisiasa, ambavyo walikabiliwa navyo walinganiaji wa Kiislamu katika kuzing’oa serekali na mifumo iliyojitokeza kutoka katika makundi haya pinzani. Na kabla ya kumalizika karne ya ishirini, ukadhoofika msaada wamakundi haya na wakadhihiri viongozi wa medani ya Kiislamu, na zikapepea bendera za Kiislamu katika kila sehemu, ambapo watu wa ummah wakarejesha uaminifu wao katika dini yao baada ya kuyakukuta makundi hayo:

كَسَرَابٍ بِقِيعَةٍ يَحْسَبُهُ ٱلظَّمْـَٔانُ مَآءً حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءَهُۥ لَمْ يَجِدْهُ شَيْـًٔا وَوَجَدَ ٱللَّهَ عِندَهُۥ

﴿٣٩﴾

**“Ni kama sarabi jangwani, mwenye kiu huyadhania ni maji, hata akiyaendea hapati chochote. Na atamkuta Mwenyezi Mungu hapo.”**
**(SuratNuru: 39)**.

**Na hivi ndivyo zilivyoanza upya zama za Uislamu.**

Pamoja na kwamba kuna changamoto za nje ambazo bado zingali zimesimama mbele ya maelekezo ya Kiislamu, kinara ikiwa ni vita vya matangazo ya kiutamaduni yenye kuangamiza Uislamu, kwa kuelezea kuwa ni dini ya ugaidi na mabavu, matangazo ambayo yamevuka mila na desturi za uhusiano baina ya dini, tamaduni na ummah nyingine, kama inavyowakilisha hilo michoro ya katuni inayomkosea adabu Nabii Muhammad (s.a.w.w.) iliyochapishwa na gazeti la Denmark, kisha ikachapishwa tena mwaka huu na baadhi ya magazeti ya nchi za Ulaya, kitendo ambacho nichangamoto ovu yenye kuamshahisia za Waislamu na kuikosea adabu dini yao na heshima yao.

Pamoja na hayo, lakini mfano wa changamoto hizi za nje hazina hatari kubwa sana kiasi cha kulazimu kuziweka mwanzoni katika orodha ya changamoto na vipaumbele muhimu katika maelekezo ya

Kiislamu. Hakika mimi naitakidi kwamba maelekezo ya Kiislamu sasa hivi yanakabiliwa na changamoto za ndani ambazo ni muhimu zaidi na hatari zaidi katika mustakabali wa Uislamu na ummah, na hivyo ni lazima kuitikia na kunyanyuka na kuwa katika kiwango cha kukabiliana nazo. Na huenda changamoto za mwanzo kabisa zinazoongoza ni hizi zifuatazo:

**Kwanza: Kuzalisha utamaduni wa kujiendeleza na kujijenga:**

Maelekezo ya Kiislamu ni mahiri katika kuandaa watu dhidi ya maadui na dhidi ya hali ya ufisadi na upotovu, na hiyo ni kazi ya kuvunja na kubomoa. Lakini nini badali ambayo ni wajibu ummah kuielekea kwa ajili ya kujijenga katika upande wa kisiasa, kiuchumi na kijamii, na kujenga maarifa na kukuza tabia njema? Na namna gani Uislamu utaongoza vita vya maendeleo na kujijenga?Haya ni mambo ambayo yanahitaji jawabu la kina linalojumuisha ratiba ya kazi na vyombo vya utekelezaji, na utamaduni wa kujituma na uendeshaji.

**Pili: Uhusiano mzuri pamoja na wengine:**

Maslahi katika ulimwengu wa leo yameingiliana, ugomvi na mizozo sio lengo wala si mkakati wakudumu, bali ni dharura kadiri ya kukabiliana na uadui. Kama ambavyo Uislamu ni ujumbe bora na ni rehema kwa wanadamu wote. Kwa kuanzia hapa ni lazima kuzalisha maelekezo yanayosaidia kufungua majadiliano pamoja na wengine na ni lazima kueneza utamaduni wenye kuvutia ili kutengeneza uhusiano mzuri pamoja na wengine na ili kuvuka  athari za hatua za ugomvi na mizozo.

Ni sahihi kwamba kuna uadui bado ungali unaendelea dhidi ya Uislamu na ummah, lakini kinachotakiwa ni kudhibiti mapambano na ugomvi dhidi ya pande zinazofanya uadui badala ya kuufanyia uadui ulimwengu wote na kueneza ugomvi katika kiwango cha dini na maendeleo.

Kuna haja kubwa mno leo hii kwa ummah kuwa na utamaduni wa uhusiano wa ndani ulio mzuri, ambapo bado tungali tunaishi na athari za ugomvi wa zamani ambao ulitokea baina ya watangulizi wetu katika karne za mwanzo katika historia ya ummah, athari ambazo zinalipuka leo kwa muundo wa fitina na mizozo ya kibaguzi. Kama ambavyo bado zingali aina za utaifana ukabila ni kikwazo mbele ya umoja wa taifa na utulivu wa kisiasa katika nchi mbalimbali za Kiarabu na za Kiislamu.

**Tatu: Kudhibiti maelekezo na shughuli za kidini:**

Dini kukubalika na kuongezeka kwa maanawi ya kwa wanadini kunaweza kumsukuma mtu kwenye mwelekeo wa kukithirisha na kupindukia katika kuelekeza, na katika shughuli za kidini, hususan ukizingatia kwamba katika madhehebu mbalimbali za ummahkuna turathi zenye mielekeo kama hii.

Kama ambavyo baadhi ya nguvu za kuiga za kidini ambazo hazimiliki miradi ya maendeleo na mwamko, zinaweza kwenda mbio kutekenya hisia za jamii na huruma zao za kidini ili kuimarisha nguvu zake na misimamo yake, ili kupambana na uongezekaji wa nguvu za urekebishaji na uendelezaji. Na haiko mbali kwamba pia baadhi ya nguvu za nje au baadhi ya nguvu za ndani za kimaslahi zinaweza kuingilia njia kwa nia yakushajiisha mwelekeo wakukithirishana kupindukia ndani ya jamii ya kidini. Hakika hatari ya mwelekeo wakukithirisha na kupindukia ni kubwa katika mustakabali wa Uislamu na ummah, na kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu Mtukufu alizitahadharisha ummah zilizotangulia zisikithirishe na kupindukia katika dini, anasema (swt):

يَـٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَـٰبِ لَا تَغۡلُواْ فِي دِينِكُمۡ وَلَا تَقُولُواْ عَلَى ٱللَّهِ إِلَّا ٱلۡحَقَّۚ ﴿١٧١﴾

**"Enyi watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo haki."** **(Surat Nisaai: 171)**.

Na mwonekano muhimu wa hatari ya kukithirisha na kupindukia unaonekanakatika nukta zifuatazo:

a- Kupotosha dhana za dini, kuziondoa hukumu za kisharia kutoka katika madhumuni yake na kuziweka mbali na makusudio ya dini na malengo yake, na kuushughulisha ummah na hali za kiibada zisizo na athari, zinazotumia juhudi katika kutengeneza hali ya ukinaifu wa uongo na hisia za uongo za kwamba mtu ametekeleza wajibu wake katika dini.

Kuzama katika pande za ghaibu kwa gharama ya akili na kuchunga sunnah za Mwenyezi Mungu za mazingira na maisha, jambo ambalo limeimarisha hali ya utegemezi, uvivu na uzembe, na kutotafiti na kutatua matatizo ya maisha kama yalivyo, na hivyo kufungua njia mbele ya masoko ya hila na uongo ambayo yanadai kuwa yana uwezo wa kutoa ufumbuzi mbalimbali wa maradhi ya kimwili na matatizo ya kinafsi na mambo ya kijamii.

Kushajiisha hali ya kutomheshimu na kumshadidia mwingine wa nje na wa ndani pia, kwa sababu ya ikhitilafu za kiitikadi na za kihistoria, na kughafilika na sehemu za makutano na ushirikiano. Sasa tuna makhatibu hodari wa kuchochea ikhitilafu za makundi na wenye kuhamasisha chuki na bughudha baina ya watu wa ummah, chanel zimewapa fursa nzuri ya kupaza sauti zao na kusambaza sumu zao katika sehemu mbalimbali.

Kufanya vitendo vya ugaidi wa kifikra dhidi ya kila rai ya anayekhalifu, na kumtuhumu kwa uasi na bidaa, ni kati ya mambo ambayo yanasimamisha harakati za ijtihadi na mwenendo wa mabadiliko na maboresho.

Hakika changamoto hizi za ndani zinasababisha maulamaa na walinganiaji wanaozijua vizuri, kuelekeza hotuba zao na mazingatio

yao katika kupambana nazo, na kuwaelimisha watu wa ummahyale yanayotumikia maslahi yao, na kuulinda ujumbe mtukufu wa Kiislamu usichezewe na wale wanaokithirisha na kupindukia.

Hakuna shaka kwamba hiyo ni kazi kubwa ambayo inazungukwa na ugumu mkubwa, kwa sababu wenye kulingania hali ya kushadidia na kupindukia huamsha hisia za kidini za watu wakawaida, na hutegemeza hali hiyo kwenye rai na visingizio vyenye mizizi katika hazina za madhehebu mbalimbali, na hudhihirisha nafsi zao kuwa ni watetezi wa itikadi na walinzi wa dhana zake, na wala hawasiti kutia shaka katika dini ya yeyote anayetofautiana nao hata katika ufafanuzi mdogo tu.

**Kulingania kwa Busara:**

Nabii (s.a.w.w.) alishazungumzia kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu juu ya sifa muhimu ya mfumo wake katika kulingania kwa Mwenyezi Mungu, nayo nikumiliki busara, anasema (swt):

قُلْ هَٰذِهِۦ سَبِيلِىٓ أَدْعُوٓا۟ إِلَى ٱللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا۠ وَمَنِ ٱتَّبَعَنِى ۖ وَسُبْحَٰنَ ٱللَّهِ وَمَآ أَنَا۠ مِنَ
ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٨﴾

**“Sema: Hii ndiyo njia yangu ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa busara, mimi na wanaonifuata. Na ametakasika Mwenyezi Mungu! Wala mimi si katika washirikina.”** **(Surat Yusuf: 108)**.

Kama ambavyo mwanadamu anahitaji jicho ili aone vitu vya kimaada katika maisha haya na ili aweze kutembea katika njia yake ili kuepuka kupotea na kutumbukia katika shimo na maporomoko, vivyo hivyo anahitaji maarifa na uelewa ili kunyoosha rai na fikra na kupambanua baina ya mapito ya kheri na maporomoko ya shari na ufisadi. Na hio ndio busara. Na mlinganiaji kuwa na busara katika daawa yake inamaanisha mambo mawili:

**Kwanza:** Jinsi alivyo na uhakika na fikra yake na ilivyo wazi kwake, ambapo haifai kwa mlinganiaji kutoa fikra ambayo hajaifanyia juhudi katika utafiti wake na wala hajapata uhakika wa usahihi wake. Na wala haipasi kuthubutu katika hotuba zake kuwasilisha jambo lililoenea na kutapakaa bila ya kuhakiki na kupembua.

Na kinachosikitisha sana ni kukuta baadhi ya maulamaa na walinganiaji wananukuu kwa watu riwaya za kihistoria, rai za itikadi na mas'ala yenye athari katika akili za watu na nyendo zao, bila ya juhudi yoyote ya kupata usahihi wa nukuu hiyo, kwa kutegemea tu kusikia kutoka katika hotuba za wengine au kuchukua katika rejea zisizo tegemewa au kwa kuitikia raghba ya wasikilizaji. Hakika mbinu za utafiti na vyombo vya maarifa vimekuwa vingi na vinapatikana, hivyo hakuna udhuru kwa wazembe na wavivu.

**Pili:** Ni kujua hali ya nje ya jamii ambayo inaguswa na fikra zinazowasilishwa, sio kila fikra sahihi inafaa kuelezwa katika kila zama na kila sehemu, pengine makusudio ya hekima katika kulingania katika tamko la aya tukufu:

ٱدْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلْحِكْمَةِ وَٱلْمَوْعِظَةِ ٱلْحَسَنَةِ ۖ وَجَٰدِلْهُم بِٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ ۚ

**"Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. "** **(Surat Nahli: 125)**.

Ni kuchagua kauli inayofaa nakatika sehemu inayofaa.

Hapa walinganiaji katika kila jamii wanahitaji kuchunguza hali za jamii zao na kusoma hali za mazingira wanayoyashughulikia, ili waanzie hotuba zao za kidini katika njia iliyodurusiwa na watilie mkazo katika vipaumbele.

Na Allammah Sheikh Adullahi Allamiy al-Ghaziy Dimishiqiy, mwalimu wa masomo ya tafisiri katika Jaamiul-Umawiy huko Damas-

cus (aliyefariki mwaka 1355 Hijiria/ 1936) ameshazungumzia aya hii tukufukatika kitabu chake kizuri *Muutamar Tafsir Surat Yusuf*:

قُلْ هَٰذِهِۦ سَبِيلِىٓ أَدْعُوٓا۟ إِلَى ٱللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا۠ وَمَنِ ٱتَّبَعَنِى ۖ وَسُبْحَٰنَ ٱللَّهِ وَمَآ أَنَا۠ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٨﴾

**"Sema: Hii ndiyo njia yangu ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa busara mimi na wanaonifuata. Na ametakasika Mwenyezi Mungu! Wala mimi si katika washirikina." (Surat Yusuf: 108)**.

Amesema chini ya anwani**'Wengi kati ya walinganiaji wa sasa si wenye busara':**

"Nabii (s.a.w.w.) alikuwa analingania kwa Mwenyezi Mungu kwa busara na vivyo hivyo Makhalifa wake na maulamaa waliotangulia na maimamu wenye kujitahidi na maulamaa wengine wema, lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba wengi kati ya walinganiaji wa leo hawana busara wala uelewa, kwa sababu wamechanganya virusi na itikadi za kidini na wameingiza bidaa na tabia mbaya katika rejea za Kiislamu, wanawafundisha wajinga mafunzo ya uongo, wamechanganya mabaya kwa mazuri, kama ambavyo wamewafundisha taawili batili ambazo zimechanganya haki na batili hadi jaala ikawa tauhid, na kupinga sababu ikawa ni imani, na kuacha amali yenye manufaa ikawa ni tawakuli, na kujua ukweli ikawa ni ukafiri na ulahidi, na kumuudhi anayekukhalifu katika madhehebu ikawa ni dini, na kutojua elimu na kujisalimisha kwenye ukhorafi ikawa ni wema, upungufu wa akili na ubovu wa rai ikawa ni uongozi na utawa, na udhalili na fedheha ikawa ni unyenyekevu, na unyonge na kukubali udhalimu ikawa ni ridhaa na kujisalimisha, na kuiga kwa upofu kwa kila kinacholetwa ikawa ni elimu na yakini."[30]

[30] Abdillahi al-Alamiy al- Ghaziy katika*Muutamar Tafsir Surat Yusuf(as)* Juz. 2, uk. 14 29

Haya ndio aliyoyaandika Sheikh mtukufu kabla ya miongo nane juu ya walinganiaji wa zama zake, je walinganiaji wa leo wana hali bora zaidi kuliko hao? Haya ndio tunayoyatazamia na kuyatarajia.

## MAREKEBISHO YAKITAMADUNI NA NAMNA YA KUISHI NA WATU

Inaonesha kwamba idadi kubwa ya maulamaa na walinganiaji huzikuta nafsi zao zikilazimika kufuata baadhi ya fikra na rai na vitendo vilioenea katika medani ya kidini, licha ya kwamba wao wenyewe hawajakinaika na usahihi wake, kwa sababu rai hizo au fikra hizo hazitokani na dalili yenye kuzingatiwa, au kwa kuwa zinapingana na mizani ya kisharia na maslahi ya ummah. Lakini wao hujizuia kutoa rai zao juu ya jambo husika, bali huonesha kuafikiana nalo na kuziunga mkono rai au fikra hizo kinyume na imani yao na kinyume na yale wanayoamini katika maamuzi ya nafsi zao. Na hudhihirisha hali hiyo kwa waliokaribu nao na katika vikao maalum na vya siri. Na hali hii ina visingizio na sababu, na huenda zinazojitokeza zaidi ni hizi zifuatazo:

1. Kuchunga upande wa kisiasa katika yale yanayohusiana na rai ambazo zinapinga maelekezo ya serikali inayotawala, na mwanachuoni na mubaligh anaogopa kutoa rai inayokhalifu maelekezo ya serikali au kupinga rai inayokubaliwa na serikali ili kuepuka kugongana na kupingana nayo, na kuepuka hatari na madhara yanayoweza kupatikana.
2. Na kujihadhari na nguvu za kimila ambazo zinapinga aina yoyote ya kuhakiki fikra za kiitikadi na rai za kifiqhi zilizoenea, na zinazopambana na mabadiliko na mageuzi yoyote

chapa ya kwanza ya 1381 Hijiria/1961 Damascus Darul-fikir.

yanayofanywa katika mila na vitendo vya kidini vilivyopo. Na mwanachuoni anapojaribu kukhalifu na kukosoa, hakika wao wanamwelekezea silaha ya fatwa ambayo inatia shaka katika dini yake na inamhukumu kwa bidaa na upotovu, na kuuwa shakhisiya yake na kudumaza wajibu wake na kudhibiti athari yake.

3. Kuogopa ghadhabu ya jamhuri, ambao aghlabu hushikamana na urithi wao na yale ambayo wamekua nayo miongoni mwa fikra na mazoea, ada na mila. Na mwanachuoni anapozungumza yale yanayokhalifu fikra hizo na mazoea hayo yaliyoenea basi kwa hakika anahatarisha nafasi yake ndani ya jamhuri hiyo. Hususan ikiwa watu wanaishi katika changamoto za kidini kutoka kwa wengine, hakika anajitenga na sifa zake zote kwa sababu ya kuhofia heshima yake na anaangalia jaribio lolote la kubadilisha na kugeuza kana kwamba ni hatua moja katika njia ya kujishusha mbele ya mwingine na kutoweka ndani ya jamhuri hiyo.

Mambo na sababu kama hizi huwasukuma hawa wanachuoni na walinganiaji kunyamaza, kwa ajili ya usalama na kuepuka matatizo, na kuhifadhi nafasi zao za kijamii. Na baadhi wanaweza kutoa visingizio wanavyovizalisha wao wenyewe kwamba ongezeko ambalo linaweza kuzaliwa na jaribio la kutaka kusahihisha, ni lenye madhara zaidi kuliko madhara ya hali iliyopo, nayo inaweza kusababisha ikhitilafu na kusambaratisha umoja wa jamii, inaweza kufungua mlango mbele ya maadui kushambulia vitu vilivyo thabiti na misingi. Kisha hakika mwanachuoni wa kidini akikosa kuaminiwa na watu basi nafasi yake itamalizika na athari yake itakosekana.

Kama ambavyo wanaweza kutia shaka katika uwezekano wa kufanikisha marekebisho na mabadiliko, na katika uwezo wa warekeb-

ishaji wa kuweza kufanikisha mabadiliko ndani ya jamii, na wanatoa dalili kupitia baadhi ya maulamaa warekebishaji ambao waliporomosha heshima yao na utu wao kwa thamani duni, na wale waliofeli katika baadhi ya majaribio ya kurekebisha katika upande wa kifikra na kijamii. Na pamoja na hadhi ya baadhi ya visingizio hivi isipokuwa kuna nukta ambazo ni wajibu kuziangalia kwa mazingatio wakati wa kutatua msimamo huu.

**Kwanza:** Jukumu la kisharia ambalo linawabebesha maulamaa na walinganiaji kazi ya kubainisha hukumu na dhana sahihi ya kidini, ambapo aya mbalimbali za Qur'aniTukufu na idadi kubwa ya Hadithi na nususi tukufu zinahadharisha kuficha elimu na maulamaa kunyamazia hali ya upotovu na ufisadi, na kwamba ni wajibu wao waamke na kutekeleza jukumu la tablighi, kuongoza, kurekebisha, kuamrisha mema na kukataza maovu, na wala wasizembee katika jukumu hilo kwa kuogopa watu au kwa ajili ya kuhifadhi maslahi ya kimaada na mapato ya kijamii.

Na inaonekana kwamba yale ambayo yanalikabili jukumu hili miongoni mwa ugumu, na vikwazo ambavyo vinaweza kumzuia mwanachuoni kusimama, ndio ambayo yamesababisha ukali wa onyo la Mwenyezi Mungu, kemeo lake kali na kuwatishia wenye kutumbukia ndani ya mtego huo, anasema (swt):

هَلۡ أَتَىٰكَ حَدِيثُ مُوسَىٰٓ ﴿١٥﴾ إِذۡ نَادَىٰهُ رَبُّهُۥ بِٱلۡوَادِ ٱلۡمُقَدَّسِ طُوًى ﴿١٦﴾ ٱذۡهَبۡ إِلَىٰ
فِرۡعَوۡنَ إِنَّهُۥ طَغَىٰ ﴿١٧﴾

**"Hakika wale wafichao aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu katika Kitabu na wakanunua kwacho thamani ndogo, hao hawali matumboni mwao isipokuwa Moto: wala Mwenyezi Mungu hatawasemesha Siku ya Kiyama, wala hatawatakasa; na wao wana adhabu chungu."**
**(Surat al-Baqarah:174)**.

**Na anasema (swt):**

وَجَٰوَزۡنَا بِبَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ ٱلۡبَحۡرَ فَأَتَوۡاْ عَلَىٰ قَوۡمٖ يَعۡكُفُونَ عَلَىٰٓ أَصۡنَامٖ لَّهُمۡۚ قَالُواْ يَٰمُوسَى
ٱجۡعَل لَّنَآ إِلَٰهٗا كَمَا لَهُمۡ ءَالِهَةٞۚ قَالَ إِنَّكُمۡ قَوۡمٞ تَجۡهَلُونَ ١٣٨

**"Hakika wale wanaoficha tuliyoyateremsha, katika ubainifu na uwongofu, baada ya Sisi kuyabainisha kwa watu Kitabuni, hao anawalaani Mwenyezi Mungu, na wanawalaani wanaolaani."** **(Surat al-Baqarah: 159)**.

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwamba amesema: "Mtu yeyote aliyepewa elimu na Mwenyezi Mungu akaificha naye anajua, atakutana na Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama hali amepigwa kwa vijinga vya moto."[31] Na kutoka kwake (s.a.w.w.): "Bidaa ikidhihiri katika ummah wangu basi mwanachuoni adhihirishe elimu yake, kwani asiyefanya hivyo ni juu yake laana ya Mwenyezi Mungu."[32]

Hakika kunyamaza kwa maulamaa na kukataa kubainisha dhana sahihi na kunyamazia makosa yaliyoenea katika fikra na vitendo vya watu, kufanya hivyokunaimarisha hali mbaya ambayo ummah unaishi nayo, kunawatia watu katika ujahili na upotovu na kunaupa Uislamu sura mbaya mbele ya mtazamo wa jamii ya ndani na ya nje. Na hili ndilo lililozalisha uchafuzi na upakaji matope sura ya Uislamu ulimwenguni, na hatimaye baadhi ya jamii na watu katika ummah wakaikasirikia dini na kuichukia.

**Pili:** Kufahamu mazingira ya msukumo wa kijamii ulioenea katika sekta mbalimbali za maisha ya watu, kunapasa kuwahamasisha warekebishaji kusimama thabiti na kuwa na msimamo, kwani ka-

---

31 *Biharul-Anuwaar*, Jz. 2, uk. 68
32 *Wasailus-Shi'ah*, Jz. 16, uk. 269 Hadith namba 21 538

tika kila upande kuna msuguano wa nguvu na matakwa, lakini yule mwenye kukimbia mapambano au anayefanya haraka kukimbia na kujitoa, hakika yeye ataupa upande mwingine fursa ya kushinda na kusonga mbele kwa urahisi na wepesi.

Hakika nguvu zinazotawala katika jamii za watu, zinanufaika sana na kitendo cha nguvu za urekebishaji na ujadidishaji kukimbia medani, na kutokana na baadhi ya pande zake kufanya haraka kujitoa katika mapambano. Na hakika tunaweza kusema kwa kujiamini kwamba: Hakika wabeba fikra za kurekebisha si wachache ndani ya jamii ya maulamaa na walinganiaji, lakini hali ya kuficha na kutodhihirisha rai na fikra haiwawezeshi kutambuana wao kwa wao, na hivyo kila muumini mwenye kuhisi mabadiliko na marekebisho hujiona kana kwamba ni yeye pekee ndiye anayelengwa na nguvu zingine pinzani.

Kama ambavyo hofu ya kuziogopa nguvu zinazotawala inazuia wengi miongoni mwa warekebishaji kushikamana na kushirikiana na wenzao, na pindi mishale ya kujeruhi, kukosoana kutuhumu inapoelekezwa kwa mmoja wao hakika wengine miongoni mwa wanaobeba fikra na maelekezo yale yale hukimbilia kunyamaza na kujiweka kando mbali kabisa, na hudhihirisha kuwa hawana uhusiano wowote na mrekebishaji anayelengwa, hiyo ni ili wasipatwe na chochote katika mishale ya vita au cheche za moto wa wapinzani.

Hakika msuguano wa kifikra na ikhitilafu za rai ni hali ya kiafya, na sio kosa au dhambi inayoogopwa na inayoepukwa kama wanavyofikiri baadhi, na athari mbaya ambazo zinaweza kupatikana katika vita vya mapambano ya kifikra na kutofautiana rai ni matokeo ya nyendo za kimakosa katika kuamiliana na rai nyingine, inatokana na roho ya ubinafsi na ukandamizaji. Na kwa wanaojishughulisha na elimu na fikra washugulike na suala la kuimarisha uhuru wa kufanya utafiti wa kiel-

imu na kutoa rai, na hilo halitotimia isipokuwa kwa kuifanyia kazi haki hii na kuitetea.

**Tatu:** Kuna mabadiliko ya wazi katika kiwango cha utamaduni na uelewa wa watu, hakika duara la kujifunza limepanuka na vyombo vya maarifa vimeshaenea, na akili za watu zimefunguka, na sasa wanakabiliwa na changamoto za utandawazi wa ulimwengu, na baadhi ya fikra na vitendo vilivyoenea vinatengeneza kizingiti na kikwazo mbele ya mwenendo wa harakati zao licha ya kuwepo mabadiliko ya maisha, jambo ambalo linapelekea suala la kujadidisha na kurekebisha kuwa hitajio la lazima ambalo umuhimu wake sehemu kubwa ya watu wa ummah wanaujua. Na haya ni mambo ambayo inapasa wayafahamu warekebishaji, na wajue kuwa kusonga mbele kiwango cha maarifa katika jamii na kukua kwa jamii kunaleta haja ya kufanya mabadiliko na maboresho katika sekta ya kidini.

Lakini mabadiliko na uboreshaji wowote hukutana na baadhi ya yale ambayo watu wameyazoea na wamerithishana miongoni mwa fikra na vitendo, hivyo inahitaji kiasi fulani cha maandalizi na kujitolea muhanga na kutoa thamani na kiwango fulani cha uthabiti na uvumilivu, ikiwa ni pamoja na kushikamana na hekima na kutumia mbinu sahihi katika ufumbuzi na uwasilishaji.

Imebaki kuashiria kwamba yale tunayozungumzia miongoni mwa mabadiliko na marekebisho yanahusu upande wa yale yanayohitaji na kukubali mabadiliko na sehemu za utafiti na mjadala katika maarifa ya dini, na upande wa mila na vitendo, kadhalika upande wa njia na mbinu. Ama yale yaliyo thabiti katika dini na ambayo ummah umekongamana kwayo au jamii, hayo ni mahala pa hatari, mafunzo ya dini hayaruhusu kuyavuka.

# HOTUBA YA KIDINI NA VIPENGELE VYA UFANISI[33]

Hakika sisi tunajua upeo wa sababu na malengo katika kumwathiri binadamu na harakati zake, katika kila kitendo anachokitekeleza, sawa iwe ni katika kiwango cha aina ya kazi au katika namna ambayo atafanikisha kazi husika, au katika mwelekeo wa kazi na hatima yake, kila sababu na malengo yanapokuwa na ikhilasi na ukweli na mazuri, basi athari ya kazi inakuwa ni kubwa zaidi na hadhi yake ni kufaulu na kukubalika, kinyume na kazi ambayo inafanikishwa katika msingi wa kimaada na maslahi ya pembeni, kwa sababu kazi kama hii itakabiliwa na upungufu na kasoro, na ni kituo cha shubhati na dosari.

Ukweli huu unadhihirika na unakuwa wazi na kupata uhalisia zaidi katika vitendo vyenye muundo wa kidini, na katika msingi huu imekuwa ni lazima kwa watendaji katika medani hii kudhihirisha uwezo mkubwa wa kujitolea nakuwa na ikhilasi kwa Mwenyezi Mungu ili vitendo vyao vikubaliwe na kuridhiwa na Mwenyezi Mungu (swt), na kisha baraka za Mwenyezi Mungu zitakuwa ni sababu ya msingi katika kufanikisha kazi na kufikia lengo lake analotarajia.

**Sababu za khatibu na malengo yake:**

Hotuba ya kidini ni kitendo cha kiibada hivyo ni lazima mwandamu kwa msingi na sababu sahihi na malengo sahihi, yeye anaweza kukusudia katika hotuba yake kupata manufaa ya kimaada na anaweza kwenda mbio kuchuma umashuhuri na heshima kupitia hotuba hiyo, au anaweza kuiwasilisha kwa ajili ya kupata majivuno na sifa kutoka kwa wasikilizaji wake, lakini malengo haya sio anayoyakusu-

[33] Ni hotuba aliyoitoa Sheikh Hasan Saffar katika mkutano wa tabligh wa kidini katika Seminari ya Masomo ya Kidini ya Sayyidati Zainab huko Damascus 8/5 /1424 Hijiria sawa na 8/7/2003.

dia mwanadamu mwenye kushikamana na dini, mkweli na muumini aliye mwema, bali muumini mwenye dini yeye hukusudia yaliyo matukufu zaidi kati ya malengo na madhumuni yanayomsukuma kutoa hotuba, na yaliyo muhimu zaidi ni:

Kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani kulinganania kwa Mwenyezi Mungu ni wajibu wa kiungu uliotegemezwa kwa kila mwanadamu mwislamu muumini, amesema (swt):

ٱدْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلْحِكْمَةِ وَٱلْمَوْعِظَةِ ٱلْحَسَنَةِ ۖ وَجَٰدِلْهُم بِٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ ۚ
إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِۦ ۖ وَهُوَ أَعْلَمُ بِٱلْمُهْتَدِينَ ﴿١٢٥﴾

**"Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako ndiye anayemjua zaidi aliyepotea njia yake na Yeye ndiye anayewajua zaidi walioongoka." (Surat Nahli: 125)**.

**Na amesema tena:**

وَلْتَكُن مِّنكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى ٱلْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ ۚ
وَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾

**"Na liwepo miongoni mwenu kundi lenye kulingania kwenye kheri, na kuamrisha mema na kukataza maovu. Na hao ndio wenye kufaulu." (Suarat Aali Imraan: 104)**.

Aya hizi mbili zinawakilisha mifano miwili mikubwa kwenu kati ya aya ambazo zinasisitiza maana hii na zinazofuatia katika mtiririko huu, mwanadamu muumini ni mwenye jukumu na wajibu mbele ya Mwenyezi Mungu kwa yale anayoyabeba miongoni mwa elimu na maarifa ya kidini, naye ni mwenye kukalifishwa wajibu wa kunukuu

maarifa hayo ya kidini kwa wengine na kuyaweka mbele ya watu ili kumwangazia yule ambaye hajui na kumkumbusha yule anayejua. Sio lazima yule anayefikishiwa awe hajui tunayoyasema, bali mwanadamu Mwislamu ameamrishwa kukumbusha katika kauli yake (swt):

وَذَكِّرْ فَإِنَّ ٱلذِّكْرَىٰ تَنفَعُ ٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٥﴾

**"Na kumbusha, kwani ukumbusho huwafaa waumini."**
**(Surat Dhariyaat: 55)**.

Na vilevile kufikisha dini kunaingia chini ya anwani ya kuusiana katika haki na kuusiana katika subira, amri iliyo katika kauli yake (swt):

إِلَّا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ وَتَوَاصَوْا۟ بِٱلْحَقِّ وَتَوَاصَوْا۟ بِٱلصَّبْرِ ﴿٣﴾

**"Ila wale walioamini, na wakatenda mema, Na wakausiana haki, na wakausiana kusubiri." (Surat al-Asri: 3)**.

Na hivyo ndivyo inavyoanza kazi ya tabligh kama sehemu ya kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kwa msingi wa yaliyotangulia tunafahamu yale waliyoyasema maulamaa wenye ikhilasi kuwa kabla khatibu hajapanda mimbari kwa ajili ya kutoa hotuba anapaswa kuleta nia ya kujikurubisha ili afahamu kwamba yeye anatekeleza kazi ya ibada ambayo anapata ukamilifu wake wakati anapo iambatanisha na nia yakujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu.

Lakini yanayosikitisha ni kutoweka ukweli huu katika akili za baadhi ya makhatibu na wahubiri, na kutawala mazingira ya kimaada na mawazo ya kimaslahi kwao, hadi kutoa hotuba na kubalighi imekuwa ni kazi na ajira kwao, na ni sababu kati ya sababu za kujipatia riziki na chumo na si vinginevyo, hivyo unamkuta yeye

anafanya kazi hii kwa ajili ya kupata malipo au kwa kuwa anapatiwa mshahara kila mwezi na mengine yasiyokuwa hayo miongoni mwa manufaa mengine ya kidunia.

Na hapa inapasa kuashiria kwamba mwanadamu kutafuta riziki yake na kujituma katika kujipatia chakula chake na mahitaji yake ni jambo la kimaumbile na la kawaida, si aibu na wala si haramu, zaidi ya hapo ni dharura ya kimaisha na ni matokeo ya uvumbuzi wa kazi. Na hivyo ni lazima taasisi za kidini zibebe majukumu yake kwa mubalighina na kwa makhatibu katika kuwapatia yanayopasa katika mahitaji yao na ambayo yatawahakikishia maisha mazuri. Na sote tunajua kwamba mubalighina na makhataibu katika madhehebu mengine wanashughulikiwa na wizara na taasisi ambazo zinabeba jukumu la kushughulikia maisha yao na masurufu yao, kama vile Wizara ya Wakfu na Uelimishaji na nyinginezo, wakati ambapo wafuasi wa Ahlulbait wameamua kutofungamana isipokuwa na Marjaa wa kidini kwa kujali kwao uhuru na kwa kuogopa kuamrishwa kutekeleza baadhi ya misimamo kama badala stahiki ya matumizi na mahitaji wanayopewa. Njia hii ya uhuru ndio inayoiwajibisha taasisi ya Marjaa kusimamia na kukidhi mahitaji ya makhatibu na mubalighina ili wajishughulishe na wajibu wa kutekeleza jukumu lao la kufanya tablighi na kuelimisha, na kujaza nafasi ya kimaanawi ambayo inaweza kusababisha wao kuacha tablighi kutokana na matatizo ya kimaisha na kutafuta mahitaji ya dharura.

Mubalighi na khatibu ni mtu kama wengine huelemewa na mahitaji ya kimaisha na kutafuta maisha ya wanaomtegemea. Hivyo haachi kushambuli wa na kuwindwa na ufakiri na ukosefu, na viwili hivyo ni kati ya sababu muhimu sana ambazo zinaathiri katika msukumowa khatibu na nia ya mubalighi, na hivyo vinamfanya awe na raghaba ya kupata mada na ziada katika maisha. Na wala haipasi kuacha kuwaelekea makhatibu na mubalighina na kuwanong'oneza

katika masikio yao kwa mapenzi yote na heshima yote kwamba wasitumie mwanya wa baadhi ya mapungufu kama kisingizio, wasisahau kwamba wao ni watu waumini wanabeba jukumu la dini yao, matumaini ya ujumbe wao na wanatekeleza ibada tukufu, hivyo haipasi wao kupuuza na kupoteza ibada zao kwa ajili ya kuelekea katika maada na dunia na kuelemea kwenye maslahi. Na tunapenda kukumbusha katika nafasi hii Hadithi iliyopokewa kutoka kwa Imam Abi Abdillahi as-Sadiq (as), amesema: "Mashia wetu wako makundi matatu:Kundi linalotupamba, na sisi ni pambo kwa anayetupamba. Kundi linalokula kupitia kwetu. Na kundi linalotokana na sisi na lipo kwa ajili yetu."[34] Na tunazikinga nafsi zenu na nafsi zetu kutokuwa katika kundi la pili ambalo wanakula kupitia Ahlulbait (as). Kama pia ilivyopokewa katika Hadithi nyingine kutoka kwake (as): "Anayekula kupitia kwetu haachi kuwa fakiri."[35]

Ni juu ya mubalighi kuhudhurisha ukweli huu katika akili yake wakati anapopanda mimbari na kuhutubia na kuwapa watu waadhi na kuwaelimisha, na hiyo ni kwa kuwa na yakini kuwa anatekeleza wajibu kwa msingi wa kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu na wajibu wake wa kulingania na kuelimisha, na hii ndio hatua ya kwanza ambayo inatengeneza kanuni ya msingi katika kazi ya khatibu.

**Kuelewa changamoto:**

Ama hatua ya pili inajikita katika kuelewa kwetu hatari za changamoto zijazo, na changamoto hatari zinazotukabili leo hii ziko bayana kwa kila mtu, changamoto ambazo zimetuweka katika shinikizo kubwa huku duara la changamoto hizi likiendelea kupanuka na kuenea ili lizingire uwepo wetu, utu wetu, utamaduni wetu, misingi yetu ya kidini na tabia. Na hakuna shaka kwamba ndugu zangu maustaadhi na mubalighina kiasi fulani wanafahamu changamoto hii yenye kue-

---

[34] *Al-Khiswali* cha Sheikh Suduuq uk. 103

[35] *Mishikaatul-Anuwaar* cha Twabarsiy uk. 150

nea na hatari inayozunguka pembezoni mwake miongoni mwa hatari zinazolenga undani wetu tukiachilia mbali nje yetu, na changamoto hizi zimefikia kilele chake katika hali yetu ya sasa.

Marekani leo hii haiwakilishi tena nguvu ya uvamizi wa kijeshi tu, na wala silaha zake haziishii tu kwenye bunduki, mabomu na jeshi lililoandaliwa kwa ajili ya vita, na wala shabaha yake haikomei katika fukwe zetu na ardhi zetu tu, ndiyo yote hayo Marekani inayalenga, lakini ina tamaa kubwa zaidi kuliko hayo na inataka makubwa na ya kina zaidi na ya hatari zaidi, pale ilipoweka utamaduni wa mataifa mbalimbali, maadili yake na misingi yake ya kimaanawi katika kipaumbele chake na malengo yake, kwa kufanya jaribio lake la kusagasaga misingi yote ya mataifa mengine na kuyeyusha tamaduni zao zote ndani ya sanduku la ustaarabu na utamaduni wa Kimagharibi.

Katika vita vyake, Marekani imeweza kupenya hadi kwenye vyumba vyetu vya kulala na sehemu za kulala watoto wetu ili kuhubiri utamaduni wake na miundo ya nyendo zake, hivyo yenyewe ndiye adui anayetutishia ndani ya nyumba zetu, kwa kila anachomiliki-miongoni mwa mbinu na kwa kila anachoandaa miongoni mwa nyenzo zenye kuathiri.

Na wajibu wetu ni kuzatiti nguvu zetu na kuimarisha azima yetu na kutumia akili zetu na kuunganisha nguvu zetu ili tusimame dhidi ya hatari inayotuvamia na adui mvamizi, tuwalinde watoto wetu na tuihami jamii yetu, na tusimame dhidi ya wimbi hili ambalo linalenga kufuta heshima ya ummah huu, na linajaribu kufuta maadili ya kiroho na ya kimaanawi ya dini yetu ya Kiislamu tukufu na ya dini nyinginezo na ya itikadi nyingine zilizopo katika jamii za kibinadamu, yote hayo yameambatana na shinikizo la kuyalazimisha mataifa yote yamwabudu mungu mmoja tu naye ni maada, maada tu. Haya ndio malengo yao yaliyotangazwa, na ni wajibu wetu kukabiliana na changamoto pamoja na kujua kwetu tofauti kubwa na pengo

kubwa lililopo baina yetu na baina yao katika upande wa uwezo wa kimaada, mbinu za kisasa na nyenzo za kisasa.

Hakuna kilichobaki kwetu isipokuwa ni kuwekeza katika aina ya kazi itakayotuwezesha kutetea, kuupa nguvu uwepo wetu na kulinda mazingira yetu. Na kati ya vitu muhimu vya msingi katika nguvu itakayotuwezesha kufanya kazi na athari yake kuenea ni nguvu hiyo kuwa na ikhilasi, ukweli na ufanisi, ili tuamshe yaliyofichikana ndani ya nafsi zetu, ili kwa nguvu hiyo tupambane na nguvu hii kubwa ya kiulimwengu katika nyanja ya kimaada, kiteknolojia na katika maendeleo ya vyombo vya kisasa, na haya ndio yanayohusu nukta ya kwanza inayowakilishwa na malengo ya khatibu na shabaha yake.

**Ufanisi wa maelekezo ya kidini:**

Hakika kipimo kinachohukumu harakati za ulimwengu katika zama za leo hii si kusema tunafanyakazi au hatufanyi kazi, dharura ya kufanya kazi ni jambo ambalo halihitaji tena mjadala, na mazingira ya maisha yanamsukuma mwanadamu na yanamlazimisha kufanya kazi, na hiyo ni kwa ajili ya kupata kiwango cha chini kabisa kati ya mahitaji ya kimaisha na dharura zake, sawa iwe katika kiwango cha mtu binafsi au jamii.

Lakini kipimo cha kila siku ambacho kwacho kazi zinapimwa katika ulimwengu wa sasa ni zile sifa zinazoizunguka kazi miongoni mwa aina za uzuri na ufanisi, na sifa hii ndio inayoshindaniwa na dola mbalimbali, inashindaniwa na mashirika na viwanda, na kila mmoja anazalisha na wote wanazalisha, na hili ni muhimu, lakini muhimu zaidi kuliko hilo ni aina ya ubora anao ufanikisha mzalishaji katika bidhaa yake, mazingatio ni ubora na sio idadi, na kwa ajili hiyo ulimwengu umeweka kipimo cha ubora wa bidhaa zinazozalishwa, hivyo kadhia si uzalishaji tu bali ni uzalishaji upi ndio bora zaidi, na ushindani uliopo baina ya Japani na Marekani hauko

katika idadi ya uzalishaji bali ushindani ni katika kiwango cha ubora na aina ya duara la ushindani huu.

Na katika wakati wetu tulionao medani ya ushindani imepanuka na imevuka sekta ya utengenezaji na ubora wake, tunapoangalia maonyesho ya matangazo na utamaduni katika ulimwengu wa leo tunagundua kwa urahisi ushindani huu mkubwa na juhudi endelevu zinazolenga kutoa aina bora zaidi ya matangazo, fikra na utamaduni katika kuathiri na kuvutia. Chanel hizi, vituo vya matangazo mbalimbali na tovuti zisizo na idadi, si kingine isipokuwa ni sura ya ushindani huu mkali, na kama mnavyojua hakika sisi Waislamu tunaishi ndani ya medani hii, bali sisi ni kati ya walengwa wa mwanzo wa harakati hizi za kimatangazo, kiutamaduni na kifikra zenye kukusudiwa.

Watoto wetu na vijana wetu wao ndio lengo la msingi na shabaha kuu ya mashambulizi haya ya kiutamaduni ya nguvu za uvamizi, na imekuwa ni kawaida kizazi hiki kupata fikra zao na nyendo zao kutoka kwenye chanel, tovuti na vyombo vingine kati ya vyombo vya matangazo na utamaduni, kama wanavyopata kutoka kwenye misikiti, Husainiya na klabu za kiutamaduni na kifikra. Hivyo sisi tunaishi katika hali ya ushindani tutake au tusitake, na hali hii inatulazimisha kutumia juhudi za ziada ili kunyanyua kiwango cha maelekezo yetu na kuendeleza vyombo vyetu na mbinu zetu ili tuwe ni wenye kuathiri katika mapambano haya yenye kuenea, ambayo medani yake kubwa na muhimu zaidi ni utamaduni na fikra.

Uzembe au dosari yoyote katika upande huu, ni hatua ya kurejea nyuma inayotoa mwanya kwa washindani wetu kuendelea mbele na kutupita na hatimaye kuharibu idadi kubwa ya watoto wetu na vijana wetu. Ni wajibu wetu tuwe katika kiwango cha changamoto hii, kadhia sasa sio tu mimi napanda mimbari na kutoa hotuba, bali kadhia imekuwa ni aina ya hotuba, ubora wake na sifa zinazoizunguka

miongoni mwa vipengele vya nguvu na vyenye kuathiri, hili ndio jambo muhimu zaidi katika harakati hizi.

Na kwa msingi huu sisi tunalazimika kufikiria na kutoa juhudi za ziada katika upande wa kunyanyua kiwango cha hotuba zetu na matangazo yetu kwa aina zake zote na namna zake zote. Na wakati tunaporejea katika utamaduni wetu na hazina yetu ya Kiislamu hakika tunakutana na aina mbili za mkazo na mafunzo, mojawapo inahimiza juu ya kazi bila sharti lolote, kama ilivyo katika kauli yake (swt):

وَقُلِ ٱعْمَلُوا۟ فَسَيَرَى ٱللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُۥ وَٱلْمُؤْمِنُونَ ۖ وَسَتُرَدُّونَ إِلَىٰ عَٰلِمِ ٱلْغَيْبِ وَٱلشَّهَٰدَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾

**"Na sema: Tendeni vitendo Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na waumini wataviona vitendo vyenu na mtarudishwa kwa Mjuzi wa ghaibu na dhahiri, naye awaambie mliyokuwa mkiyatenda." (Surat Tawba: 105)**.

Wakati ambapo nususi zingine na maneno mengine yamelenga kuelekeza upande wa ufanisi wa kazi na kunyanyua kiwango cha ubora wake. Anasema (swt) katika yanayoambatana namazungumzo ya kuzungumza na watu:

وَقُل لِّعِبَادِى يَقُولُوا۟ ٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ ۚ ﴿٥٣﴾

**"Waambie waja Wangu waseme maneno mazuri." (SuratIsraai: 53).**

Aya hizi ziko wazi katika kutaka kunyanyua kiwango cha hotuba katika daraja bora zaidi na aina bora zaidi, suala sio tu tuseme maneno, kadhia sio tu tujaze wakati fulani kwa hotuba na mazungumzo, bali kinachotakiwa ni kuhakikisha hotuba zinanyanyuka hadi katika kiwango bora zaidi na aina bora zaidi kadiri inavyowezekana.

Na vilevile tunapoingia katika mapambano na mjadala pamoja na makundi mengine ya kifikra na hotuba mbalimbali shindani, ni lazima tuendeshe medani hii kwa ubora, kwa maneno bora, kwa mbinu za ufanisi zaidi na kwa njia bora zaidi. Na kwaajili hiyo anasema (swt):

۞ وَلَا تُجَٰدِلُوٓاْ أَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ إِلَّا بِٱلَّتِي هِيَ أَحۡسَنُ ﴿٤٦﴾

**"Wala usijadiliane na watu wa Kitabu isipokuwa kwa njia iliyo nzuri kabisa." (al-Ankabut: 46).**

Ni lazima kupata ubora wa kuwashinda wengine kwa ajili ya kushinda mchezo, wakati mapambano yanapopamba moto na ushindani unapokuwa mkali zaidi. Na mambo hayaishii katika sekta ya fikra, medani ya matangazo na klabu za mijadala, bali yanavuka hadi kwenye aina ya mapambano ya kivitendo na namna ya kuamiliana pamoja na wengine, ambapo Qur'ani inatuelekeza tutumie mbinu bora zaidi, katika kauli yake (swt):

ٱدۡفَعۡ بِٱلَّتِي هِيَ أَحۡسَنُ ٱلسَّيِّئَةَۚ نَحۡنُ أَعۡلَمُ بِمَا يَصِفُونَ ﴿٩٦﴾

**"Kinga maovu kwa yaliyo mema zaidi. Sisi tunayajua wanayoyasifia." (al-Muuminina: 96).**

Na vilevile enyi ndugu maulamaa na mubalighina, hakika nususi za Kiislamu zinatilia mkazo ubora wa kazi na kuilinda kama vile zinavyotilia mkazo asili ya kazi na ufanisi wake, na nyote - walhamdulillahi – mko katika safu za mazingira ya nususi hizi na ni kati ya wenye elimu na wenye ufahamu huo.

Na katika yanayonukuliwakutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kama darasa kubwa katika upande huu, ni kwamba wakati alipomzika mtoto wake Ibrahim na akamuweka

katika mwanandani pamoja na kundi la Masahaba, alijali sana ufanisi wa kazi hii na ubora wake, liwekwe kila tofali na jiwe katika sehemu yake inayofaa na izibwe mianya baina ya mawe. Nabii alitaka kazi yake hii izushe maswali katika nafsi za Masahaba wake na wenye kuitenda, je kaburi linahitajia ufanisi na ubora wote huu? Akajibu swali hilo kwa hadithi mashuhuri: "Hakika Mwenyezi Mungu anapenda mja anapofanya kazi basi aifanye kwa ufanisi."[36] Na hata kuchinja, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) anatuamuru tuchinje kwa njia nzuri, na hiyo ni katika kauli yake (s.a.w.w.): "Mnapochinja basi chinjeni vizuri."[37]

Na tunahitimisha katika muhtasari huu kwamba, sio sahihi kuhutubia vyovyote iwavyo bila sisi wenyewe kuridhika (na ubora wa hotuba), isipokuwa ni lazima hotuba zetu ziwe na ufanisi na maandalizi, na tutafakari katika vipengele vyenyenguvu na kuondosha kila kipengele chenye udhaifu, na jambo hilo ni kati ya mambo yenye kuibua vipaji na kunyanyua kiwango cha mwanachuoni, khatibu na mubalighi. Zaidi ya hapo jambo hilo linamfanya awe karibu na malengo anayoyatarajia wakati wa kuandaa hotuba na kuiwasilisha kwake, kwani msikilizaji hulinganisha baina ya anayoyapokea katika hotuba na yale anayoyasikia katika maneno hata kama hakukusudia kufanya hivyo.

**Mambo yanayoleta ufanisi:**

Baada ya kujua umuhimu wa hotuba na jinsi inavyoakisi kwa mpokeaji na khatibu, tunaulizia mambo muhimu zaidi na njia bora zaidi zenye mwingiliano na kazi ya maandalizi na kunyanyua kiwango cha ubora wa hotuba, na tunaweza kujibu kutokana na uzoefu

[36] *Wasailus-Shi'ah* Juz. 3 uk. 230.

[37] Muslim bin al-Hajaaji Ani Saburiy katika *Sahihi Muslim*uk. 1080 chapa ya kwanza 1941 Hijiria ya Riyaadh, Daru al-Mughiniy Hadithi namba 19 55.

na angalizo juu ya swali lililopo, kwamba hakika hayo yanafupishwa katika mambo matatu:

**Jambo la kwanza:-**
**Upeo mpana wa khatibu kielimu na kimaarifa:**

Kila elimu ya khatibu inapokuwa ni pana na maarifa yake ni ya kina ndivyo uwezo wake katika ufanisi wa hotuba unavyokuwa mkubwa, na inatusikitisha kusema kwamba baadhi yetu sisi wanafunzi wa elimu ya dini hatujitaabishi katika kutafuta maarifa na ujuzi wa kielimu, na tumeshasikiliza maneno ya Amirul-Muuminina (as) ambaye anazingatia kulingania kwa ulimi ni sehemu ya jihadi, na hiyo ni kauli yake (as): "Mcheni Allah kwa kufanya jihadi kwa mali zenu, nafsi zenu na ndimi zenu."

Na asili ya jihadi ni kama wanavyosema watu wa lugha: Ama ni kutokana na juhudi, taabu na shida au ni kujituma, nako ni kutoa uwezo na nguvu. Na kwa ajili hiyo yeyote anayetaka kutoa hotuba ajue kwamba yeye anafanya kazi ya jihadi hivyo inamlazimu awena daraja la juu la maandalizi. Sio hekima mwanadamu kuiingiza nafsi yake katika uwanja wa vita kabla ya kufanya mazoezi ya fani za vita na kukamilisha mahitajio ya maandalizi. Na sisi tunaishi katika zama bora kiasi kwamba zinapatikana njia za maarifa na vyanzo vyaelimu, hivyo sisi tuko mbali na maulamaa wa zama zilizopita waliokuwa wanakosa zana ndogo kabisa na wanaishi katika nyakati zenye ugumu, hawamiliki tunayomiliki kati ya nyenzo za umeme na viyoyozi, na vitabu walivyokuwa navyo havikuwa katika kiwango hiki cha maandishi yaliyo bayana ambayo yanampa raha mwenye kuvisoma. Lakini pamoja na hali hiyo, sira yao inatusimulia juhudi kubwa waliyokuwa wanaitoa na muda mrefu ambao walikesha, walitumia wakati wao mtukufu katika kutafuta elimu na kuchuma maarifa, na mwanadamu muumini anatakiwa kutoa juhudi zote za ziada katika viwango vyote.

Tunapotazama katika upande wa kiibada mafunzo hayasimami katika wajibu maalumu wa Swala tu kwa mfano, bali yanamhamasisha muumini na kumhimiza aongeze ibada zake ili Swala yake iwe ni zaidi ya faradhi iliyo juu yake katika kiwango cha wajibu wa lazima. Muumini wa kweli ni mwenye kuswali rakaa 51 kwa usiku na mchana. Hali ni hiyo hiyo kulingana na Swala yenyewe, kwani ni chache na fupi sana kama tutakuwa tumechagua tu amali zake na tukaishia katika wajibu tu, bali sisi tunaitekeleza pamoja na mustahabu zilizopokelewa humo.

Juhudi za nyongeza ni jambo linalotakiwa katika viwango vyote, kwa ajili ya kutafuta ukamilifu na ufanisi, na mwenye kutafuta elimu katika Hawza zetu hapaswi kutosheka tu na silabasi ya elimu iliyopangwa katika madrasa yake, kwani hicho ni kiasi cha chini na daraja inayofaa, lakini medani inabaki wazi kwa ajili ya ushindani usio na mpaka katika kutafuta elimu, kuchuma maarifa na kupanua utamaduni na uwelewa, na hili ndio jambo la kwanza kati ya mambo yenye kuleta ufanisi wa hotuba.

**Jambo la pili:**
**Kujua sifa za wenye kuhutubiwa:**

Na kati ya mambo muhimu yenye kuleta ufanisi katika hotuba ni khatibu kuwa ni mwelewa, mwenye kujua mazingira ya kijamii ya wenye kuhutubiwa. Kila jamii ina sifa zake mahususi na matatizo yake na kiwango chake, na kila mazingira yanatofautiana na mengine, na kila sehemu ina misemo yake. Maarifa humsaidia khatibu kuandaa hotuba yake itakayoafikina na mazingira ya wenye kuhutubiwa na kumwepusha kutumbukia katika makosa na pia humkinga na dosari.

Imepokewa kutoka kwa Imamu al-Baqir (as) kuwa alisema: “Mtendaji mwenye kujua zama zake.” Na katika nasi ny-

ingine: “Mwenye kuwajua watu wa zama zake, hatopatwa na mkanganyiko.”[38] Na mfano bora zaidi wa kujua nyakati za jamii na kutofautiana kwa mazingira yake ni tunayoyaona katika sira ya Manabii na visa vyao na njia za kazi zao. Kila Nabii anatilia mkazo juu ya jambo maalumu na anatilia umuhimu lengo maalumu, na hilo sijambo linalotokea tu, bali chanzo chake ni kubaini uhalisia wa jamii husika na kujua hali yake na kujaribu kuirekebisha.

Nabii waMwenyezi Mungu Ibrahim (as) alitilia mkazo juu ya tawhidi na kupuuza ibada ya masanamu, amesema (swt):

وَٱتۡلُ عَلَيۡهِمۡ نَبَأَ إِبۡرَٰهِيمَ ﴿٦٩﴾ إِذۡ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوۡمِهِۦ مَا تَعۡبُدُونَ ﴿٧٠﴾ قَالُواْ نَعۡبُدُ
أَصۡنَامٗا فَنَظَلُّ لَهَا عَٰكِفِينَ ﴿٧١﴾ قَالَ هَلۡ يَسۡمَعُونَكُمۡ إِذۡ تَدۡعُونَ ﴿٧٢﴾ أَوۡ
يَنفَعُونَكُمۡ أَوۡ يَضُرُّونَ ﴿٧٣﴾ قَالُواْ بَلۡ وَجَدۡنَآ ءَابَآءَنَا كَذَٰلِكَ يَفۡعَلُونَ ﴿٧٤﴾ قَالَ
أَفَرَءَيۡتُم مَّا كُنتُمۡ تَعۡبُدُونَ ﴿٧٥﴾ أَنتُمۡ وَءَابَآؤُكُمُ ٱلۡأَقۡدَمُونَ ﴿٧٦﴾ فَإِنَّهُمۡ عَدُوّٞ لِّيٓ
إِلَّا رَبَّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ﴿٧٧﴾ ٱلَّذِى خَلَقَنِى فَهُوَ يَهۡدِينِ ﴿٧٨﴾ وَٱلَّذِى هُوَ يُطۡعِمُنِى
وَيَسۡقِينِ ﴿٧٩﴾ وَإِذَا مَرِضۡتُ فَهُوَ يَشۡفِينِ ﴿٨٠﴾ وَٱلَّذِى يُمِيتُنِى ثُمَّ يُحۡيِينِ ﴿٨١﴾
وَٱلَّذِىٓ أَطۡمَعُ أَن يَغۡفِرَ لِى خَطِيٓـَٔتِى يَوۡمَ ٱلدِّينِ ﴿٨٢﴾ رَبِّ هَبۡ لِى حُكۡمٗا
وَأَلۡحِقۡنِى بِٱلصَّٰلِحِينَ ﴿٨٣﴾ وَٱجۡعَل لِّى لِسَانَ صِدۡقٖ فِى ٱلۡأٓخِرِينَ ﴿٨٤﴾
وَٱجۡعَلۡنِى مِن وَرَثَةِ جَنَّةِ ٱلنَّعِيمِ ﴿٨٥﴾ وَٱغۡفِرۡ لِأَبِىٓ إِنَّهُۥ كَانَ مِنَ ٱلضَّآلِّينَ ﴿٨٦﴾ وَلَا
تُخۡزِنِى يَوۡمَ يُبۡعَثُونَ ﴿٨٧﴾ يَوۡمَ لَا يَنفَعُ مَالٞ وَلَا بَنُونَ ﴿٨٨﴾ إِلَّا مَنۡ أَتَى ٱللَّهَ بِقَلۡبٖ
سَلِيمٖ ﴿٨٩﴾

[38] Al-Kaafiy Juz. 1, uk. 26

**"Na wasomee habari za Ibrahim. Alipomwambia baba yake na kaumu yake: Mnaabudu nini? Wakasema: Tunaabudu masanamu nasi tutaendelea kuyanyenyekea. Akasema: Je yanawasikia mnapoyaita? Au yanawafaa au yanawadhuru? Wakasema: Bali tumewakuta mababa zetu wakifanya hivyo hivyo. Akasema: Je, mmewaona mnaowaabudu? Nyinyi na baba zenu wa zamani? Hakika hao ni maadui zangu isipokuwa Mola wa walimwengu wote. Ambaye ameniumba Naye ananiongoza. Na ambaye ananilisha na kuninywesha. Na ninapougua basi Yeye ananiponya. Na ambaye atanifisha kisha atanihuisha. Na ambaye Ndiye ninayemtumai kunighufuria makosa yangu siku ya malipo. Mola Wangu! Nitunukie hukumu na uniunganishe na wema. Na unijaalie kutajwa kwa wema na wengine. Na unijaalie katika warithi wa Bustani za neema. Na umghufirie baba yangu, kwani alikuwa miongoni mwa wapotevu. Wala usinihizi siku watakapofufuliwa. Siku ambayo haitafaa mali wala wana. Isipokuwa mwenye kuja kwa Mwenyezi Mungu na moyo uliosalimika." (Surat Shu'araa: 69- 89).**

Na Nabii Ibrahim (as) alitoa juhudi nyingi katika nyanja hii na jihadi yake ilikuwa katika medani hii.

Wakati ambapo juhudi za Musa (as) zilijikita katika jambo jingine, hatukuti katika kisa cha Musa(as) yale yaliyokuwa katika kisa cha Ibrahim(as), habari za masanamu na miungu ya uwongo, lakini mahala alipotia mkazo Musa(as) panaonekana katika kauli yake (swt):

ٱذۡهَبَآ إِلَىٰ فِرۡعَوۡنَ إِنَّهُۥ طَغَىٰ ﴿٤٣﴾

**"Nendeni kwa Firauni, hakika yeye amepituka mipaka."**
**(Surat Twaha: 43).**

Hapa suala linahusiana na kupiga vita ukandamizaji na uasi wa kisiasa, pamoja na kwamba sisi tunakuta baadhi ya ishara za kuwepo masanamu katika kauli yake (swt) kupitia ulimi wa watu wa Musa:

قَالُواْ يَـٰمُوسَى ٱجْعَل لَّنَآ إِلَـٰهًا كَمَا لَهُمْ ءَالِهَةٌ ۚ ﴿١٣٨﴾

**"Wakasema: Ewe Musa! Hebu nasi tufanyie waungu kama hawa walivyo na waungu."** **(Surat al-A'araaf: 138).**

Lakini jambo la msingi kwa Musa (a.s.) lilikuwa ni kujikita katika kupiga vita uasi na ukandamizaji.

Na Nabii wa Mwenyezi Mungu Lut (as) alikuwa na jukumu lingine alilopewa la kutibu ufisadi wa kitabia kama inavyosimulia Qur'aniTukufu katika kauli yake (swt):

وَلُوطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِۦٓ إِنَّكُمْ لَتَأْتُونَ ٱلْفَـٰحِشَةَ مَا سَبَقَكُم بِهَا مِنْ أَحَدٍ

مِّنَ ٱلْعَـٰلَمِينَ ﴿٢٨﴾

**"Na Lut alipowaambia watu wake: Hakika nyinyi mnafanya uchafu ambao hajawatangulia yeyote kwa hilo katika walimwengu."** **(Surat al-Ankabuti: 28).**

Na ujumbe wa Shuaib (as) ulikuwa katika kupiga vita ufisadi wa kiuchumi ulioenea katika jamii yake wakati huo, alikuwa anawahutubia watu wake:

فَأَوْفُواْ ٱلْكَيْلَ وَٱلْمِيزَانَ

وَلَا تَبْخَسُواْ ٱلنَّاسَ أَشْيَآءَهُمْ وَلَا تُفْسِدُواْ فِى ٱلْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَـٰحِهَا ۚ

ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٨٥﴾

**"Basi kamilisheni kipimo na mizani wala msiwapunje watu vitu vyao, wala msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kutengenea kwake. Hayo ndiyo bora kwenu ikiwa nyinyi mmeamini."** **(Surat al-A'araaf: 85).**

Na katika kutofautiana muundo wa hotuba ya Qur'ani baina ya aya za Makka na za Madina ni mfano wa wazi katika kuchunga nyakati na kubainisha kutofautiana kwa mazingira ya kijamii, aya zilizoshuka Madina zinatofautia na na zile zilizoshuka Makka, ambapo muundo wa kupiga mifano na jaribiola kutia mkazo, yote hayo yanaonyesha kipengele cha wakati na sehemu na mazingira kina mchango katika kupangilia aina ya hotuba na kuchagua mbinu za kuwasilishia.Wakati unapokuwa mubalighi Syria basi wewe upo katika mazingira tofauti na yale ya unapokuwa mubalighi Lebanon kwa mfano, au India au Pakistan, na hapa ndipo inapojitokeza thamani ya kupembuam azingira ya jamii ambayo humo mubalighi anafikisha ujumbe wake.

Na inafaa kuashiria kwamba mubalighi anaweza kushindwa kufanikisha jukumu hili peke yake, na hapa inakuja nafasi ya taasisi za tablighi katika kumsaidia kumuongezea ufafanuzi, taarifa na maalumati ambayo kwayo atapata msaada wa kutengeneza picha inayokaribiana na uhalisia wa jamii ambayo anafanyakazi humo.

**Jambo la tatu:**
**Maandalizi mazuri na kujiandaa kuhutubia:**

Uzoefu umetufundisha kwamba hotuba ambayo tunaiwasilisha baada ya kujiandaa na kujitayarisha vizuri kwa namna nzuri inakuwa ni hotuba inayofaa, na inakuwa na uwezo mkubwa wa kuathiri katika nafsi za wasikilizaji, wakati ambapo hotuba ya kushitukiza isiyo na maandalizi haileti matokeo hayo. Hakika mimi ninahisi kabla ya mwingine udhaifu wa hotuba hii na ufinyu wa kuathiri kwake, na hili ni jambo la kawaida. Na kwa sababu hiyo ni juu ya mwanadamu kujiandaa kwa kila mazungumzo vyovyote yatakavyokuwa muhimu, hata kama ni kikao binafsi, kupanga pa kuanzia na kupanga sehemu za kusimama na mbinu za mazungumzo. Ni miongoni mwa mambo

yanayosaidia kufanikisha kazi, na kila mwanadamu anayetaka akili yake iheshimiwe na neno lake lisikilizwe ni juu yake kutoghafilika na jambo hili.

Na kwa hiyo imepokewa kutoka kwa Amirul-Muuminina (as): "Ulimi wa mwenye akili uko nyuma ya moyo wake na moyo wa mpumbavu uko nyuma ya ulimi wake."[39]

Mwanadamu muumini inapaswa ajiandae vizuri na afikirie katika anayoyazungumza, na inanukuliwa katika sehemu hii kutoka kwa Sheikh al-Khatibu Muhammad Taqiy Falsafiy (r.m) naye ni kati ya makhatibu wakuu katika zama hizi: Kwamba hatoi hotuba wala muhadhara kabla ya kujiandaa kwa muda usiopungua saa nane, na vitabu vyake vimechapishwa na kutarjumiwa katika lugha ya Kiarabu na humo kuna faida nyingi za kielimu na kiutamaduni.

Vile vile Dr. Ahmad al-Waailiy(r.m) naye pia alikuwa anajitahidi sana kujiandaa na kujitayarisha jambo ambalo limenyanyua kiwango cha hotuba zake na mihadhara yake ambayo ni maarufu kwa uzuri na ufanisi. Hivyo hakuna nafasi ya kudharau na kuzembea katika suala la maandalizi ya kila kazi vyovyote itakavyokuwa umbo lake na vyovyote itakavyokuwa mazingira yake, sisi tunaishi zama ambazo zinapatikana zana zote zinazohitajika katika kujiandaa na katika kuleta ufanisi.

Rejea zimeenea na taabu ya kuzifikia ni ndogo sana ukiongezea na njia zote na sababu zote zinazosaidia, hivyo haibakii kwa mubalighi isipokuwa kuisumbua akili yake na kuishughulisha na kutafakari katika maudhui yake kisha kurejea kwenye rejea zinazohusiana nayo, ikiwa ni pamoja na kushauriana na mazingira ya kijamii yanayomzunguka ili kukamilisha sehemu za hotuba nzuri na kazi yenye ufanisi.

[39] *Wasailus-Shi'ah*, Juz. 1, uk. 281

Inawezekana kwa kila mmoja wenu anayekwenda kwenye tablighi katika moja ya miji kupanga ziara ya kukutana na shakhsiya muhimu katika mji ili ashauriane nao na kufaidika na rai zao, kwa sababu wao wanajua zaidi mambo ya mji wao.

Na hivi ndivyo yanavyojipanga mambo haya matatu: Kutafakari, kurejea vitabu vya rejea na kuwataka ushauri watu, katika kuandaa hotuba yenye ufanisi, na mazungumzo yanayojumuisha mengi kati ya vipengele vya kuathiri na uzuri, na yenye kuepukana na nukta nyingi za udhaifu na dosari.

# FASLU YA TATU

## UTEKELEZAJI WA KIJAMII, MTAZAMO NA UNYOOFU

**Mwanachuoni wa kidini baina ya unyenyekevu na kujikweza:**

Mwanachuoni wa kidini ni namna gani anaiangalia nafsi yake? Na ni namna gani anawaona wengine mbele yake? Hakika mtazamo wa mwanadamu kuhusu dhati yake hupanga mtazamo wake kwa wengine, na hutengeneza msingi na mazingira ya namna ya muamala wake na uhusiano wake na wengine.

Kutokana na umuhimu wa uhusiano baina ya mwanachuoni wa kidini na jamii, na jinsi kiwango chake kinavyoathiri katika jamii ya kidini, na kutokana na baadhi ya maswali na maangalizo yanayojitokeza kuhusu hali ya uhusiano huu kupitia baadhi ya mifano na harakati, sisi tutazungumzia hali hii kupitia kona muhimu kati ya kona zake, nayo ni mtazamo anaoutengeneza mwanachuoni wa kidini juu ya dhati yake kwa upande wa nafasi yake kwa wengine, na nafasi yao kwake.

**Kujikweza:**

Mwanadamu anapomiliki nukta za nguvu zinazomfanya awe juu kuliko wanaomzunguka, mara anaweza kupatwa na hali ya majivuno na maringo, na kujikuta daima tofauti aliyonayo haitoki akilini mwake, na hivyo kumpelekea kusahau dosari na upungufu alionao, jambo ambalo hutoa fursa kwa mapungufu hayo kumea na kuongezeka katika shakhisiya yake, kama ambavyo pia humfanya asahau nukta za

nguvu za wengine, na hivyo huwa haoni kama wana thamani yoyotena umuhimu wowote, bali huwatazama daima kupitia ziada aliyonayo na tofauti yake.

al-Abushihiy anataja katika kitabu chake *al-Mustatwaraf* baadhi ya mifano ya waliopatwa na maradhi ya kujikweza, ananukuu kutoka kwa Jadhiymatu al-Abrash: Kwamba alikuwa hafuatani na yeyote kwa kiburi chake na alikuwa anasema: "Hakika mimi nafuatana tu na *al-Farqadan*, yaani jua na mwezi!"

Ama Ibnu A'wanah alimwambia mfanyakazi wake siku moja: "Ninyweshe maji." Mfanyakazi akasema:"Sawa."Ibnu A'wanah Akasema: "Hakika anasema:'sawa'yule ambaye anaweza kusema 'hapana', mpigeni." Basi akapigwa! Na siku moja alimwita mkulima akaongea naye, alipomaliza akaomba maji akasukutua kinywa kwa kuona kinyaa kutokana na kuongea naye.

Masurur bin Hindu alimwambia mtu mmoja: "Unanijua?" Akasema: "Hapana." Akasema: "Mimi ni Masurur bin Hindu." Yule mtu akasema: "Sikujui." Akasema: "Maangamio na udhalili yawe kwa asiyeujua mwezi."[40]

Haya ni maradhi ya kujivuna na kujikweza, nayo ni maradhi hatari sana yanaweza kupatikana kutokana na cheo na nguvu au kumiliki mali na utajiri au kwa kupata kiwango cha elimu na nafasi ya kidini katika jamii.

Kwa sababu hiyo mwana chuoni wa kidini anakabiliwa na virusi vya maradhi haya kama hatoidhibiti dhati yake na kujitahidi kuirekebisha, kuidhibiti na kujikinga, anaweza kuwa ni muathirika wa maradhi haya hatari, ambayo yanaakisi athari zake na madhara yake katika heshima ya dini na hali ya kidini kwa ujumla.

[40] Muhammad bin Ahmad al-Abushihiy katika *al-Mustatwaraf fiy kuli fani mustatwaraf* Juz. 1, uk: 223 chapa ya pili 2000 ya al –aswiriyati

Na Sheikh Abu Hamid al-Ghazaliy anaona kwamba uwezekano wa mwanachuoni kupatwa na maradhi haya ni mkubwa zaidi kuliko mwengine yeyote, anasema katika *IhiyaauUlumi diyn*: "Ni wepesi ulioje wa kiburi kuwapata wanachuoni! Na kwa sababu hiyo amesema (s.a.w.w.): 'Maafa ya mwanachuoni ni kiburi.'Hivyo mwanachuoni asikae na kujikweza kwa utukufu wa elimu, asijihisishe katika nafsi yake uzuri wa elimu na ukamilifu wake, na asiikweze nafsi yake na kuwadharau watu na kuwaona ni kama wanyama, na asiwafanye kuwa ni wajinga, na asitake wao ndio wamwanze kwa salamu, na kama atamwanza yeyote kati yao kwa salamu au kumwitikia kwa bashasha au akimsimamia au akiitika wito wake, asione hilo ni fadhila kwake na ni msaada alioutoa kwake ambao inamlazimu msaidiwa kumshukuru yeye.

Na hapa sikuitakidi kwamba amewakirimu na amewafanyia mazuri wasiyositahiki kufanyiwa na mtu mfano wake, na kwamba inapasa wawe dhalili kwake na wamtumikie kwa kumshukuru kwa kitendo chake, bali aghlabu ni wao humfanyia wema na wala yeye hawafanyii wema, wanamzuru na wala yeye hawazuru, wanamtembelea na wala yeye hawatembelei, anamtumikisha anayeamiliana naye na anamtumia kwa mahitaji yake, hivyo kama mtu atazembea asimkemee kana kwamba ni mtumwa wake au kibarua wake na kana kwamba elimu yake ni fadhila yake kwao, na ni wema wake kwao, na ni jambo analostahiki kulipwa na wao…"[41]

**Mazingira ya mtihani:**

Namna gani mwanachuoni wakidini anatahiniwa kwa maradhi haya hatari? Na namna gani virusi vyake vinapenya katika nafsi yake? Hakika mwanachuoni wa kidini ni kama wanadamu wengine, ameumbwa katika dunia hii kwa ajili ya balaa na mtihani kutoka

[41] Abu Hamid al-Ghazaliy katika *Ihiyaai Ulumi Diyn,* Juz. 3 chapa ya kwanza ya 1992 (Beirut, Darul-Haadiy) uk. 506.

kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na mtihani wa Mwenyezi Mungu una mbinu zake na njia zake mbalimbali, unaweza kuja kupitia neema na kheri alizozipata, au kupitia shida na matatizo yaliyomfika, anasema (swt):

كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ ٱلْمَوْتِ ۗ وَنَبْلُوكُم بِٱلشَّرِّ وَٱلْخَيْرِ فِتْنَةً ۖ وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ﴿٣٥﴾

**"Kila nafsi itaonja mauti. Na tutawajaribu kwa mtihani wa shari na kheri na Kwetu mtarejeshwa." (Surat al-Anbiyai: 35)**.

Na kama ilivyo mali au cheo au uzuri ni mtihani, vivyo hivyo neema ya elimu ni sehemu ya mtihani, na kwa msingi wa jinsi mja atakavyoamiliana na neema hii ndivyo inapangika daraja yake mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na ili sura na mafunzo ya mtihani huu ambao anaupitia mwanachuoni wa kidini viwe bayana katika kona hii, tunaashiria nukta zifuatazo:

**Kwanza:**Hakuna shaka kwamba elimu ina uwezo na thamani ambayo inamuwezesha mwenye kuibeba kutukuka. Na fadhila ya elimu inadhihiri zaidi kwa mwenye nayo pindi anapoishi baina ya majahili. Anawaona wanahitajia elimu yake na anaikuta nafsi yake inatofautiana nao kwa maarifa ambayo wao hawayajui. Na hii inaweza kuwa ni sababu ya kujivuna na kukweza dhati kwa baadhi ya wenye kubeba elimu, na hususani kwa asiyechanganyika na maulamaa walio mfano wake au waliojuu yake, na daima huishi na hisia ya kuwa yeye ni mtu tofauti ndani jamii yake. Ama yule anayechanganyikana wenye kumzidi elimu au wenye kulingana naye katika fadhila, hali hiyo inaweza kumsaidia kuleta uwiano katika hisia zake na kusawazisha dhati yake.

Na huwenda baadhi ya ulamaa katika raghaba yao ya kujitenga mbali na wasomi wengine miongoni mwa watoto wa rika lao, na

kutotaka kuchanganyikana wafuasi wao na wanafunzi wao wanaomhitajia, huwa wanataka kuishi daima katika hali ya kuhisi kuwa wao ni watu tofauti.

**Pili:** Kuna baadhi ya nususi za kidini nyingi zinazungumzia fadhila za mwanachuoni na nafasi yake, ambapo aya tukufu zinakiriubora wa mwanachuoni katika muundo wa swali katika kauli yake (swt):

قُلْ هَلْ يَسْتَوِي ٱلَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَٱلَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُو۟لُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ

**"Sema: Je, wanalingana sawa wale ambao wanajua na wale ambao hawajui? Hakika wanaokumbuka ni wenye akili tu."** **(Surat Zumar: 9)**.

Imekuja katika Hadithi tukufu kutoka kwa Nabii (s.a.w.w.): "Fadhila ya mwanachuoni kwa shahidi ni kubwa zaidi kwa daraja moja."[42] Na kutoka kwake (s.a.w.w.): "Hakika Malaika humfunika kwa mbawa zao yule mwenye kutafuta elimu." Na kutoka kwake (s.a.w.w.): "Mwenye kutafuta elimu Malaika humkunjulia mbawa zao kwa kuridhia anayoyatafuta." Na kutoka kwake (s.a.w.w.): "Fadhila ya elimu kwa mja ni kama fadhila ya mwezi usiku wa mbalamwezi kwa sayari zingine."[43]

Kuna Hadithi na riwaya nyingi katika kubainisha fadhila za mwanachuoni na nafasi yake. Aliyepewa elimu anapoziona nususi hizi na kuzisoma inaweza kutokea kwake aina fulani ya ghururi na majivuno, kama tu ataizingatia nafsi yake kuwa ndio mfano halisi na sehemu halisi ya kutabikisha riwaya hizo.

**Tatu:**Hadhi anayoipata mwanachuoni wa kidini ya kutukuzwa na kuheshimiwa na watu, ambapo huonekana na kudhihirika hadhi

[42] Fadhili bin Hasan Twabarisiy katika *Majimaul-Bayaan* Juz. 9 uk. 418 chapa ya kwanza ya 1995 (Beirut muasasatul- ilimiy ya uchapishaji)

[43] *Kanzul-Umaal*, Hadith namba 28726

hiyo kwa kumsimamia kwao anapoingia, kumtanguliza katika mambo, kumpa nafasi ya mbele katika vikao, kubusu uso wake au mkono wake kama ilivyo ada katika baadhi ya jamii, na kurejea kwenye rai yake katika mas'ala na mambo mbalimbali, yote hayo yanaweza kukweza hisia zake na kumfanya ajikweze na kuhisi tofauti.

Hakika kuwaheshimu wenye elimu na kuwatukuza ni jambo linalotakiwa, akili inalikubali na sheria inaliamuru, kwa sababu huo ni udhihirisho wa kuiheshimu dini na elimu. Na ni utangulizi wa kuitikia maelekezo ya maulamaa na mafunzo yao. Imepokewa katika Hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Mwenye kuwapokea maulamaa, basi ameshanipokea mimi, na mwenye kuwatembelea maulamaa basi ameshanitembelea mimi, na mwenye kukaa na maulamaa basi ameshakaa na mimi, na mwenye kukaa na mimi kana kwamba amekaa na Mola Wangu."[44] Na kutoka kwake (s.a.w.w.): "Wakirimuni maulamaa. Hakika wao ni warithi wa Manabii, mwenye kuwakirimu basi ameshamkirimu Mwenyezi Mungu na Mtume Wake."[45]

**Malezi ya kiroho na kitabia:**

Kama ambavyo mali na utajiri unaweza kuwa ni sababu ya upotovu na uasi:

كَلَّآ إِنَّ ٱلْإِنسَـٰنَ لَيَطْغَىٰٓ ۝٦ أَن رَّءَاهُ ٱسْتَغْنَىٰٓ ۝٧

**"Si hivyo! Hakika mtu bila ya shaka hupituka mipaka. Kwa kujiona amejitosheleza."** **(al-Alaq: 6 – 7)**.

Na madaraka yanaweza kuwa ni sababu ya dhulma na ukandamizaji, vile vile elimu inaweza kuwa ni sababu ya ghururi na kiburi,

[44] *Kanzul-Umaal* Hadith namba 28883
[45] Rejea iliyotangulia hadithi namba 28764

na kwa sababu hiyo imepokewa kutoka kwa wema waliotutangulia: “Hakika katika elimu kuna uasi kama vile uasi wa mali.”[46]Na kwa ajili ya kupata uwiano wa kinafsi kwa mtu na kudhibiti uasi wa hisia zake na ubinafsi wake ni lazima kuilea roho katika tabia njema.

Mwanachuoni wa kidini akipata fungu tosha la kuitakasa nafsi anakuwa na kinga na ulinzi kutokana na maradhi ya majivuno, ghururi na maradhi mengine ya kitabia. Na kwa sababu hiyo Qur’aniTukufu inatanguliza utakaso wa nafsi kabla ya kujifunza, hiyo ni kwa sababu ya umuhimu wake, Mwenyezi Mungu (swt) anasema:

هُوَ ٱلَّذِى بَعَثَ فِى ٱلْأُمِّيِّـۧنَ رَسُولاً مِّنْهُمْ يَتْلُوا۟ عَلَيْهِمْ ءَايَـٰتِهِۦ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ
ٱلْكِتَـٰبَ وَٱلْحِكْمَةَ وَإِن كَانُوا۟ مِن قَبْلُ لَفِى ضَلَـٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٢﴾

**“Yeye Ndiye Aliyempeleka Mtume kwenye watu wasiojua kusoma, aliyetokana na wao, awasomee Aya Zake, na awatakase, Na awafunze Kitabu na hikima, Japokuwa hapo kabla walikuwa katika upotofu ulio dhahiri. “ (Surat al-Jumu’a: 2)**.

Nususi za kidini zinatia mkazo juu ya dharura ya kutakasa nafsi kwanza, hususan kwa mwanachuoni wa kidini, anasema Imamu Ali (as): “Mwenye kuinasibisha nafsi yake kuwa imamu wa watu basi aanze kuifunza nafsi yake kabla ya kumfunza mwingine, na iwe kujiadabisha kwake ni kwa mwenendo wake kabla ya kuadabisha kwa ulimi wake. Na mwenye kuifunza nafsi yakeana haki zaidi ya kuheshimiwa kuliko mwenye kuwafundisha watu na kuwaadabisha.”[47] Na anasema(s.a.w.w.): “Vipi atamrekebisha mwingine yule ambaye harekebishi nafsi yake.”[48]

---

[46] Ihiyaau Ulumi diyn Juz. 3, uk. 527
[47] *Nahjul-Balaghah*, hekma namba 73
[48] Abdul-Wahdi al-Amadiy Tamiymiy katika *Ghuraril-Hilkimi wa Durari l-kalimi* chapa ya kwanza 1987 (Beirut muasasatu al-Alamiy ya uchapishaji)

Hakika malezi ya kiroho yanafanya mtazamo wa mwanadamu juu ya nafsi yake uwe ni wenye uhalisia zaidi na wa kimaudhui zaidi, na kila anaposonga mbele kielimu ndivyo anavyojua undani wa maarifa na upana wa wigo wa elimu, na anatambua kwamba aliyoyapata katika elimu si kingine isipokuwa ni kidogo tu na ni kiasi kidogo sana, na hali hiyo huziba mianya ya majivuno na ghururi na maringo kwenye nafsi yake, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَمَآ أُوتِيتُم مِّنَ ٱلۡعِلۡمِ إِلَّا قَلِيلٗا ٨٥

**"Nanyi hamkupewa katika elimu ila kidogo tu."** **(Suratal-Israai: 85)**.

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwamba amesema: "Mwenye kusema mimi ni mwanachuoni basi yeye ni jahili."[49] Na katika wasia wake kwa mtoto wake Hasan anasema Imamu Ali (as): "Hakika mwanachuoni ni yule ambaye anajua kwamba anayoyajua katika yale asiyoyajua ni machache sana, na hivyo anaihesabu nafsi yake kuwa ni jahili."[50]

Inanukuliwa katika sira ya mwanafalsafa na mwanafiqihi Mula Haadiy as-Sabzawaariy aliyezaliwa 1212 na kufariki 1289 Hijiria, mwenye *al-Mandhumatul-Falsafiyatu* ambacho kinasomeshwa katika Hawza za elimu, kwamba alikwenda mji wa Karmaan bila kujulikana na yeyote, ili abakie humo kwa muda fulani, akaingia katika madrasa na akaomba chumba kwa msimamizi wa madrasa na huyo msimamizi, kwa kuwa hakuwa anamjua akamuuliza: "Je, wewe ni kati ya maulamaa?" Akasema: "Hapana." Msimamizi akasema: "Hakika vyumba ni maalum kwa ajili ya wanafunzi, lakini unaweza kubakia katika chumba cha mtumishi

[49] *Biharul-Anwaar,* Juz. 2 uk. 110
[50] *Biharul-Anuwaari*, Juz. 74 uk. 221

wa madrasa ili umsaidie kazi za utumishi."Akaafiki na akabakia hivyo hadi pale walipoijua shakhsiya yake.[51]

Mwanachuoni wa hadithi mkubwa Sheikh Abbas al-Qumiy aliyezaliwa mwaka 1294 na kufariki mwaka 1359 Hijiria, mwandishi mwenye vitabu vingi mashuhuri,[52] alipoandika kitabu chake *al-Fawaid ar-Ridhawiyyah Fii Tarajumi Ulamaail-Imamiyyah*, kitabu kinachozungumzia wasifu wa maulamaa wa Kishia, alipofika katika kutoa wasifu wake mwenyewe kama mmoja wa maulamaa wa Kishia, aliandika hivi: "Kwa kuwa kitabu hiki kinabainisha hali za maulamaa, sioni kama inafaa mimi mwenyewe kuwasilisha wasifu wangu mwenyewe, kwani mimi ni duni na mdogo ambaye sipasi kuiweka nafsi yangu miongoni mwao, na kwa ajili hiyo sintashughulika na wasifu wangu bali nitakomea tu kutaja vitabu vyangu."[53]

Na mmoja kati ya Marajii alikuwa anaandika katika saini yake: *Turabu Aqdaamil-Ulamaai*, yaani vumbi la nyayo za maulamaa. Na imeenea kwa maulamaa wengi kwamba huandika katika saini zao 'mtu duni'. Hivi ndivyo hufanya mara nyingi mwanachuoni mwenye kuiadabisha nafsi yake. Badala ya kuihesabu nafsi yake kuwa ni mwanachuoni, yeye huiona si chochote, achilia mbali kutotawaliwa na majivuno, ghururi au kujifakharisha kwa elimu yake.

**Elimu ni wajibu na taklifu:**

Mwanadamu anaposoma elimu ya dini hutarajiwa kuwa itamfanya awe ni mwenye ufahamu zaidi wa utukufu wa Mwenyezi Mungu, na ni mwenye kuhisi zaidi kuwa ana majukumu na wajibu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kwamba elimu anayoipata ni hoja

[51] Haiatu Muhammad al-Amini: *al-Akhlaaqi wal-Adaabul-Islamiyati* chapa ya kwanza 2000 (Kuwait) uk. 235

[52] Sheikh Abbas al-Qumiy ndiye mwandishi wa kitabu maarufu cha dua na maombi, kitabu *Mafatihul-Jinan* ambacho kwa sasa kinapatikana kwa lugha ya Kiswahili katika maduka ya *al-Itrah Foundation* –Mhariri.

[53] Sheikh Radhiyu Mukhtar, *Saymaus-Salihin,* Chapa ya 1992 Miladiya, Beirut.

juu yake mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa sababu hiyo wanasifika maulamaa kwa wingi wa hofu na kumuogopa Mwenyezi Mungu, anasema (swt):

إِنَّمَا يَخْشَى ٱللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ ٱلْعُلَمَٰٓؤُا۟ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ عَزِيزٌ غَفُورٌ ﴿٢٨﴾

**"Hakika si mengineyo wanaomcha Mwenyezi Mungu, katika waja Wake ni wale wajuzi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye maghufira."** **(Surat Fatwir: 28)**.

Elimu ya dini ni wajibu na taklifu kabla ya kuwa hadhi na utukufu, na ni juu ya wenye kubeba elimu waweke mbele ya macho yao tahadhari ya kiungu iliyoelekezwa kwao kupitia aya za Qur'ani tukufu na Hadith za Nabii (s.a.w.w.) na kizazi chake kitukufu (as), ili wadhibiti uasi wa ubinafsi katika nafsi zao na ili wazidhalilishe nafsi zao daima na milele kwa ajili ya kuzihisabu na kuzichunga, na ili wakumbuke kwamba hali yao ni hatari kuliko watu wengine, na kwamba watu wa kawaida ni wenye wajibu mwepesi kuliko wao, na ni wenye hisabu nyepesi mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuliko wao.

Kuna idadi ya Hadithi tukufu zinahadharisha kuitumia elimu kwa ajili ya kupata umaarufu na kujitokeza kijamii, imekuja katika Hadith kutoka kwake (s.a.w.w.): "Mwenye kutafuta elimu kwa ajiliya kuwajadili wapumbavu au kwa ajili ya kuwajadili maulamaa au kwa ajili ya kuwavutia watu kwake basi na ajiandalie makazi yake motoni."[54]

Na hadithi kadhaa zinaashiria ukubwa wa hisabu na adhabu ya mwenye elimu kama hakujali majukumu yake na wajibu wake. Imepokewa kutoka kwake (s.a.w.w.) kwamba amesema: "Nilipelekwa

[54] *Kanzul-Umaal* Hadith namba 29057

siku ya Israi kwa watu waliokuwa wanakatwa midomo yao kwa mikasi ya moto, nikasema: 'Ewe Jibril ni nani hawa?' Akasema: 'Ni makhatibu wa ummah wako. Wanasema wasiyoyafanya na wanasoma kitabu cha Mwenyezi Mungu na wala hawakifanyii kazi.'"[55]

Na kutoka kwake (s.a.w.w.): "Hakika watu wenye adhabu kali zaidi Siku ya Kiyama ni mwanachuoni ambaye Mwenyezi Mungu hajamnufaisha kwa elimu yake."[56] Na kutoka kwake (s.a.w.w.): "Malaika wa motoni ni wepesi zaidi kwa mafasiki wenye kubeba Qur'ani miongoni mwao kuliko waabudu masanamu, basi watasema: Wataanza kwetu kabla ya waabudu masanamu? Wataambiwa: Anayejua sio sawa na asiyejua."[57] Imepokewa kutoka kwa Imamu Ja'far as-Sadiq (as): "Hakika anasamehewa jahili dhambi sabini kabla ya kusamehewa mwanachuoni dhambi moja."[58]

Nususi hizi na mfano wake zinamkumbusha mwanachuoni wa kidini jukumu na wajibu wa kutenda kwa mujibu wa elimu yake na kuitumia bila majivuno na ghururi, hivyo hakuna thamani ya elimu bila ya uchamungu, wala haina faida ikiwa haitoambatana na tabia njema.

**Unyenyekevu ni matunda ya elimu:**

Kukuza dhati kunampelekea mhusika ajione kuwa ni bora zaidi kuliko watu wengine kutokana na elimu aliyoipata, na kwamba ni wajibu watu wamheshimu na kumtukuza, wamkirimu na wamfurahishe kwa kumtumikia. Na wakubali kutoka kwake kila kitu bila ya kujadili wala kupinga, kwani yeye ni mwanachuoni na anawakilisha sharia na anasema kwa jina lake, na wao ni watu wasio na elimu, kazi yao ni kusikiliza na kutii. Na anaweza kuona nafsi yake ni mlango wa radhi za Mwenyezi Mungu na msamaha wake, asiyeafiki

---

[55] *Kanzul-Umaal* Hadith ya 29026
[56] Rejea iliyotangulia Hadith ya 29099
[57] " " 29005
[58] *Bihaarul- Anuwaar*, Juz. 2 uk. 27

rai yake na kunyenyekea katika matakwa yake basi ameshafukuzwa katika rehema za Mwenyezi Mungu. Na hayo yanafanana na yale waliyodai viongozi wa kanisa katika zama za kati walipokuwa wanauza mkataba wa msamaha kwa watu. Hakika fikra hii na tabia hii ni kinyume na msingi wa elimu na inakhalifu madhumuni ya dini:

أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٦٠﴾

**"Je, si katika Jahannamu makazi ya wanaotakabari?"(az-Zumar:60).**

Na kutoka kwake(s.a.w.w.): "Watu wenye kuchukiwa sana ni wenye kiburi."[59] Na Mwenyezi Mungu anaamrisha unyenyekevu na anawapenda wanyenyekevu;anasema (swt):

فَسَوْفَ يَأْتِي ٱللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُۥٓ أَذِلَّةٍ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى ٱلْكَـٰفِرِينَ

**"Mwenyezi Mungu atawaleta watu anaowapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa waumini, wenye nguvu juu ya makafiri." (al-Maida: 54).**

Na anasema Imamu Ali (as): "Jilazimishe kunyenyekea, hakika hiyo ni ibada tukufu mno."[60]

Na elimu ya kweli inamsukuma mwenye elimu kuwa mnyenyekevu kwa watu, na kila kiwango chake cha elimu kinapoongezeka nafsi yake inazidi unyenyekevu na upole, imekuja katika Hadithi kutoka kwake (s.a.w.w.): "Mwenye kutafuta elimu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu hatopata mlango isipokuwa utazidi udhalili katika nafsi yake na unyenyekevu kwa watu, hofu kwa Mwenyezi Mungu na juhudi katika dini, na huyo ndiye anayenufaika kwa elimu yake."[61]

[59] *Biharul-Anuwaar*, Juz. 70, uk: 231
[60] Rejea iliyotangulia, Juz. 72 uk. 119
[61] " " Juz. 2 uk. 34

Ama kujikweza na kiburi ni sifa ya wanaojidai wana elimu, ambao wanaitumia kwa ajili ya kushibisha utashi wao. Imepokewa kutoka kwake (s.a.w.w.): "Mwenye kutafuta elimu kwa ajili ya dunia na kupata cheo kwa watu na heshima kwa watawala, hatoingia mlango isipokuwa yatazidi katika nafsi yake makuu na kiburi kwa watu, na ghururi kwa Mwenyezi Mungu na uovu katika dini, na huyo ni asiyenufaika na elimu yake."[62]

Vivyo hivyo, hakika maarifa ya kweli yanamlea mwanadamu katika unyenyekevu na yanakuza katika nafsi yake heshima kwa wengine. Anasema Imamu Ali (as): "Unyenyekevu ni tunda la elimu."[63] Na anasema (as): "Na hakika haipasi kwa mwenye kujua utukufu wa Mwenyezi Mungu kujikweza."[64]

Na mwisho tumuombe Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa unyenyekevu pamoja na Imamu Zainul-Abdiyn (as) katika dua ya *Makarimul-Akhilaq* ambapo anasema: "Eee Mwenyezi Mungu mteremshie rehema Muhammad na kizazi cha Muhammad, na wala usininyanyue daraja kwa watu isipokuwa unishushe katika nafsi yangu kwa mfano wake, na wala usinipatie utukufu wa dhahiri isipokuwa unipatie udhalili ndani ya nafsi yangu kwa kiwango kile kile."Amin ewe Mola Mlezi wa viumbe.

## TUNDA LA ELIMU NI UNYENYEKEVU

Yeyote mwenye kuhisi anawashinda na kutofautiana na wengine kwa kumiliki kwake nguvu maalumu, ili hisia zake zisimsukume katika kujikweza, majivuno na kiburi, ni wajibu azidhalilishe hisia hizi kwa kutafiti na kujiuliza: Je, ni kweli yeye ni tofauti na yuko juu ya wengine?

[62] *Biharul-Anuwar*, Juz. 2, uk. 35
[63] *Ghurarul-Hikami wa Durari-Balimi*
[64] *Nahjul-Balaghah*, khutuba ya 147

Hakika nukta za nguvu na maendeleo zinatofautiana baina ya watu, ni mara chache na nadra sana kukusanyika kwa mtu mmoja sababu zote zinazomfanya mtu awe juu zaidi ya wengine, mtu anaweza kuwa juu kielimu, na mwingine katika uwezo wa kuendesha mambo, na mwingine katika kumiliki utajiri, na wanne katika kupata nguvu na utawala, na watano kwa uzuri na umbo zuri, na wa sita katika kabila na ukoo n.k. Na kisha hakika ni juu ya mwanadamu afanye hisabu makini kwa kutizama nguvu za wengine na wala asijikweze kwa yeyote maadamu yeye hapendi yeyote awe na kiburi kwake.

Sisi kama Waislamu, tunaitakidi kwamba kupata ukaribu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kunusurika Siku ya Kiyama ndio ushindi mkubwa na kufaulu kuliko muhimu. Je, mtu anaweza kujihakikishia hilo katika nafsi yake? Je, mwanachuoni wa kidini anaweza kuthibitisha mfano wa hayo kwamba yuko karibu zaidi na Mwenyezi Mungu na ana haki zaidi katika ridhaa Yake na pepo Yake kuliko hawa watu wa kawaida ambao anaweza kuhisi ubora wake juu yao?

Imekuja katika Hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Huwenda mwenye nywele timtimu, mwenye vumbi na aliye masikini mwenye kudharauliwa, atakubaliwa kama ataapa kwa Mwenyezi Mungu**.**"[65] Na anasema Imamu Ali (as): "Utajiri na ufakiri ni baada ya kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu."[66]

Hakika maasumina ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu amewateua kati ya waja wake, pamoja na kwamba wanamiliki duniani na Akhera ubora mkubwa na tofauti ya ukamilifu mbele ya wasiokuwa wao, isipokuwa wao wanasifika kwa daraja la juu kabisa la unyenyekevu, katika nyoyo zao hakuna hata chembe ndogo ya majivuno, wala haidhihiri kwao fikra ya kiburi wala kujikweza kwa yeyote.

---

[65] *Kanzul-Umaal* Hadith namba 5953

[66] *Nahjul-Balaghah*: Qiswaarul-hikami 452

Nabii wetu Muhammad (s.a.w.w.) ni bwana wa viumbe na ndio mbora wao mbele ya Mwenyezi Mungu, na ndiye aliyepata ubora kushinda viumbe vyote, lakini kama tutasoma sira yake nzuri tutakuta yeye ni mfano wa juu kabisa katika unyenyekevu na wepesi katika kuamiliana na watu, na katika uongofu wake wamepita Maimamu watukufu wa Ahlulbayt wake na masahaba wema:

أُوْلَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ هَدَى ٱللَّهُۖ فَبِهُدَىٰهُمُ ٱقۡتَدِهۡۗ قُل لَّآ أَسۡـَٔلُكُمۡ عَلَيۡهِ أَجۡرًاۖ إِنۡ هُوَ إِلَّا
ذِكۡرَىٰ لِلۡعَٰلَمِينَ ﴿٩٠﴾

**"Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewaongoza, basi fuata mwongozo wao. Sema: Siwaombi ujira juu ya haya. Haikuwa hiyo ila ni mawaidha kwa walimwengu wote."** **(Surat al-An'aam: 90)**.

**Unyenyekevu wa Mawalii:**

Hakika unyenyekevu ni siri kati ya siri ya utukufu wa mawalii wa Mwenyezi Mungu, nao unatokana na malezi ya kiungu ambapo Mwenyezi Mungu anawafunza adabu Manabii wake na anawaelekeza katika tabia hii njema. Anasema Mwenyezi Mungu akimhutubia Nabii wake:

لَا تَمُدَّنَّ عَيۡنَيۡكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعۡنَا بِهِۦٓ
أَزۡوَٰجًا مِّنۡهُمۡ وَلَا تَحۡزَنۡ عَلَيۡهِمۡ وَٱخۡفِضۡ جَنَاحَكَ لِلۡمُؤۡمِنِينَ ﴿٨٨﴾

**"Usikodolee macho yako yale tuliyowastareheshea makundi mbalimbali. Wala usiwahuzunikie. Na inamisha bawa lako kwa Waumini."**

**(Surat al-Hijir: 88)**.

**Na aya nyingine:**

وَٱخۡفِضۡ جَنَاحَكَ لِمَنِ ٱتَّبَعَكَ مِنَ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ ﴿٢١٥﴾

**"Na inamisha bawa lako kwa wanaokufuata katika waumini."**
**(Surat Shu'araa: 215)**.

Na kuinamisha bawa ni mfano wa upole na unyenyekevu, ni sawa na hali ya ndege anapotaka kutua ardhini, anainamisha mabawa yake akitaka kuteremka au akitaka kujitayarisha kwa kuwafunika vifaranga wake, ndege wanapotaka kudhihirisha upole wao kwa vifaranga vyao wanaviweka chini ya mabawa yao baada ya kuyainamisha.

Na kufanya unyenyekevu ni kitendo cha ibada kwa Manabii na mawailii, kwacho wanajikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, anasema (s.a.w.w.): "Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanyenyekevu na anawachukia wenye kiburi."[67] Na amesema (s.a.w.w.) siku alipowaambia baadhi ya Masahaba zake: "Mbona sioni kwenu utamu wa ibada?" Wakasema:"Ni nini utamu wa ibada?" Akasema: "Unyenyekevu."[68] Na amesema Imam Ali (as): "Jilazimishe kufanya unyenyekevu hakika ni kati ya ibada tukufu mno."[69]

Na kwa unyenyekevu Manabii wanazivutia nyoyo za watu katika daawa yao ya kiungu, ambapo watu wanampenda anayenyenyekea kwao, wakati ambapo wanamkimbia yule anayejikweza kwao na kufanya kiburi kwao. Anasema Imamu Ali (as): "Tunda la unyenyekevu ni upendo, na tunda la kiburi ni matusi."[70]

Na Qur'an inakiri ukweli huu na kutilia mkazo kwamba tabia ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ndio iliyowavutia watu katika dini, na kama sio huruma yake na upole wake wakati wa kua-

[67] *Kanzul-Umaal* Hadith ya 5734
[68] Muhammad al-Mahdiy Naraaqiy katika *Jaamiu Sa'adaati* Juz. 1, uk: chapa ya saba ya 1422 (Beirut muasasatu al-alamiy ya uchapishaji) uk. 394
[69] *Biharul-Anuwaar*, Juz. 72 uk. 119
[70] *Ghurarul-Hikami wa-durarul-Kalimi*

miliana nao basi wasingekubali daawa yake, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

فَبِمَا رَحْمَةٍ مِّنَ ٱللَّهِ لِنتَ لَهُمْ ۖ وَلَوْ
كُنتَ فَظًّا غَلِيظَ ٱلْقَلْبِ لَٱنفَضُّوا۟ مِنْ حَوْلِكَ ۖ فَٱعْفُ عَنْهُمْ وَٱسْتَغْفِرْ لَهُمْ
وَشَاوِرْهُمْ فِى ٱلْأَمْرِ ۖ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى ٱللَّهِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُتَوَكِّلِينَ ﴿١٥٩﴾

**"Kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu, umekuwa laini kwao. Lau ungelikuwa mkali mwenye moyo mgumu, bila shaka wangelikukimbia. Basi wasamehe na uwaombee maghfira na ushauriane nao katika mambo. Utakapoazimia, basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wamtegemeao." (Surat al-Imaraan: 159).**

Na ikiwa unyenyekevu unatakiwa kwa kila mmoja, basi mwanachuoni wa kidini anafaa zaidi na anastahiki zaidi kuwa na tabia hii njema, kwa kuyajua kwake mafunzo ya Uislamu, kwa kujishughulisha kwake na ulinganiaji na uongozaji, na kwa nafasi yake ya kidini aliyonayo katika macho ya watu, ambapo mtazamo wa watu wengi kuhusu dini hupatikana kupitia shakhisiya yake na mwenendo wake. Na kwa unyenyekevu na tabia yake njema anaipa dini sura nzuri na mwonekano mzuri unaovutia nafsi za watu kwenye dini. Ama akiwa amepatwa na maradhi ya majivuno na kujikweza, atafeli katika jaribio la kuvutia nyoyo za watu, na atatoa mfano mbaya wa hali ya dini.

Na tunajifunza kutoka katika madrasa ya tabia njema za Nabii (s.a.w.w.), baadhi ya mafunzo ya tabia ya unyenyekevu ili yawe ni taa kwa wanaolingania kwa Mwenyezi Mungu na wenye kujali mambo ya kidini na ya kijamii.

**Kutokuhusudu kutukuzwa:**

Katika kila jamii yameenea mambo na mila za kudhihirisha heshima na kuwatukuza watu maarufu, na hadhi ya mwanachuoni katika jamii ya Kiislamu, kwani watu huonyesha kwake heshima nyingi ya utukufu, hivyo husimama kwa ajili ya kumheshimu pindi anapoingia katika kikao, na wanampa nafasi ya kukaa mbele ya baraza, na wanamuanza kwa kumsalimu na kumwamkia.Wanabusu kichwa chake au mkono wake, na wanamtanguliza mbele yao katika mambo na misimamo mbalimbali, na katika shughuli zingine na maadhimisho mbalimbali.

Mila na desturi hizo zinaweza kutofautiana kulingana na jamii husika. Hakika kumheshimu mwanachuoni wa kidini na kumuenzi ni jambo linalotakiwa na linalopendeza sana kisharia kama zinavyoonyesha hivyo nususi zilizopokelewa. Lakini mwanachuoni wa kidini mwenyewe inapasa asiyape mambo hayo mazingatio makubwa katika nafsi yake, na hivyo kutu kuzwa huko kukawa kana kwamba ni wajibu ambao watu wanawajibika kumtendea, na kana kwamba ni haki yake ya msingi na hivyo anakereka pindi anapozembea yeyote kuitekeleza kwake. Hivyo kama ataingia katika kikao na ikatokea baadhi ya wahudhuriaji hawajamsimamia, au hawajampa nafasi ya mbele, au hawaja mtanguliza, na hawajamfanyia mengine ya utukuzo mfano wa hayo, hakika ni wajibu kwake kutoruhusu hali hiyo kuacha athari mbaya katika nafsi yake. Na kwa maneno mengine hakika asitafute utukufu huo wala usimshughulishe.

Hakika kusimama anapowasili muuminina hususan mwanachuoni au ambaye anatokana na kizazi cha Nabii (s.a.w.w.), ni jambo la mustahabu. Imepokewa kutoka kwa Is'haq bin Ammaar amesema: "Nilimwambia Abi Abdillahi as-Sadiq (as): Vipi kuhusu mwenye kusimama mahala pake kwa kumtukuza mtu? Akasema (as):'Ni

makuruhu isipokuwa kwa mtu wa dini.'"[71] Na imepokewa katika sira ya Nabii kwamba yeye (s.a.w.w.) alikuwa anasimama pindi baadhi ya watu wanapoingia kwake, isipokuwa alikuwa anachukia watu kumsimamia kwa ajili ya kumnyenyekea yeye.

Imekuja katika Hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwamba amesema: "Mwenye kutaka watu wamsimamie basi ajiandalie makazi yake motoni."[72] Imepokewa Hadithi hii katika *Sunan Abi Daud*, *Wasailu Shiah*, *Mustadrak* na *Biharul- An'war*.

Na kutoka kwa Abu Ummamah amesema: "Alitoka kwetu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)huku akiwa ameegemea fimbo, tulipomsimamia akasema: 'Msisimame kama wanavyosimama waajemi, kwa baadhiyao kuwatukuza baadhi yao.'"[73] Na kutoka kwa Zayd Zaraad katika asili yake amesema: "Nilimsikia Abu Abdillahas-Sadiq (as) akisema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alitoka siku moja kutoka katika baadhi ya vyumba vyake, watu kati ya Masahaba wake walikuwa wamekusanyika na mara walipomuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) wakasimama. Akawaambia: 'Kaeni na wala msifanye kama wanavyofanya waajemi katika kutukuzana.'"[74]

Na kutoka kwa Anasi bin Maliki amesema: "Hakuna mtu aliyekuwa anapendeza kwao kuliko Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), na walikuwa wanapomuona hawamsimamii kutokana na wanavyojua jinsi anavyochukia hilo."[75] Abu Dardai amesema: "Katika baadhi ya nyakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ali-

---

[71] *Bihaarul-Anuwaar*, Juz. 72, uk: 466

[72] Abu Daud Suleiman bin al-Ash'ath as Sajastaaniy katika *Sunan Abi Daudi* chapa ya kwanza 1988 (Beirut: Daarul-Jinaan - Muasasatu Thaqaafah) Hadith namba 5229.

[73] *Sunan Abi Daud* Hadith ya 5230

[74] Sheikh Ali Namaaziy katika *Mustadrak Safiynatil-Bihaar*, Juz. 8, chapa ya 1418 Hijiria (Qum: Muasasatu Nashiril-Islaaamiy) uk. 632

[75] *Biharul-Anwaar*, Juz. 16 uk. 229

kuwa anatembea pamoja na Masahaba wake na mara anawaamuru watangulie na anatembea nyuma yao."[76] Na kutoka kwa Abu Dharr al-Ghafaariy amesema: "Nilimuona Salman na Bilal wanamjia Nabii (s.a.w.w.) ambapo Salman aliinama katika nyayo za Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuzibusu. Nabii (s.a.w.w.) akamkemea kwa hilo kisha akamwambia: 'Ewe Salman usinifanyie hivyo kama wanavyowafanyia waajemi wafalme wao, mimi ni mja kati ya waja wa Mwenyezi Mungu.'"[77]

Amenukuu Sharif Radhii katika *Nahjul-Balaghah* kwamba Imamu Ali (as) wakati wa kwenda kwake Sham alipitia Anbaar, wakamwendea viongozi wa wakulima na wakasongamana mbele yake, akasema (as): 'Ni nini hiki mlichofanya?' Wakasema: 'Ni tabia yetu, kwayo tunawatukuza viongozi wetu.' Akasema: 'Wallahi hawanufaiki kwa haya viongozi wenu!Hakika nyinyi mnazitaabisha nafsi zenu, na kwa hayo mtapata taabu katika Akhera yenu."[78]

Na kutoka kwa Hisham bin Salim kutoka kwa Imamu as-Sadiq (as) amesema:"Amirul-Mu'minina (as) alitoka na wafuasi wake naye amepanda farasi, wakawa wanatembea nyuma yake, mara alipowageukia alisema: 'Mnahaja yoyote?' Wakasema hapana ewe Amirul-Mu'minina, lakini sisi tunapenda kutembea pamoja na wewe, akawaambia. 'Ondokeni hakika matembezi ya pamoja ya mmoja anatembea kwa miguu na mwingine amepanda kipando, ni kumharibia aliyepanda na ni udhalili kwa anayetembea kwa miguu.'" Akasema: "Na wakati mwingine alipanda, wakatembea nyuma yake, yeye akasema: Ondokeni, hakika mtikisiko wa viatu nyuma ya visigino vya wanaume huharibu nyoyo za wapumbavu."[79]

[76] Rejea iliyotangulia Juz. 70, uk. 206
[77] Rejea iliyotangulia Juz.73 uk. 63
[78] *Nahjul-Balaghah* Qwaaril-hikam 37
[79] *Biharul-Anwaar*, Juz. 41 uk. 55

Na kuhusu kukaa mbele kwenye baraza, zimepokewa Hadith nyingi zinazoashiria kwamba kupenda jambo hilo kunafichua daraja ya majivuno na kujikweza, na kwamba tabia ya unyenyekevu inapelekea kujizuia na hali hii. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Hakika miongoni mwa matendo yakuonesha unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu ni kuridhia kukaa mwisho wa baraza."[80] Na kutoka kwa Imamu as-Sadiq (as): "Unyenyekevu ni kuridhia kukaa sehemu iliyo chini ya hadhi yako, kuwasalimia uliowakuta, na kuacha kujionyesha hata kama unastahiki, na kilele cha kheri ni unyenyekevu."[81]

Imepokewa kutoka kwa Abi Abdillahi as-Sadiq (as) amesema:"Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa anapoingia katika nyumba hukaa mwisho wa baraza pale anapoingilia, na kwamba (s.a.w.w.) alisema: 'Anapoingia mmoja wenu katika majilisi basi akae sehemu ambayo majilisi imeishia.'"[82]

Vivyo hivyo ni mustahabu kwa watu kuonesha heshima kwamwanachuoni wa kidini, lakini mwanachuoni wa kidini inapasa asihusudu mandhari haya wala asiyatafute au asikasirike kwa sababu ya kuyakosa.

**Kuheshimu watu na kuwahudumia:**

Mwanachuoni anajua zaidi kuliko mwingineyeyote nafasi ya watu na utukufu wao katika mafunzo ya Uislamu, kwani Mwenyezi Mungu amejaalia mwanadamu akirimiwe kama mwanadamu bila kuangalia tofauti zingine zinazomnyanyua na kumpa daraja la nyongeza la heshima, lakini asili ya kutukuzwa imehifadhiwa kwa watu wote, anasema (swt):

[80] *Kanzul-Umaal* Hadith 5724
[81] *Biharul-Anwaar*, Juz. 72, uk. 123
[82] *Biharul-Anwaar*, Juz. 16, uk. 240

﴿ وَلَقَدۡ كَرَّمۡنَا بَنِيٓ ءَادَمَ وَحَمَلۡنَٰهُمۡ فِي ٱلۡبَرِّ وَٱلۡبَحۡرِ وَرَزَقۡنَٰهُم مِّنَ ٱلطَّيِّبَٰتِ
وَفَضَّلۡنَٰهُمۡ عَلَىٰ كَثِيرٖ مِّمَّنۡ خَلَقۡنَا تَفۡضِيلٗا ٧٠ ﴾

**“Hakika tumewatukuza wanaadamu na tumewabeba nchi kavu na baharini na tumewaruzuku vitu vizuri na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tuliowaumba.”** **(Surat Israai: 70)**.

Watu wa kawaida hata kama hawana kiwango bora cha elimu lakini wao bado ni wanadamu wana utukufu wao na heshima yao, hivyo haisihi kwa mwanachuoni kumdharau yeyote miongoni mwa watu, kwa sababu tu ya wao kutokuwa na elimu. Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anawapenda viumbe wake na anampenda anayewaheshimu na anayewanufaisha kama ilivyopokewa katika *Hadithul-Qudusiy* aliyoipokea Imamu as-Sadiq (as) amesema: “Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ‘Viumbe ni waja wangu, anayependeza zaidi kwangu ni mpole wao na mwenye kuwasaidia katika haja zao.’”[83] Na kutoka kwake (as): “Hakika mmoja wenu asimkosee yeyote kati ya waja wangu kwani hajui nani kati yao ni walii wa Mwenyezi Mungu.”[84]

Na kutoka kwake (s.a.w.w.): “Viumbe ni waja wa Mwenyezi Mungu anayependeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu ni yule mwenye kuwafanyia wema waja wake.”[85] Kwa sababu hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na Maimamu waongofu (as) walikuwa wanajali sana kuonyesha heshima ya daraja la juu na adabu kwa watu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa anawatolea salamu hata watoto wadogo, anawatembelea wagonjwa na anasindikiza jeneza, anawaulizia wasiokuwepo kati ya Masahaba wake na anaitikia wito wao.

[83] *Al-Kaafiy*, Juz. 2, uk. 199
[84] *Biharul-Anwaar*, Juz. 72, uk. 147
[85] *Kanzul-Umaal,* Hadith ya 16171

Imepokewa kwamba Nabii wa Mwenyezi Mungu Isa bin Mariyam (as) alisema: "Enyi wafuasi wangu, nina haja kwenu nitimizieni. Wakasema: 'Haja yako imeshatimizwa ewe roho ya Mwenyezi Mungu.'Akasimama akaosha miguu yao. Wakasema: 'Sisi ndio tunastahili zaidi kukufanyia haya ewe roho wa Mwenyezi Mungu.' Akasema: Hakika mwenye kustahili zaidi kuwatumikia watu ni mwanachuoni, hakika nimefanya unyenyekevu huu ili muwe wanyenyekevu kwa watu baada yangu kama unyenyekevu wangu huu kwenu."[86]

Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa anachukia kupata raha ya kuwatumikisha Masahaba wake bali alikuwa anashirikiana nao katika kazi na katika kuhudumia. Kama vile kufanya kazi pamoja nao katika kujenga Msikiti wa Madina. Asiyad bin Hadhir alipomuona anabeba jiwe katika tumbo lake akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nipe nikubebee."Akasema (s.a.w.w.): "Hapana nenda ukabebe jingine."[87]

Na njiani wakati wa kwenda Badri Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), Ali bin Abu Talib na Murthad bin Abi Murthad walikuwa wanapokezana ngamia mmoja, mmoja kati yao anampanda kwa muda kisha anamwachia mwingine, ndipo Murthad na Ali wakataka kumwachia hisa zao za kupanda ngamia na wakasema: "Sisi tutatembea kwa miguu badala yako." Akawaambia: "Nyinyi hamna nguvu za kutembea kunishinda mimi wala mimi sijatosheka na malipo kuliko nyinyi." Akakataa isipokuwa hisa yake ya kupanda ngamia kama mmoja kati yao. Na katika kuchimba handaki alikuwa (s.a.w.w.) anapiga kwa nyundo na anabeba udongo juu ya mgongo wake kama Waislamu wengine.

Imepokewa katika sira ya Imamu Ali (as) kwamba yeye alipokuwa mtawala katika nchi ya Kiislamu na Amirul-Muumini na wao,

[86] *Biharul-Anuwaar*, Juz. 2, uk: 62
[87] *Biharul-Anwaar*, Juz. 19, uk. 112

alikuja kwake baba na mtoto wake, akasimama na akawakirimu na akawakalisha mbele ya majilisi yake, naye akakaa mbele yao kisha akaagiza chakula akamkaribisha kila mmoja kati yao. Kisha akaja Qambar na beseni, birika, ubao na kitambaa cha kukaushia mikono. Alipotaka kummiminia maji mwanaume, Amirul-Muuminina (as) akasimama akachukua birika ili ammiminie mwanaume juu ya mikono yake. Amirul-Muuminina (as) akasimamana akachukua birika ili ammiminie. Imamu akasema: "Kaa na nawa mikono, hakika Mwenyezi Mungu anakuona na ndugu yako ambaye hajitofautishi na wewe wala hajifadhilishi kwako, anakuhudumia, katika kukuhudumia kwako anataka pepo mfano wa mara dufu ya watu wa duniani na mfano wa hesabu hiyo ya watumishi wake humo."

Mwanaume akakaa Imamu Ali (as) akamwambia: "Nimeapa kwa utukufu wa haki yangu ambayo umeshaijua, naomba unawe hali ya kuwa na matumaini kama ambavyo ungenawa kama angekumiminia Qambar." Mwanaume akafanya hivyo, alipomaliza akampa birika mtoto wake Muhammad bin Hanafiya na akasema: "Ewe mtoto wangu kama huyu mtoto angenijia bila ya baba yake ningemmiminia katika mikono yake, lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu anakataa kulinganisha baina ya mtoto na baba yake unapowakusanya sehemu moja. Lakini baba amemmiminia baba na mtoto ammiminie mtoto."[88]

Na Ali (as) alikuwa anatembea sokoni peke yake anamuongoza aliyepotea, anamsaidia mnyonge na pengine alimbebea mzigo wake, na pengine alikaa katika duka la rafiki yake Maytham Tammaar na kuuza tende pamoja naye.

Imamu as-Sadiq anamzungumzia babu yake Imamu Ali bin Husain (as), anasema: "Ali bin Husain alikuwa hasafiri isipokuwa kwa kufuatana na watu wasiomjua, na alikuwa anaweka sharti kwao

---

[88] Sayyid Haadiy al-Mudarrisiy katika *Akhlaqiyaati Amirul-Muuminina (as)* chapa ya kwanza 1411Hijiria (Beirut, Muasasatu al-ilamiy ya uchapishaji) uk. 116

kwamba yeye awe ni kati ya watumishi wa wasafiri katika mahitaji yao. Wakati mmoja alisafiri pamoja na watu, mtu mmoja akamuona na akamjua, akawaambia: 'Mnajua huyu ni nani?' Wakasema: 'Hapana.' Akasema: 'Huyu ni Ali bin Husain.' Wakamrukia wakimbusu huku wanamtaka radhi kwa kusema: 'Nini kimekupelekea kufanya haya?' Akasema: 'Hakika mimi nilisafiri mara moja pamoja na watu wanaonijua, wakanipa kwa ajili ya Mtume wa Mwenyezi Mungu nisiyoyasitahiki, hivyo naogopa nyinyi kunipa mfano wa hayo. Hivyo ikawa kuficha jambo langu kunapendeza zaidi kwangu.'''[89]

Na vivyo hivyo ni wajibu mwanachuoni wa dini awe ni mwenye kujali heshima ya watu, kwa kwenda mbio katika kuwahudumia. Mwenye mahusiano pamoja nao, hakubali kuwatumikisha wao kwa mambo yake binafsi wala hapati raha ya kuwatumikisha wao, bali anashirikiana pamoja nao katika kazi na huduma. Ama kusema kwamba mwanchuoni ni kama Kaaba anatembelewa na wala hatembelei, na anatumikiwa na wala hatumikii, hiyo ni sera inayakhalifu sira ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na Maimamu waongofu (as), na ambayo inapingwa na Hadithi na nususi za kidini.

**Ushauri na kuheshimu rai:**

Mwanachuoni wa kidini hata awe na maarifa kiasi gani, hata awe ni bingwa kiasi gani, bado ataendelea kuhitaji rai za wenye ujuzi na uzoefu miongoni mwa watu katika sekta mbalimbali, kwani yeye anajua hukumu za kisharia, lakini kuainisha maudhui na sehemu za utekelezaji na kujua nyakati na mbinu za harakati na kazi, yote hayo atayapata kupitia ushauri wa wengine na katika kufaidika na rai zao. Hakika ukandamizaji wa rai na ukiritimba wa maamuzi na mawazo katika mambo yanayohusiana na ummah na maslahi ya watu, na katika mambo ya kidini na kijamii, ni njia ya kimakosa.

[89] *Wasailu Shi'ah,* Hadith ya 15177

Watu wana akili na wana uzoefu na ujuzi. Ushauri unamaanisha kunufaika kutokana na uwezo wao, vilevile unawawezesha kushirikiana katika kubeba jukumu na kuwafanya wawe ni wenye nguvu na ushirikiano zaidi. Kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu anamwamrisha Nabii wake Muhammad (s.a.w.w.) pamoja na utukufu wake na nafasi yake awashauri waliokaribu naye, anasema (swt):

وَشَاوِرْهُمْ فِي الْأَمْرِ ۖ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِينَ ﴿١٥٩﴾

**"Na ushauriane nao katika mambo. Utakapoazimia, basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wamtegemeao." (Surat al-Imraan: 159)**.

Na imepokewa kwamba (s.a.w.w.) alikuwa mwingi wa kuwashauri Masahaba wake. Na Imamu as-Sadiq (as) wakati mmoja alimtaka ushauri mfuasi wake, ndipo mfuasi wake akasema: "Mwenyezi Mungu akutengenezee mambo yako, hivi kweli mtu mfano wangu anaweza kumpa ushauri mtu mfano wako?" Imamu (as) akamjibu:"Ndio, utakapotakiwa ushauri."[90]

Na anasimulia Imamu Ali Ridhaa (as) kutoka kwa baba yake Musa al-Kaadhim (as), anasema: "Akili yake ilikuwa hailinganishwi na akili yeyote, lakini kuna wakati alikuwa anamtaka ushauri mtu mweusi pamoja na weusi wake. Akaambiwa: 'Unamtaka ushauri mtu kama huyu?' Akasema: 'Akitaka Mwenyezi Mungu aliyetukuka, kwani pengine ameufungua ulimi wake."[91]

[90] *Biharul-Anwaar,* Juz. 72, uk. 101

[91] Rejea iliyotangulia

# ZAKA YA ELIMU

**Zaka kilugha:** Ni ongezeko na ziada. Inasemwa *Zakaa Zar'u*: mazao yanapostawi na kuongezeka, na *Zakat Nafaqat*: Mtu anapobarikiwa. Na pia hutumika kwa maana ya utakaso, amesema (swt):

قَدْ أَفْلَحَ مَن زَكَّىٰهَا ﴿٩﴾

**"Hakika amefaulu aliyeitakasa."** **(ash-Shamsi: 9)**.

Imekuja katika kamusi ya Kiarabu *Lisanul-Arab*: "Na asili ya Zakaat katika lugha: Ni kujitakasa, kuongezeka na baraka. Na katika Hadith ya Imamu al-Baqir (as) ni kwamba amesema: 'Zaka ya ardhi ni kukauka kwake.' Akikusudia kutakasika kwake kutokana na najisi kama vile mkojo na mfano wake, kwa kukauka na kuondoka athari zake."[92]

Na kutokana na falsafa ya Zaka katika sharia ya Kiislamu inadhihirika kwamba maana mbili zimechukuliwa kwa mazingatio, kutoa Zaka ya mali kunatwaharisha nafsi ya mwanadamu kutokana na ubinafsi, ubakhili na uroho kwa mwanadamu, uroho ambao humfanya ahisi kwamba mali ambayo anaipata ni miliki yake peke yake na iko chini ya umiliki wake na kwa ajili ya matumizi yake tu, na kutoa kwake Zaka ni kusawazisha na kurekebisha hisia na mawazo haya, na kwa sababu hiyo anasema (swt):

خُذْ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِم بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ ۖ إِنَّ صَلَوٰتَكَ سَكَنٌ لَّهُمْ ۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٠٣﴾

**"Chukua sadaka katika mali zao uwasafishe na uwatakase kwayo. Na uwaombee rehema. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Msikizi, Mjuzi."** **(at-Tawba: 103)**.

---

[92] *Lisanul-Arab*, Juz. 3 uk. 36

Na wakati huo huo hakika kutoa Zaka kunaongeza mali na kuizidishia baraka za Mwenyezi Mungu na fadhila zake, na hata katika wigo wa mtazamo wa kijamii na kiuchumi, kwani kuwaangalia mafakiri kunaleta amani ya kijamii ambapo kunazuia kutokea hali ya uovu, uhalifu na uadui unaotokana na ufakiri na kukosa, kama ambavyo kueneza utajiri katika jamii kunaharakisha na kukuza hali ya kiuchumi na matokeo yake yatawarudia wenye rasilimali pia. Na kuanzia hapa ndipo tunaona nchi kubwa zinatoa kiasi cha msaada kuunga mkono juhudi za nchi fakiri zisizoendelea ambapo zitakapoendelea uchumi wake utatumika katika uzalishaji wa nchi zilizoendelea.

Nususi za kidini zinaashiria nafasi ya Zaka na sadaka katika kuleta ustawi wa mali na pato kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Ukitaka Mwenyezi Mungu aongeze mali yako basi itolee Zaka."[93] Na kauli ya Imamu al-Baqir (as): "Zaka inaongeza riziki."[94]

**Kila kitu kina Zaka:**

Si tu utajiri wa mali anayoimiliki mwanadamu ndio unamfanya ahisi ubinafsi na ubakhili, bali kila uwezo anaoupata mwanadamu unamsababishia hisia hizi, na unaandamana naye katika nafsi yake na mwendo wake, na kwa hiyo ana haja ya kuongoza hisia zake na nyendo zake katika kila kinachopatikana kwake miongoni mwa uwezo na chumo katika maisha haya, ili katika kutumia kwake uwezo huo aelekee katika kutumikia maslahi ya jamii.

Hapa nususi za kidini zinaashiria kwamba kila kitu kina Zaka, kama ambavyo ni wajibu mwanadamu kutoa hisa yake ya mali kulingana na udhibiti wa kisharia kwa maslahi ya mafakiri na huduma za jamii, hivyo ni wajibu wake atoe chochote katika uwezo wake na

[93] *Biharul-Anwaar*, Juz. 93, uk. 23
[94] Biharul-Anuwaar, Juz. 93, uk. 14

juhudi zake mbalimbali kwa maslahi ya jamii na kuhudumia watu wa jinsia yake na jamii yake. Anasema Imamu Ali (as): "Kila kitu kina Zaka."[95]

Na elimu na maarifa ni kati ya uwezo mkubwa na chumo muhuimu, na mwanadamu anapopata kiwango na uwezo wa kielimu anaweza kupatwa na ghururi na kujikweza kwa wanaomzunguka, na kutawaliwa na ubinafsi na kuzuia elimu na maarifa kwa ajili ya nafsi yake tu na kufanya ubakhili wa kutowanufaisha wengine kwa elimu hiyo isipokuwa katika mpaka wa kutumikia dhati yake na maslahi yake. Na kwa sababu hiyo yamekuja mafunzo ya kidini yakitilia mkazo juu ya wajibu wa mwanachuoni kuwatumikia watu, na yanawajibisha kwake kutoa elimu yake kwa wanaoihitaji na wanaonufaika nayo. Na kutoa elimu ndio Zaka yake. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwamba amesema: "Zaka ya elimu ni kumfundisha asiyeijua."[96]

Na kutoka kwa Imamu Ali (as): "Zaka ya elimu ni kuitoa kwa anayestahiki."[97]Hakika kutoa elimu kwa watu kunatakasa nafsi na kuitwaharisha kutokana na ubinafsi na ubakhili, na kunaimarisha hali ya kuhisi majukumu na wajibu, hivyo elimu sio utukufu tu, bali ni majukumu, wajibu na taklifu. Na katika upande mwingine, hakika kutoa elimu kunaiongeza na kuistawisha kama anavyosema Imamu Ali (as): "Na elimu inakua kwa kuitoa."[98] Yaani inaongezeka na kustawi. Hiyo ni kwa sababu kutoa maalumati kunayaimarisha katika kumbukumbu ya mwanadamu, kwani fikra au maalumati ambayo yanatolewa mara nyingi, yanakuwa tayari kwa wingi katika akili yake na hujiweka mbali na usahaulifu na mghafiliko.

[95] *Ghurarul-Hikami wa Durarul-Kalimi* herufi ya Laam
[96] Rejea iliyotangulia, Juz. 2 uk. 25
[97] *Ghurarul-Hikami wa Durarul-Kalimi* hefufi ya Zaa
[98] *Nahjul-Balaghah*

Kutoa fikra na rai mbele ya wengine kunatoa fursa na nafasi ya kupembua na kuikosoa na kuijadili. Mwanadamu anaweza akajifungia katika mtazamo fulani akiitakidi usahihi wake na kupatia kwake, lakini anapoitoa fikra katika mzunguko wa kielimu baina ya watu hakika anaweza kuamsha maswali, kukubaliwa na kukataliwa, jambo ambalo humfanya mwenye fikra husika kuiangalia na kuipitia upya kwa kuondoa kasoro na nukta za udhaifu katika nadharia husika, ambapo anaipa nguvu na kuifanya iwe ya kina zaidi, au kuiacha kama atagundua ubatili wake. Na hilo ni chumo muhimu na faida kubwa ambayo haipatikani kwa mwanachuoni anayejifungia na elimu yake, bali ni kwa anayeitoa elimu na kuisambaza.

Na katika upande mwingine, hakika kuitoa elimu kunachangamsha harakati za kifikra na kielimu katika jamii, na hivyo ni maslahi ya mwanachuoni mwenyewe, ambapo hakika kujiunga kwake na jamii hai yenye harakati na maarifa kunaongeza uchangamfu wake wa kielimu, na kunamsukuma zaidi katika harakati na maendeleo. Kwa yote hayo kutoa elimu kutakuwa ni Zaka yake, yaani ni sababu ya kuongezeka elimu yake na kubarikiwa kwake.

**Kutoa elimu:**

Hakika mwanadamu huelekea katika kujifunza elimu ya dini na maarifa ya kisharia kwa ajili ya kumiliki uoni katikadini yake kwanza. Pili, ilikujua taklifu inayoelekezwa kwake ili afanye kazi ya kuwaongoza wengine na kuwaelekeza, anasema (swt):

۞ وَمَا كَانَ ٱلْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُوا۟ كَآفَّةً ۚ فَلَوْلَا نَفَرَ مِن كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَآئِفَةٌ
لِّيَتَفَقَّهُوا۟ فِى ٱلدِّينِ وَلِيُنذِرُوا۟ قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوٓا۟ إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ ﴿١٢٢﴾

**"Wala haiwafalii waumini kutoka wote. Kwa nini kisitoke kikundi katika kila kundi miongoni mwao kujifunza dini nakuwaonya watu wao watakapowarudia, ili wapate kujihadhari."** **(Surat Tawba: 122)**.

Na jukumu la pili linafuatia kwa namna ya kawaida na ya lazima katika kufanikisha jukumu la kwanza, kwani mara tu mwanadamu anapopata elimu na maarifa huwa ana jukumu la kuwafundisha wengine na kuwafahamisha, hata kama hakuwa na lengo hilo tangu mwanzo.

Kwa hakika kuna nususi zinazozungumzia jukumu na wajibu alionao mtu mbele ya elimu kwa namna ya jumla, yaani kila elimu wanayoihitajia watu na wanayonufaika kwayo katika mambo ya dini yao au dunia yao. Imepokewa kutoka kwa Imamu Musa al-Kadhim (as): "Kati ya haki za wajibu kwa ndugu yako ni kutomficha chochote kinachomfaa katika dunia yake na Akhera yake."[99] Imekuja katika Hadith kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Mambo matatu ni kati ya ukweli wa kiimani…, na kutoa elimu kwa mwenye kujifunza."[100] Na utoaji wa elimu una njia nyingi, na zilizomuhimu zaidi ni: Kufundisha, kuandika na hotuba. Tutaangazia kwa haraka juu ya njia hizi tatu ambazo wamezifuata maulamaa katika kueneza elimu yao katika jamii za kibinadamu.

**Kufundisha na kujifunza:**

Ni njia ya kurithishana elimu baina ya vizazi na kuhama kwa ujuzi na maarifa, ambapo mwanachuoni anajibidiisha kufundisha kundi la wanaopenda kujifunza elimu na anadumu katika kuwafundisha kwa kuwafunza ndani ya silabasi na mitaala maalumu inayotofautiana baina ya muda na muda mwingine.

Na kufundisha kwa kuwajibika kunachukua juhudi ya mwanachuoni na wakati wake. Nayo ni kati mifano halisi ya kutoa elimu na ni udhihirisho wa kubeba jukumu lake. Na kwa ajili hiyo Imamu Ja'far as-Sadiq (as) anahadharisha kutopuuza katika kutekeleza

[99] Muhammad Ridhaa na Muhammad Ali al-Hakimiy katika *al-Hayaatu*, Juz. 2 uk. 338 chapa ya sita ya 1410 (Beirut – Darul- Isamiyati)

[100] *Biharul-Anwaar*, Juz. 2 uk: 15

wajibu huu ambapo anasema katika hadithi iliyopokewa kutoka kwake: "Hakika miongoni mwa maulamaa kuna anayependa kulimbikiza elimu yake na wala haichukuliwi kutoka kwake, huyo atakuwakatika tabaka la chini kabisa la moto."[101]

Na ambalo tunapenda kuashiria hapa ni dharura ya kupanuka njia za kufundishia elimu kwa wasiokuwa wanafunzi rasmi. Katika jamii yetu kuna kundi la wasomi wanaojali mambo ya kifikra na kijamii lakini maarifa yao katika elimu ya dini ni madogo. Na ni kana kwamba maarifa na elimu ya dini ni maalum kwa wanafunzi wa Seminari za Kidini, na hii ni sababu ya utengano baina ya wasomi wa sekyula na wasomi wa dini. Hivyo inapasa kutoa nafasi na kufungua medani, na maulamaa watukufu wajitolee kusomesha masomo ya Tafsiri, Aqaid, Fiqhi, Usul na mengineyo kwa kundi hili la vijana hata kama ni katika baadhi ya siku za wiki, ili tuwe na tabaka la wasomi wenye kujua misingi ya Uislamu wao, dhana zake na sharia yake.

**Kuandika na kutunga:**

Kwa sababu Uislamu ni harakati za kimaendeleo, dini ya elimu na maarifa, basi umetoa kipaumbele katika njia za elimu na vyombo vya kuelimishia. Umezipa umuhimu mkubwa njia na vyombo vya kuelimishia, na kwa hiyo Qur'aniTukufu imesifia njia na vyombo hivyo kuvifanya ni anwani ya sura kati ya sura zake, nayo ni Surat al-Qalam, ambayo Mwenyezi Mungu ameapa katika mwanzo wake kwa kalamu na maandiko:

نٓ ۚ وَٱلْقَلَمِ وَمَا يَسْطُرُونَ ﴿١﴾

**"Nun. Naapa kwa kalamu na yale wanayoandika!"** **(Surat al-Qalam: 1)**.

Kama ambavyo aya za mwanzo za Qur'ani kushuka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) zilikuwa ni wito wa kusoma na ku-

[101] *Biharul-Anwaar*, Juz. 2, uk: 108

kumbusha juu ya neema ya kalamu na nafasi yake katika kumfundisha mwanadamu, ikiwa ni neema kubwa kwa mwanadamu baada ya neema ya kuumbwa kwake na kupatikana kwake, anasema (swt):

ٱقۡرَأۡ بِٱسۡمِ رَبِّكَ ٱلَّذِي خَلَقَ ۝١ خَلَقَ ٱلۡإِنسَٰنَ مِنۡ عَلَقٍ ۝٢ ٱقۡرَأۡ وَرَبُّكَ ٱلۡأَكۡرَمُ ۝٣ ٱلَّذِي عَلَّمَ بِٱلۡقَلَمِ ۝٤ عَلَّمَ ٱلۡإِنسَٰنَ مَا لَمۡ يَعۡلَمۡ ۝٥

**"Soma kwa jina la Mola Wako aliyeumba. Amemuumba mtu kwa pande la damu. Soma! Na Mola Wako ni Karimu zaidi! Ambaye amefundisha kwa kalamu. Amemfundisha mtu aliyokuwa hayajui."**
**(Surat al-Alaq: 1-5)**.

Na kalamu kama neema nyingine, inahitaji kuzalishwa na kufanyiwa kazi kwani wengi kati ya wanaomiliki uwezo na utayari wa kuandika na kutunga, wanaweza wasifasiri kivitendo nguvu hizo kabisa katika maisha yao, na kutoitoa silaha ya kalamu katika kutetea misingi yao na njia ya kuhifadhi fikra zao na uzoefu wao na kuunukuu kwa wengine. Pamoja na kwamba Uislamu katika mafunzo yake unatia mkazo juu ya kila aliyepewa sehemu ya elimu aihifadhi kwa kuiandika kwa ajili ya nafsi yake na kwa ajili ya vizazi vinavyokuja. Imepokewa katika Hadith kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwamba amesema: "Idhibitini elimu kwa kuiandika."[102]

Na zaidi ya hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amezingatia kwamba nafasi ya kuandika na kutunga ni muhimu zaidi na ni bora zaidi kuliko nafasi ya kupigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu hadi kufa shahidi, ambapo imepokewa kutoka kwake (s.a.w.w.) kuwa amesema: "Siku ya Kiyama utapimwa wino (elimu) ya wanachuoni na damu ya mashahid basi wino (elimu) wa wanachuoni, nao utazidi (uzito) damu ya mashahidi."[103]

[102] *Kanzul-Umaal*, Juz. 10, uk. 249 Hadith ya 29332
[103] Rejea iliyotangua Juzuu 10, uk. 173 Hadith ya 28902

Kwa kuanzia na maelezo haya ya Kiislamu na kwa kufahamu umuhimu wa nafasi ya kalamu katika kueneza elimu na kusambaza maarifa kwa kujitolea, maulamaa wetu watukufu walibeba majukumu yao ya kimsingi katika nyanja hii na wakaathiri harakati za kifikra za kibinadamu kwa uzalishaji wao mkubwa wa kielimu katika nyanja mbalimbali za maarifa na maisha.

Pamoja na kwamba baadhi yao walikuwa wanaishi katika nyakati ngumu mno na walikuwa wanakabiliwa na ugumu na vikwazo, isipokuwa malengo makubwa na moyo wa kujitolea na kutoa, tabia ya kusubiri na juhudi, yote hayo yalisaidia kuvuka changamoto na vikwazo hivyo. Kuandika na kutunga ni wajibu ambao unapasa uwe ni sehemu ya ratiba ya maisha ya mwanachuoni, sambamba na majukumu mengine na mahitaji yake, na haipasi kutoa udhuru kwa shughuli mbalimbali zenye kuzuia jukumu hili muhimu.

Na katika zama hizi wakati mwanadamu anaishi katika utajiri wa maalumati na mawasiliano, utandawazi wa maarifa na matangazo, hakika ummah wa Kiislamu unakabiliwa na changamoto kubwa katika kuhifadhi heshima yake na kushikamana na asili yake na kuendana na mabadiliko ya maisha, na kujua mtazamo wa kidini kuhusu matatizo magumu ya kijamii, jambo ambalo linahitaji harakati kubwa za kielimu na kiutamaduni.

Na ikiwa maulamaa waliotangulia walikuwa wameandika juu ya mambo na mas'ala yaliyowasilishwa na yaliyoenezwa katika zama zao, hakika maulamaa wetu wa leo wanatakiwa kujielekeza katika kutatua matatizo ya maisha ya kileo.

Hakuna shaka kwamba mazingira ya utafiti na kuandika, na nyakati za kutunga na kuchapisha, sasa hivi yameandaliwa na yametayarishwa vizuri na rahisi kuliko zama zilizopita, ambapo inamaanisha utoaji wa fikra na uzalishaji wa elimu ni mwingi zaidi na mpana zaidi kwa maulamaa na wanafikra wa zama hizi.

**Hotuba:**

Ikiwa kufundisha na kutunga kunaelekea kwa kundi dogo katika jamii, basi hotuba ni daraja la mawasiliano kati ya mtu na jamhuri na watu wa kawaida. Kama walivyokuwa Manabii na Mitume wanafikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa watu wote kwa njia hiyo, hakika maulamaa wa kidini na wao ni warithi wa Manabii na wabeba ujumbe wao, ni lazima wazungumze na watu wote. Na Uislamu umefaradhisha hotuba ya watu wengi kuwa ni sehemu ya Swala katika Swala ya Ijumaa na Iddi mbili.

Na hotuba ya wazi inatakiwa iwe nyepesi na katika kiwango maalumu na kwa istilahi maalumu ya kielimu, kwani hiyo sio kama somo au maandishi. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) naye ni mjuzi zaidi, alikuwa anawahutubia Waarabu pamoja na kutofautiana nasaba zao na mataifa yao, na kutofautiana koo zao na makabila yao, lakini alikuwa anawahutubia wote yale wanayoyafahamu, na anazungumza nao yale wanayoyajua, na kwa ajili hiyo amesema: “Nimeamrishwa kuwahutubia watu kwa kadiri ya akili zao.”[104]Na amepokea Abu Daud katika *Sunan* yake Hadith namba 4839 kwamba “Maneno ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) yalikuwa wazi anayafahamu kila anayeyasikia.”[105]

Na miongoni mwa makosa yaliyoenea katika baadhi ya mazingira ya kielimu nikuona nafasi ya hotuba ya wazi haioani na nafasi ya elimu ya juu, na kwamba hotuba ni kazi ya kuajiriwa inayofanywa na kundi maalum la wenye kiwango duni cha elimu, ama maulamaa wakubwa kufanya hivyo hakunasibiani na hadhi yao na mambo yao!

Amezungumza Shahid Sayyid Mahdiy al-Hakiimu katika kumbukumbu yake kwamba, alipoanza kutoa muhadhara wa wazi

[104] Muhammad bin Yusuf Swaalihiy Shaamiy katika *Subulul-Hudaa wa Rashaad*, Juz. 2, uk. 94

[105] *Subulul-Hudaa wa Rashaad*, Juz. 7, uk. 129

walikuja baadhi ya maulamaa kwa mzazi wake MarjaaSayyid al-Hakiim ili wamsihi aache kufanya hivyo, kwa sababu kutoa muhadhara na hotuba ya wazi hakulandani na hadhi yake na nafasi yake!

Hakika katika historia yetu kuna maulamaa mashujaa waliotoa waadhi na mwongozo kwa jamhuri, na jambo hilo lilikuwa na athari kubwa katika jamii zao, kama vile Sheikh Ja'far Shushtariy aliyefariki mwaka 1303 Hijiria, ambaye Sayyid Amini anasema kuhusu yeye: "Alikuwa mwanachuoni kati ya wanachuoni wajuzi, faqihi, mtoa waadhi na mashuhuri sana. Na alikuwa mashuhuri kwa waadhi na hotuba, na maelfu walikuwawanakusanyika mbele ya mimbari yake ili kusikiliza mawaidha yake. Alirejea katika mji wake Tasatar huko Iran, akawa ni kiongozi mwenye kutiiwa na Marjaa wa taqlid na hukumu. Akawa anatoa waadhi katika mwezi wa Ramadhani na miezi mingine, na akawa mashuhuri katika hilo ambapo hapakuwa na mfano wake. Na ikapatikana athari nzuri, na kukapatikana katika mawaidha yake kuongoka kwa watu wengi."[106]

Vivyo hivyo kupitia katika njia hii na chaneli, kupitia kufundisha, kutunga na kutoa hotuba, mwanachuoni anatekeleza jukumu lake katika kutumikia dini na ummah anafanya kazi ya kusambaza elimu na maarifa, na kwa hilo anatoa Zaka ya elimu yake. Na katika zama hizi na ambapo ummah unashambuliwa na mawimbi ya changamoto na unakabiliwa na matatizo na hatari chungu nzima, hakika inapasa kutangaza hali ya hatari katika maisha ya maulamaa wa kidini kwa kuongeza juhudi zao na kuzidisha harakati zao za kielimu, kiutamaduni na kijamii, hadi ummah uvuke hali ya hatari iliyotuvamia.

---

[106] Sayyid Muhsinal-Amin katika *A'ayaan Shiati*, chapa ya 1406 Hijiria (Beirut – Daru taawun) uk: 95

# JAMII NA MAULAMAA WA KIDINI

Yanapimwa maendeleo ya jamii katika nyanja yoyote ile kupitia kiwango cha idadi ya wabobezi na wenye kujishughulisha nayo. Kila inapoongezeka idadi ya matabibu basi hiyo inakuwa ni dalili ya kuongezeka kiwango cha maendeleo ya tiba na afya katika jamii. Vilevile hakika wingi wa wanafasihi unatoa habari ya kuongezeka kiwango cha fasihi, na vivyo hivyo katika nyanja nyingine.

Kwa sababu uhusiano uliopo ni baina ya mambo mawili, kama si kuwepo hali ya kuijali nyanja hiyo basi isingeelekea huko idadi kubwa kati ya wanajamii, kama ambavyo wingi wa wenye kuelekea kwenye nyanja yoyote ile unaimarisha hali ya kuijali na kupanua wigo wake. Na kwa msingi huu inatuwezesha kuzingatia kwamba kiwango cha idadi ya maulamaa wa kidini katika nchi moja ni moja ya vipimo muhimu vya kujua hali ya kidini katika jamii, kwa sababu inadhihirisha kiwango cha watu kujali dini na jinsi dini ilivyojikita na kuota mizizi ndani ya jamii yao.

Na nchi yetu, kabla ya miongo mitatu, takriban sehemu ya Mashariki ilikuwa inakabiliwa na uchache wa maulamaa wa kidini na udhaifu wa kwenda kusoma masomo ya kidini, miji mingi na vijiji havikuwa na mwanachuoni wa kidini hata mmoja, bali maulamaa wa kidini walikuwa wanahesabiwa kwa vidole katika nchi hii. Nakumbuka kwamba baadhi ya maulamaa huko al-Hufuf au al-Mubaraz walikuwa wanatenga usiku mmoja katika wiki kwa ajili ya kijiji hiki au kile, na katika baadhi ya nyakati usiku mmoja katika kila wiki mbili.

Na Qatif baadhi ya Maulamaa kama Sheikh Faraj al–Imraan na Sheikh Abdul-Hamid al-Khatwiy, Mwenyezi Mungu awarehemu, walikuwa wanafanya mzunguko wa kila mwaka katika baadhi ya vi-

jiji na kukaa katika kila kijiji siku kadhaa ili kujaza pengo la maelekezo ya kidini ambayo vijiji vinayahitajia. Lakini kwa mwamko mtukufu wa kidini ambao umetokea, ambao upepo wake umevuma katika ulimwengu wetu wa Kiislam, na baraka zake zimeijumuisha sehemu yetu, idadi kubwa imejitokeza ya watoto wa sehemu hii na vijana wake kwenda kusoma elimu ya dini ndani ya nchi yao, na kwa kuhamia katika sehemu zenye Seminari za Masomo ya dini. – Alhamdulillahi nchi yetu imejaa idadi nzuri ya maulamaa na wanafunzi wenye kujifunza elimu ya dini, na katika kila mji au kijiji kuna kundi miongoni mwao.

**Nafasi inayotarajiwa:**

Hakika jamii yetu leo ina haja sana ya kuhamasisha nafasi ya maulamaa na wanafunzi wa elimu ya dini, ambapo tunakabiliwa na tufani ya matangazo, habari na utamaduni unaotushambulia kutoka katika tamaduni za kimagharibi za kimaada, ambazo zinabeba dhana potofuna kusambaza maadili na tabia zinazokhalifu maadili yetu ya Kiislamu na mafunzo yetu ya kidini. Jambo ambalo linahitaji harakati za kimaarifa nyingi na juhudi za kiutamaduni kubwa kwa ajili ya kuhifadhi heshima na kuhifadhi maadili.

Hakika mabadiliko yanayokuja katika elimu na teknolojia yanachochea maswali mengi ya kiitikadi, kiutamaduni na kimaadili kwa vijana wetu, hivyo ni lazima maulamaa wenye kujua dini na wenye kuelewa matatizo ya maisha, kujitokeza ili kujibu maswali haya na changamaoto hizi. Na kizazi hiki kipya cha vijana wa kiume na wa kike ambao inawezekana hayapatikani kwao maelekezo ya kidini yanayotakiwa ndani ya familia, kwa sababu ya shughuli za wazazi na wingi wa majukumu yao au ufinyu wa kiwango chao, hakika kuna haja ya kuelimisha na kufundisha maadili ya kidini na hukumu zake, vinginevyo watakabiliwa na upotovu na ufisadi kama yanavyotokea hayo hasa katika sehemu kubwa katika kizazi hiki.

Na katika jamii kuna matatizo na mambo yanahitaji kukabiliana nayo na kutatuliwa. Na ni upande wa dini ndio wenye uwezo zaidi wakubeba majukumu haya ya utatuzi, na ndio wenye nafasi kubwa zaidi ya kuleta ufumbuzi, hiyo ni kutokana na uelewa, ikhilasi, ushawishi na nguvu iliyonayo dini. Nafasi inayotarajiwa katika mazingira ya kidini ni kusambaza maarifa ya Kiislamu na kuandaa maelekezo, na kulea kizazi kinachokua na kukabiliana na matatizo ya jamii na mambo yake.

**Wajibu wa jamii:**

Baadhi ya watu pindi wanapoona uwepo wa idadi kadhaa ya wenye kujihusisha na elimu ya dini na wenye kufuata njia ya kutafuta elimu ya dini, ambao wamejikita katika vazi lao maalum na nguo zao za kipekee, hujiuliza ni upi mchango wa maulamaa na wanafunzi hawa wa dini? Na hatimaye huvuka mipaka katika kuwabebesha majukumu na katika kukuza matarajio wanayoyasubiria kutoka kwao. Pamoja na kukubali wajibu wanaoubeba watu wa kundi hili la kidini miongoni mwa kazi na majukumu yanayojitokeza, lakini jambo ambalo wanasahau kulizungumzia ni kukumbusha wajibu wa jamii mbele ya maulamaa na wanafunzi.

Mwanafunzi wa elimu ya dini, ni mwanadamu aliyejitolea katika kuitumikia elimu na dini, na hivyo anahatarisha mustakabali wa maisha yake ambapo hakuna kazi ya uhakika wala pato la kimali thabiti na la kudumu analolitegemea. Wala hakuna taasisi rasmi anayojiunga nayo, naye anavumilia ugeni na kuhama kwa ajili ya kutafuta elimu. Na anakabiliana na changamoto mbalimbali, naye ni mwenye jukumu la kuihudumia familia yake, jambo ambalo linamfanya ahitajie sana kuungwa mkono na msaada kwa ajili ya kupata mahitaji yake ya kimaisha ili aishi kama watu wengine katika jamii yake, katika kiwango cha hali ya kati, na katika upande wa kutekeleza majukumu yake ya kidini na ya kijamii. Anahitaji misimamo ya kutia

moyo na kumsaidia ili aweze kufanya wajibu wake wa kulingania na wa tablighi. Kuna haki za kupeana na wajibu wa kubadilishana baina ya maulamaa na wanafunzi kwa upande mmoja, na jamii kwa upande mwingine.

Na sio sahihi maulamaa kutaka heshima na msaada kwa jamii bila ya wao kufanya wajibu wao wa kutoa elimu na kusambaza maarifa na kujali mambo ya jamii. Kama ambavyo haisihi kwa jamii kutarajia kutoka kwa maulamaa majukumu na kazi yote hiyo bila ya kusimama karibu yao na kutoa kwao wanayoyahitaji miongoni mwa misaada na kuwaunga mkono.

**Kujitolea kwa Mwanachuoni:**

Mwanachuoni wa elimu ya dini huwa amejipamba na maarifa ya Kiislamu na amekusanya kiasi fulani cha elimu na mafunzo yake na ameishi karibu na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah ya Mtume Wake (s.a.w.w.) na sira ya Maimamu waongofu (as). Na amekuwa karibu na maisha ya maulamaa wema ambao amejifunza katika mikono yao au amesikia na kusoma juhudi zao na kujitolea kwao. Baada ya yote haya, inatakiwa awe ni mwenye kujitolea katika kubeba jukumu lake katika dini na jamii, na ni hofu yake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndio inapasa kumsukuma kufanya hivyo:

إِنَّمَا يَخْشَى ٱللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ ٱلْعُلَمَٰٓؤُا۟ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ عَزِيزٌ غَفُورٌ ﴿٢٨﴾

**"Hakika si mengineyo wanaomcha Mwenyezi Mungu, katika waja Wake ni wale wajuzi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye maghufira."** **(Surat al-Fatwir: 28)**.

Na raghaba yake iwe ya kutaka thawabu zake na kujua kwake upeo wa changamoto na hatari ambazo zinazunguka dini na jamii. Na ikiwa anakabiliwa na baadhi ya matatizo ya maisha na vikwazo

katika njia ya kazi, ni juu yake ajipambe kwa subira na msimamo, na akabidhi yanayomkabili kwa Mwenyezi Mungu, na ahudhurishe katika akili yake na nafsi yake yale ambayo wameyavumilia Manabii na Maimamu na mawalii wema katika njia ya Mwenyezi Mungu na katika kuhudumia dini. Walivumilia njaa, ufakiri, taabu na aina mbalimbali za adha na matatizo na wala hayo hayakuwatoa katika njia ya kufanya wajibu wao wa kulingania kwa Mwenyezi Mungu:

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ لَا يُصِيبُهُمْ ظَمَأٌ وَلَا نَصَبٌ وَلَا مَخْمَصَةٌ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ وَلَا يَطَـُٔونَ مَوْطِئًا يَغِيظُ ٱلْكُفَّارَ وَلَا يَنَالُونَ مِنْ عَدُوٍّ نَّيْلًا إِلَّا كُتِبَ لَهُم بِهِۦ عَمَلٌ صَـٰلِحٌ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿١٢٠﴾

**"Hayo ni kwa sababu ya kuwa hakiwapati kiu wala taabu wala njaa katika njia ya Mwenyezi Mungu; wala hawakanyagi ardhi ichukizayo makafiri, wala hakiwapati chochote kutokana na adui, ila huandikiwa kuwa ni amali njema. Hakika Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa watendao mazuri."** **(Surat Tawba: 120)**.

Maulamaa ni warithi wa Manabii na ni manaibu wa maimamu na ni mwendelezo wa mwenendo wa daawa. Hakika anayoyaona mwanachuoni katika jamii yake miongoni mwa udhaifu wa ushirikiano na kutokujali, ni matokeo ya uchache wa maelekezo na malezi ya kidini na kiimani, na kwa hivyo hali hiyo inambebesha majukumu makubwa na wajibu mzito zaidi katika kazi ya kurekebisha na kutengeneza. Na uzoefu umethibitisha jinsi harakati na mwamko wanaouleta maulamaa na wanafunzi wa dini unavyobadilisha hali ya jamii kwa kiwango kikubwa na kuifanya ni yenye harakati zaidi na yenye uzingativu zaidiwa mambo ya kidini, nani yenye ukuruba zaidi na kujongea zaidi karibu na maulamaa.

Hiyo ni kwa sababu watu wanapoona ikhilasi, juhudi, tabia njema na ukunjufu wa moyo kwa mwanachuoni, na wakaona athari za maelekezo yake kwa watoto wao na jamii yao, na ushughulikiaji mzuri wa mambo yao na matatizo yao, hakika wao kama jamii huelekea kwake na kujongea karibu yake na humuunga mkono na kumpa msaada wao wote.

**Uitikiaji wa jamii:**

Tunapoilingania jamii kuheshimu maulama na wanafunzi wa elimu ya dini na kujongea karibu yao na kushirikiana pamoja nao, hiyo sio kwa ajili ya shakhisiya yao na wala sio kwa ajili ya kuwatimizia manufaa yao binafsi, ingawa elimu inastahiki heshima na kutukuzwa. Lakini lengo linalokusudiwa ni kuzalisha juhudi zao na kufaidika na kazi ambayo wanaifanya kwa ajili ya maslahi ya jamii.

Na inaweza kukawa na angalizo wanaloweza kulitoa baadhi ya watu kwa baadhi ya maulamaa na wanafunzi wa elimu ya dini, na linahusiana na kiwango cha elimu na utamaduni, pale wanapoona kasoro na uzembe kwa baadhi ya wanafunzi na hususan katika mabadiliko ya kifikra na kielimu ya kisasa, ambayo yanadhoofisha uwezo wao katika kuzungumza na wasomi na kizazi kilichosoma kilichofunguka kwa wakati uliopo.

Na angalizo lingine linafungamana na mwenendo na tabia katika kuamiliana, kama vile kuamiliana na baadhi ya watu kwa njia isiyo ya kujali na kuheshimu, kutumia njia ya utawala na ukandamizaji bila ya kutoa fursa ya majadiliano na mazungumzo, na kisha kutoheshimu rai na kukubali kukosolewa na wengine.

Hatuko katika muktadha wakujibu angalizo hili au kulikataa. Watu wa tabaka hili sio maasumina, ni kama kundi jingine kati ya makundi ya jamii, hivyo wanatofautiana kiwango, hivyo kuna aina isiyowajibika au isiyofaa. Utalikuta jambo hili hata kwa matabibu,

wahandisi, waalimu na wengineo, ambapo kati yao kuna waliobora, wakawaida na dhaifu katika uwezo, na kati yao wamo wenye ikhilasi na waaminifu, wazembe na wabaya. Lakini haisihi kujumuisha na kuwahukumu wote kwa ujumla kupitia aina hii au kupitia walio wengi.

Katika upande mwingine, hakika baadhi ya angalizo inawezekana kulitatua kwa nasaha na kwa mwongozo. Na baadhi ya wanafunzi wa dini wanaweza kukosa ujuzi na uzoefu kwa uchanga wa uzoefu wao wa kijamii. Hivyo anapopewa fursa ya kutosha na akapewa nasaha na ukosoaji wenye kujenga, hujikuta anavuka udhaifu na mapungufu aliyonayo.

Hakika utafiti wa kielimu na kinadharia ni jambo moja, na utekelezaji wa kivitendo wa kijamii ni jambo jingine. Vyovyote atakavyosoma mwanafunzi wa dini na akapata mafanikio, hakika bado anahitaji muda wa ujuzi na uzoefu wa kielimu ili kunoa vipaji vyake na kukamilisha shakhsiya yake. Hivyo tunapoona upungufu au udhaifu kwa mmoja wao haisihi kumuondoa katika hesabu na kumwangusha nje ya mazingatio, bali tumsaidie katika kuvuka udhaifu wake na kuondoa kasoro zake.

**Kuheshimu vipaji:**

Kati ya mambo ya kujivunia katika nchi yetu na kustahiki utukufu na kujifaharisha, ni kujitokeza kundi lenye vipaji na uwezo wa kielimu uliopevuka. Katika muda huu, wamo wanachuoni watukufu, makhatibu mahiri, wanafikra wajuzi, waandishi wenye uwezo naviongozi wapambanaji kwa ajili ya mambo ya kijamii. Na hii ni neema kubwa, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwayo, na ni wajibu tuipokee kwa namna inayostahiki kwa harakati na ushirikiano, ili vipaji hivi vichukue nafasi yake katika kuitumikia dini na nchi.

Hakika kati ya watu kuna asiyevutiwa na vipaji vya nchi yake. Daima anavutiwa na walio nje ya nchi yake tu, na wakati mwingine inatokea anapuuza baadhi ya haki za wenye vipaji kwa sababu ya matabaka au makundi. Kwa sababu yule anatoka katika familia yenye hali dhaifu au ni kutoka katika wafuasi wa Marjaa fulani, basi anapuuza nafasi yake na wala haheshimu kipaji chake. Na hii ni dhulma na kutokuwa na insafu, na ni kuinyima jamii fursa ya kunufaika na vipawa vya watu wake. Hakika Mwenyezi Mungu anahadharisha na anakataza kupunja haki, ambapo anasema:

فَأَوۡفُواْ ٱلۡكَيۡلَ وَٱلۡمِيزَانَ وَلَا تَبۡخَسُواْ ٱلنَّاسَ أَشۡيَآءَهُمۡ وَلَا تُفۡسِدُواْ فِي
ٱلۡأَرۡضِ بَعۡدَ إِصۡلَٰحِهَاۚ ذَٰلِكُمۡ خَيۡرٞ لَّكُمۡ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ ٨٥

**"Basi kamilisheni kipimo na mizani wala msiwapunje watu vitu vyao, wala msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kutengenea kwake. Hayo ndiyo bora kwenu ikiwa nyinyi mmeamini." (Surat A'araaf: 85)**.

Na aya hii imekaririwa mara tatu katika Qur'aniTukufu; katika Surat A'araaf aya 85, Surat Hud aya ya 85, na Surat Shuaraa aya ya 183. Na *bakhas*ni kupunguza haki, sawa iwe ni haki ya kimaada au ya kimaanawi, na tamko la 'vitu' linahusu pande mbili, kimaada na kimaanawi, kwa mwanadamu yeyote mwislamu au kafiri:

**Wala msiwapunje watu vitu vyao**.

## NYANJA ZINGINE ZA KAZI YA KIDINI

Mwanadamu anapoelekea kwenye elimu ya kisharia na kujiunga na mwenendo wa maulamaa wa kidini, hii ina maana kwamba ameiweka nafsi yake nadhiri kwa ajili ya kuutumikia Uislamu na amekuwa askari mwenye kujitolea kwa ajili ya kusambaza itikadi na

misingi, hiyo ni kwa sababu kujua dini na kujua hukumu zake kuna mbebesha mwanadamu jukumu la kufanya tablighi na kufundisha, kwani kujifunza dini ni utangulizi wa kuwaonya watu na kuwaelekeza, kama anavyosema (swt):

۞ وَمَا كَانَ ٱلْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُوا۟ كَآفَّةً ۚ فَلَوْلَا نَفَرَ مِن كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَآئِفَةٌ
لِّيَتَفَقَّهُوا۟ فِى ٱلدِّينِ وَلِيُنذِرُوا۟ قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوٓا۟ إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ ﴿١٢٢﴾

**“Wala haiwafalii waumini kutoka wote. Kwa nini kisitoke kikundi katika kila kundi miongoni mwao kujifunza dini na kuwaonya watu wao watakapowarudia, ili wapate kujihadhari.”** **(Surat Tawba: 122)**.

Kwa kiwango kile kile anachojifunza mwanadamu dini ni wajibu wake kutoa elimu yake kwa wengine, na kila hisa yake ya elimu inapokuwa nyingi basi ni kwa kiwango hichohicho yanaongezeka majukumu yake katika kusambaza maarifa ya dini na kufafanua hukumu zake na dhana zake. Na hususan katika nyakati muhimu, wakati unapotokea upotovu katika njia ya sawa au upotoshaji katika chochote katika misingi ya ujumbe, au wakati akili zinaposhambuliwa na shubhati za maadui na upotoshaji wa wenye kukhalifu, hakika kazi ya maulamaa na wajibu wao katika kubainisha ukweli na kutetea misingi unakuwa ni mkubwa zaidi na wadharura sana. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

إِنَّ ٱلَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَآ أَنزَلْنَا مِنَ ٱلْبَيِّنَٰتِ وَٱلْهُدَىٰ مِنۢ بَعْدِ مَا بَيَّنَّٰهُ لِلنَّاسِ فِى
ٱلْكِتَٰبِ ۙ أُو۟لَٰٓئِكَ يَلْعَنُهُمُ ٱللَّهُ وَيَلْعَنُهُمُ ٱللَّٰعِنُونَ ﴿١٥٩﴾

**“Hakika wale wanaoficha tuliyoyateremsha, katika ubainifu na uwongofu, baada ya Sisi kuyabainisha kwa watu Kitabuni, hao anawalaani Mwenyezi Mungu, na wanawalaani wanaolaani.”** **(Surat al-Baqarah: 159)**.

Imepokewa katika Hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Inapodhihiri bidaa katika ummah wangu, basi mwanachuoni adhihirishe elimu yake, kwani asiyefanya hivyo basi ni juu yake laana ya Mwenyezi Mungu."[107]

Ikiwa kazi ya mwanachuoni ni kubainisha ukweli wa kidini na kutetea misingi yake, hakika udhihirisho wa kufanya kazi hii na kubeba jukumu hili unakuwa katika muundo na sura mbalimbali na kupitia njia na mbinu mbalimbali kulingana na tofauti za nyakati, mazingira, sehemu na jamii husika.

**Nafasi ya mazoea:**

Lakini angalizo hapa ni kwamba kuna dauru iliyozoeleka na ya kuiga, aghlabu wanaifanya wale wanaojihusisha na njia ya kutafuta elimu ya dini. Mara nyingi katika Seminari za Masomo ya Dini, maulamaa na wanafunzi hujikita katika kusoma na kufundisha na kutafiti katika elimu ya Fiqhi na Usuli, na kujishughulisha na umarjaa na kutoa fatwa.

Na katika jamii mara nyingi dauru ya mwanachuoni wa kidini huishia katika mihirabu, mimbari na yanayofuatia hayo ikiwa ni pamoja na kusoma *nikah*, kuchukua haki za kisharia na kujibu mas'ala ya kifiqhi. Ndio, hili ni jukumu linalotakiwa na muhimu, haiwezekani kulipuuzia wala kuliacha, lakini jambo linalowajibisha angalizo na tahadhari ni kitendo cha mwelekeo wa huduma na uwajibikaji kukomea katika majukumu haya yaliyozoeleka na yaliyo maarufu, licha ya kuwepo nafasi na haja muhimu katika sehemu na sekta zilizobakia.

Kwa mfano katika upande wa kielimu maulamaa katika Seminari za Masomo ya Dini wanatoa juhudi kubwa, wakati wao na fikra zao katika kutafiti mas'ala ya kifiqhi na kiusuli, na wanapata

[107] *Wasailus-Shi'ah*, Juz. 16 uk. 269. Hadith ya 21538.

maarifa angavu na ujuzi wa kina katika kuchambua kila dhana na kuijadili kwa juhudi na ufanisi, na jambo hili huwafanya wapate utukufu na kujifakharisha kwa uhodari wao na ikhilasi yao ya kielimu.

**Kazi zisizo na watu:**

Lakini maendeleo makubwa katika nyanja za kifiqhi na kiusuli hayakuendana na maendelo katika nyanja za elimu nyingine za kisharia kama vile elimu ya tafsiri, hadith, aqaid, tarikh na akhlaq. Ndio, kuna jitihada binafsi zinaongoza katika baadhi ya nyanja hizi kama vile juhudi za Allammah Sayyid Muhammad Husain Tabataba'i katika tafsiri ya Qur'ani, ambapo amefanikisha tafsiri yake nzuri *al-Miizan*, kwayo akaongeza nyongeza yenye thamani ya juu katika nyanja ya tafsiri. Na vilevile Allammah Sheikh Abdul-Husain Aminiy katika nyanja ya Aqaid, katika rejea yake muhimu*al-Ghadir*, na uzingativu wa Sheikh Aghaa Buzurk Taharaniy wa kukusanya utunzi na utafiti wa ulamaa na wanafasihi wa kundi la Mashia, ambapo alifanikiwa kutoa Enklopedia yake iitwayo *ad-Dharia*. Na ni lazima pia kuashiria utafiti wa Shahidi Muhammad al-Baaqir as-Sadir wa uvumbuzi katika nyanja za falsafa, uchumi na mantiki, katika vitabu vyake vitatu *Falsafatuna*, *Iqtiswaduna*, na *al-Ususu al-MantwiqiyatiLil- Istiqraai*.

Ilikuwa inawezekana kwa Sayyid Tabataba'i, Sheikh Aminiy na Sheikh Aghaa BuzurkTaharaniy kuungana na maulamaa wa rika lao na wenzi wao, katika kushughulika na tafiti za kifiqhi na kiusuli, na kushughulika na nafasi ya kutoa fatwa na umarjaa, lakini wao waliainisha mahitaji na pengo lililopo katika nyanja nyingine, wakazielekea na wakatoa maisha yao katika kuzishughulikia, Mwenyezi Mungu awalipe kheri kwa ajili ya Uislamu na watu wake. Lakini mfano wa shakhsiya hizi ni chache mno, zinahesabiwa kwa vidole kati ya mamia ya maulamaa, wabobezi

na wahakiki hodari waliozoeleka na kuheshimiwa katika Seminari za Masomo ya Dini.[108]

Hapa nakariri tena kwamba mimi sikusudii kudharau nafasi ya mwanachuoni yeyote aliyeitumikia sharia katika nyanja yoyote ile kati ya nyanja za elimu, na wala sipingi umuhimu wa elimu ya fiqhi na usuli, wala sidharau nafasi ya kutoa fatwa na kuchukua umarjaa, lakini mimi naitakidi ulazima wa kujaza pengo la maarifa na kuendeleza utafiti wake na utatuzi wa matatizo yake na mas'ala yake, kwa daraja lile lile la kina na la uzingativu na umuhimu ambao unatolewa katika elimu ya fiqhi na usuli.

Hii ni katika upande wa Seminari za Masomo ya Dini.

**Kazi za kijamii:**

Ama katika upande wa kijamii hakika huko kuna majukumu mengi yaliyoachwa, ambayo maulamaa na wanafunzi wa masomo ya dini ambao wanafanya kazi ndani ya jamii wanapaswa kuyaelekea. Ni majukumu yasiyo ya kawaida ambayo hayajazoeleka, na si yakwenye mimbari na mihirabu, kama ilivyotangulia.

Jamii zetu zina haja ya kuwa na taasisi za utafiti na vituo vya masomo vyenye kuchunguza mazingira ya jamii na kufuatilia mabadiliko yake na kuainisha mahitaji yake ya kifikra na kimalezi. Kisha

[108] Hili ni moja ya tatizo kubwa lililopelekea Waislamu wa huku kwetu Afrika Mashariki hasa Tanzania, kubaki nyuma kimaendeleo, kwani asilimia tisini ya Masheikh na ulamaa wetu wenye kutegemewa, kama si wote, hawana ubobezi katika fani nyingine zinazoitumikia dini na jamii zaidi ya Fiqhi. Kila utakayemgusa na kumtahini utamkuta ni mzuri katika Fiqhi tena katika milango ya Ibada, na si katika milango ya Miamala pia. Jambo ambalo linawanyima ulamaa wetu fursa ya kuitumikia jamii katika medani nyingine muhimu za kijamii na kutoa maoni na suluhisho la kidini katika sekta nyingine nje ya Ibada kuu. Na hapa nakumbuka wakati nilipokuwa ningali mwanafunzi katika Seminari moja ya Masomo ya Dini, Mkuu wetu alikuwa anatafuta Walimu wa kiwango cha juu wa kuweza kufundisha katika michepuo mbalimbali, alipewa orodha ndefu ya Masheikh wakubwa wa Mkoa wa Dar es Salaam, na kila aliyezungumza naye alimjibu yeye ni mjuzi wa Fiqh, jambo liliolazimu kuleta Walimu kutoka nje ya nchi – **Mhariri**.

ziweke taratibu na mfumo wa kuelimisha na kufundisha, na kutengeneza upya fikra na dhana za Kiislamu kulingana na changamoto za kileo.

Kama ambavyo katika zama zetu hizi tuna haja kubwa ya kuwa na taasisi za habari za Kiislamu, ikiwa ni pamoja chanel na vituo vya tovuti na wavuti, na kutoa magazeti na majarida, na kuanzisha nyanja zingine za fani mbalimbali kwa ajili ya maslahi ya mambo ya Uislamu na Ummah. Hakika nyanja hizi na mfano wake inapasa kuziwekea tabaka la wabobezi wa dini, kuzijali na kujitolea kujaza pengo lake.

Lakini sehemu kubwa ya matatizo inatokana na jamii zetu kutoangalia majukumu mfano wa haya kwa mtazamo wa heshima na uzingativu ambao anaupata yule anayejitolea katika majukumu ya kawaida yaliyozoeleka (Kusalisha, kuzika, kusoma maulidi, kusoma nikah, kuchukua haki za kisharia, kujibu mas'ala ya kifiqhi, na mengineyo), na hatimaye huwa hawaungwi mkono wala kutiwa moyo wanafunzi wa sekta hizo, jambo ambalo limefanya vijana wengi wenye kutafuta elimu ya dini kuona na kuhisi kwamba hawatakuwa wametekeleza jukumu lao, kazi yao na wajibu wao, isipokuwa ndani ya majukumu na nafasi hizi zilizozoeleka (Kusalisha, kuzika, kusoma maulidi, kusoma nikah, kuchukua haki za kisharia, kujibu mas'ala ya kifiqhi, na mengineyo).

Kwa kuongezea ni kwamba nafasi hizo za kawaida zilizozoeleka (Kusalisha, kuzika, kusoma maulidi, kusoma nikah, kuchukua haki za kisharia, kujibu mas'ala ya kifiqhi, na mengineyo) zina miiko yake na udhibiti wake uliowazi, na anayejitolea katika nafasi hizohujikuta mbele ya mifano na uzoefu unaompa matumaini na kumwongezea ujuzi, na hivyo hujiona si mwenye kuingia katika kazi muhimu isiyoeleweka wala nafasi isiyojulikana.

Wakati ambapo ubobezi katika nyanja nyingine na kujitolea katika kazi mpya inakuwa ni mfano wa kujihatarisha na kujizungushia vikwazo mbalimbali, na inahitaji juhudi kubwa kuasisi na kutayarisha fursa ya kufaulu. Na hivyo hawajitolei katika hilo isipokuwa wale waliotayari kubeba majukumu na matatizo katika njia ya kutumikia malengo matukufu ya dini, na walio tayari kwa ajili ya kutengeneza jamii zao na maendeleo yake.

# OORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashariyyah
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr

20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur’an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur’an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur’an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur’ani Tukufu

42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusherehekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi

64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)

85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Huduma ya Afya katika Uislamu
97. Sunan an-Nabii
98. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
99. Shahiid Mfiadini
100. Ujumbe - Sehemu ya Kwanza
101. Ujumbe - Sehemu ya Pili
102. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
103. Ujumbe - Sehemu ya Nne
104. Kumswalia Nabii (s.a.w)
105. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
106. Hadithi ya Thaqalain

107. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
108. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
109. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
110. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
111. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
112. Safari ya kuifuata Nuru
113. Fatima al-Zahra
114. Myahudi wa Kimataifa
115. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
116. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
117. Muhadhara wa Maulamaa
118. Mwanadamu na Mustakabali wake
119. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
120. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
121. Khairul Bariyyah
122. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
123. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
124. Yafaayo kijamii
125. Tabaruku
126. Taqiyya
127. Vikao vya furaha

128. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
129. Visa vya wachamungu
130. Falsafa ya Dini
131. Kuhuzunika na Kuomboleza - Azadari
132. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
133. Kuonekana kwa Allah
134. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
135. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
136. Ushia ndani ya Usunni
137. Maswali na Majibu
138. Mafunzo ya hukmu za ibada
139. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
140. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
141. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
142. Abu Huraira
143. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
144. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
145. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
146. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
147. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
148. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
149. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)

150. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
151. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
152. Uislamu Safi
153. Majlisi za Imam Husein Majumbani
154. Uislam wa Shia
155. Amali za Makka
156. Amali za Madina
157. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
158. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
159. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
160. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
161. Umoja wa Kiislamu na Furaha
162. Mas'ala ya Kifiqhi
163. Jifunze kusoma Qur'ani
164. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
165. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
166. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
167. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
168. Uadilifu katika Uislamu
169. Mahdi katika Sunna
170. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo

171. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
172. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
173. Vijana na Matarajio ya Baadaye
174. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
175. Ushia – Hoja na Majibu
176. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
177. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
178. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
179. Takwa
180. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
181. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (a.s.)
182. Kuelewa Rehma ya Mwenyezi Mungu
183. Mtazamo kuhusu msuguano wa kimadhehebu
184. Upotoshaji Dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
185. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
186. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah kwa Imam Ali (a.s.)
187. Uongozi wa kidini – Maelekezo na utekelezaji wa Kijamii
188. Huduma ya Afya katika Uislamu
189. Historian a Sira za Viongozi Waongofu – Sehemu ya Pili
190. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3 Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

# MUHTASARI